# Nipashe

Jumatatu Desemba 16, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580102

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

CEFA

215544702




## Matapeli sasa waona fursa wafungwa waliosamehewa

UKURASA 2

RIPOTI MAALUMU:

# Simu yagharimu uhai mamilioni barabarani

• **Meseji** kinara, adhabu mpya 500,000/- ... *Endelea uk. 4*



## YALIYOMO


UKURASA WA 8

**MKONG'OTO VIJANA WA JKT WADAIWA KUUA**

BAADHI ya vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kambi ya Milundikwa...

UKURASA WA 26

**KORTINI TUHUMA KULISHA ABIRIA BISKUTI, KUWAIBIA**

WATU watatu waishio maeneo tofauti nchini, wamefikishwa Mahakama...


## Kibano watoro shuleni chaja

UKURASA 2

## Mkuu wa shule mbaroni tuhuma rushwa ngono

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store



MICHEZO | CECAFA YAMZUIA STRAIKA MGANDA UK.31 | MAONI, KATUNI UK.6

# Kibano wanafunzi watoro chawadia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha waraka kudhibiti utoro shuleni ambao pamoja na mambo mengine, utapunguza siku na kuwa chini ya 90.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki jijini hapa na Mkurugenzi Msaidizi Msingi na Uendelezaji wa Sera wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Yesse Kanyuma ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Akwilapo wakati wa kufunga Kongamano la 14 la Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSA).

Alisema siku zitapunguzwa ili kuwe na siku kidogo mwanafunzi asipoonekana shule hatua zichukuliwe haraka.

"Lengo la serikali si kumfukuza mtoto bali ni kuwataka wamalize masomo yao pale wanapoanza darasa la kwanza wafike hadi la saba na watakapoanza kidato cha kwanza wafike kidato cha nne, utoro ni tatizo tusipodhibiti utatutia doa," alisema.

Alisema waraka huo utabainisha wajibu wa wadau wote katika suala zima la utoro.

"Awali zilikuwa siku 90 mtoto asipoonekana basi anafukuzwa shule, sasa tutapunguza zitakuwa kidogo ili kudhibiti utoro," alisema.

Alisema waraka huo utaangalia ni namna gani mwalimu wa darasa, mkuu wa shule, mwalimu wa nidhamu wanaweza kutimiza wajibu wao katika suala zima la usimamizi katika suala zima la utoro katika shule.

"Taarifa zilizopo ni kwamba mtoto anapopotea shuleni wakati mwingine hakuna mawasiliano ya aina yoyote ile kati ya uongozi wa shule na mzazi au mlezi au kiongozi wa serikali eneo husika ili kujua ni tatizo gani limemsibu mwanafunzi, na kuwa mtoro katika siku zote hizo," alisema.

Alieleza kumekuwa na pengo kubwa kati ya uongozi wa shule na wazazi au walezi na mtoto mwenyewe, wakuu wa shule watakuwa wasimamizi wakuu.

Aliwataka wakuu wa shule kuwa na kamati hai za nidhamu na ushauri ili kuondoa hali ya sasa ya fukuza fukuza ya wanafunzi.

Kanyuma alisema kuanzia mwaka ujao, serikali inatarajia kuanza kutekeleza mpango wa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari kwa kujikita katika kuzalisha uchapaji wa vitabu, kuboresha miundombinu na kuendeleza walimu.

Alisema ili kutekeleza mradi huo kwa wakati, wakuu wa shule watatakiwa kusimamia miradi hiyo kwa uadilifu na uaminifu mkubwa kwani itatumia mfumo wa force akaunti ambao hautahusisha mkandarasi

Aliwahimiza kufuata sheria, kanuni na taratibu kusaidia kuleta ufanisi katika shule zao na kuondoa mlolongo wa mashauri ya walimu kwenye Tume ya Utumishi wa Walimu kwa walimu ambao wanakwenda kinyume.

Naye Kaimu Mkurugenzi Idara ya Elimu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), George Jidamva, alisema kongamano hilo lililenga kuwajengea uwezo wakuu wa shule za sekondari nchini wa kusimamia sekta ya elimu.

"Yapo mambo mengi yanalenga kuimarisha utendaji kazi, zipo changamoto zimeainishwa na zitatafutiwa ufumbuzi kama vile upungufu wa walimu wa sayansi, vitabu," alisema.



Kamanda wa Usalama Barabarani nchini, Fortunatus Muslim, akiteta jambo na mmoja wa mabalozi wa usalama barabarani eneo la Kijiji cha Bwiko mkoani Tanga, wakati wa operesheni kwa madereva wa mabasi yanayofanyakazi zake mikoa ya Kanda ya Kaskazini. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Mkuu wa shule mbaroni tuhuma rushwa ngono

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) imemkamata Mkuu wa Shule ya Sekondari Serengeti iliyoko mkoani Mara, Baraka Sabi, akituhumiwa kuomba rushwa ya ngono.

Mwalimu Sabi (41), anadaiwa kuomba rushwa hiyo kwa mwanafunzi aliyehitimu kidato cha sita katika shule hiyo mwaka 2016, ili ampatie cheti cha kuhitimu.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana kuhusu tukio hilo, alidai mwanafunzi huyo alikuwa anahitaji cheti chake ili akamilishe taratibu za kuomba ajira baada ya kuhitimu Chuo Kikuu cha Dar es Saalam (UDSM).

Alidai baada ya binti huyo kuwasiliana na mwalimu huyo, alimtaka waonane jijini Dodoma ambako alikuwa anahudhuria mkutano wa wakuu wa shule.

"Mwalimu huyo alimwambia mwanafunzi aende Pahi Hoteli iliyopo jijini hapa ili ampatie cheti hicho na alipofika, alimwambia waende katika chumba alichofikia na kumwambia ampe rushwa ya ngono ndiyo atampa cheti chake.

"Mwanafunzi baada ya kuona hivyo, alimwambia Mwalimu Baraka kuwa wafanye tendo hilo siku iliyofuata kwa sababu siku hiyo hakuwa vizuri," alidai.

Aliongeza kuwa siku iliyofuata mhitimu huyo alitekeleza sharti la kwenda kujamiiana ndipo Takukuru walipoweka mtego wao na kufanikiwa kumkamata mwalimu huyo na kuhakikisha taratibu za kisheria zinafuatwa.

Kibwengo alidai mtuhumiwa huyo ametenda kosa hilo kinyume cha kifungu 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na marejeo yake ya mwaka 2018. Alidai kosa hilo ni la jinai huku akipongeza mhitimu huyo kwa kuvunja ukimya na kuamua kuviweka wazi vitendo vya aina hiyo.

Alidai Takukuru ilifanikiwa kupata cheti cha mtoa taarifa na kuongeza kuwa uchunguzi wa suala hilo bado unaendelea ili taratibu za kisheria na hatua stahiki zichukuliwe.

Alisema Takukuru inaendelea kuwaomba wananchi kushiriki katika kampeni ya 'Vunja Ukimya, Kataa Rushwa ya Ngono' yenye lengo la kuhamasisha jamii kutoa taarifa za vitendo vya rushwa ya ngono.

# Matapeli waona fursa msamaha wafungwa

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Magereza limetahadharisha kuhusu kuibuka kwa matapeli wanaowafuata ndugu na jamaa za wafungwa walioko magerezani na kuwaomba fedha kwa ahadi ya kuwawezesha ndugu zao kunufaika na msamaha wa Rais John Magufuli. Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Amina Kavirondo, Msemaji wa Jeshi la Magereza, ilieleza kuwa matapeli hao wameibuka baada ya Rais Magufuli kutangaza Desemba 9, mwaka huu kutoa msamaha kwa wafungwa 5,533 waliokuwa kwenye magereza mbalimbali nchini.

Katika taarifa yake hiyo, Kavirondo alisema kitendo cha matapeli hao ni kinyume cha sheria za nchi, hivyo Jeshi la Magereza linautahadharisha umma kuhusiana na aina hiyo ya utapeli.

Alisema kuwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi Ibara ya 45(1)(d), mwenye mamlaka ya kusamehe wafungwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na si mtu mwingine yeyote.

"Kwa muktadha huo, mtu yeyote atakayejitokeza na kudai kuwa ana uwezo wa kusaidia ndugu aliyefungwa gerezani, kunufaika na msamaha huo, apuuzwe kwa kuwa hana mamlaka hayo na taarifa za tukio hilo zitolewe haraka iwezekanavyo katika vyombo vya sheria ili hatua stahiki za kisheria zichukuliwe dhidi yake," alisema.

HABARI KITAIFA

# Walia mbele ya Mpina kisa kutaifishwa ng'ombe 2,400

**Na Mwandishi Wetu,**
KAHAMA

WAFUGAJI wa vijiji vinavyozunguka Pori la Akiba la Kigosi Moyowosi Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga, wameangua kilio mbele ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, baada ya ng'ombe zaidi ya 2,400 kukamatwa na kutaifishwa na maofisa wa pori hilo, huku wakilalamikia kukosa msaada kutoka serikalini.

Wafugaji hao wamesema awali walikuwa wakitumia eneo la msitu wa asili wa Hifadhi ya Usumbwa lenye ukubwa ekari 94,030 lililokuwa likimilikiwa na Halmashauri ya Ushetu kihalali kwa GN Namba 442 ya mwaka 1958, lakini wakashangazwa mwaka 2002 hifadhi hiyo ya msitu ilijumuishwa katika Hifadhi ya Kigosi Moyowosi na kusababisha mifugo mingi kufa na kutaifishwa kwa kisingizio kuwa wamekamatwa ndani ya hifadhi.

Wafugaji hao walisema maeneo ambayo wafugaji wameathirika na mgogoro huo ni kata za Nyankende, Idahina, Ulewe, Ubangwe, Ulowa na Ushetu ambazo zimepakana na Hifadhi ya Kigosi Moyowosi, ambapo tangu mwaka 2016 hadi sasa zaidi ya ng'ombe 2,400 walikamatwa na kutaifishwa na kuwasababishia umaskini mkubwa.

Mmoja wa wafugaji hao, Samuel Shineneko, akizungumza huku akibubujikwa na machozi mbele ya Waziri Mpina, alisema mifugo yake aliichunga kwa miaka mingi, lakini yote imekamatwa na kushikiliwa ndani ya Pori la Akiba la Kigosi Moyowosi kwa kipindi kirefu na mingine kudaiwa kuuzwa.

Alimwomba Mpina kufikisha kilio cha wananchi hao kwa Rais John Magufuli kuwa licha ya kiongozi huyo mkuu wa nchi kuwapigania wanyonge wasinyanyaswe, bado watendaji wa serikali wamekuwa wakitumia kivuli cha uhifadhi kuwadhulumu wananchi mali zao na kubaki maskini.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Kahama, Doa Limbu, alisema mbali na changamoto hiyo ya mifugo kutaifishwa pia wafugaji wa eneo hilo wanalazimika kutembea umbali wa kilomita 40 kufuata huduma za josho na kuiomba serikali kusogeza karibu huduma hiyo katika maeneo ya Nyankende, Idahina, Ulewe, Ubagwe na Bulungwa ili kuboresha uzalishaji wa mifugo.

Kufuatia malalamiko hayo, Waziri Mpina aliwahakikishia wananchi hao kuwa serikali itaendelea kuchoma vichaka vyote vya ufisadi na dhuluma kwa wananchi wake.

Alionya kuwa mtumishi yeyote atakayetumia kisingizio cha kusimamia sheria, huku wakifanya wizi na dhuluma hatapona, na kwamba wataendelea kubainishwa na kuchukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria.

Waziri aliunda timu maalumu itakayofika eneo hilo ili kujua uhalali wa umiliki wa Hifadhi ya Msitu Usumbwa kama unamilikiwa na Halmashauri ya Ushetu au Pori la Akiba la Kigosi Moyowosi ili kumaliza mgogoro huo.

Pia timu hiyo itafufua na kuainisha mipaka upya pamoja na kuweka alama, ambapo kila mdau atalazimika kuheshimu mipaka hiyo ukiwa ni mkakati wa kumaliza mgogoro huo uliodumu kwa zaidi ya miaka 10.

Pia aliwaagiza watendaji wa serikali ngazi zote kusimamia na kuzielewa vizuri sheria zote zikiwamo za hifadhi na za mifugo ili kutenda haki katika maeneo yenye migogoro ya aina hiyo.

Waziri Mpina pia alikosoa tabia ya baadhi ya watendaji wa serikali waliopewa dhamana ya kusimamia sekta ya mifugo kujifungia maofisini, huku wafugaji wakiendelea kunyanyaswa bila msaada wowote.

Aidha, aliwataka watendaji wa sekta ya mifugo kuhakikisha wanafika kwenye maeneo ya wafugaji na kutatua changamoto zao kuliko kusubiri ziara za viongozi wa kitaifa ndipo wananchi hao watoe malalamiko yao kana kwamba hakuna mfumo rasmi wa serikali wa kughughulikia matatizo yao.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alimshukuru Waziri Mpina kwa ziara hiyo ambayo imewafungua macho kwani awali walikuwa wakiamini kwamba baadhi ya maeneo hawaruhusiwi kuhoji ikiwamo suala la mifugo kukamatwa ndani ya hifadhi.

## Mkemia Mkuu akusanya sampuli zaidi 5,000

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Kanda ya Kati, imesema katika kipindi cha miaka miwili tangu kuanzishwa kwa kanda hiyo, imekusanya sampuli mbalimbali 5,106.

Meneja wa Kanda hiyo, Musa Kuzumila, alisema hayo alipokuwa akizungumzia mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka miwili na nusu tangu kuanzishwa kwa ofisi hiyo, katika ziara ya timu ya maofisa habari wa wizara na taasisi zake mkoani hapo.

Alisema kati ya sampuli mbalimbali 5,106 zilizokusanywa kwa kipindi hicho, sampuli 36 za vinasaba (DNA) zililenga kuangalia uhalali wa watoto.

Majibu ya sampuli hizo husaidia kumaliza kesi au migogoro kwa wakati.

"Hapa sina takwimu sahihi za kinababa wangapi wamesingiziwa watoto, tumekusanya sampuli 36 za DNA asilimia 90 kati ya hizo ni za kusaka uhalali wa baba wa mtoto."

"Huwa tunapeleka kuchunguza kwenye maabara zetu zilizopo Dar es Salaam na Mwanza, tumekusanya na kufanya uchunguzi sampuli 5,106 hadi Desemba hii, tunapofanya chunguzi za namna hii inahusika moja kwa moja na kutoa ushahidi mahakamani na kusaidia kesi kutatuliwa kwa wakati," alisema.

INAENDELEA UK. 8

### KADI YA GARI IMEPOTEA

WILBERT ROBERT URIO anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.733 DJW aina ya MISTUBISHI ROSA. Yenye chasis namba BE438E41191 na Engine namba Z898HL

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi
TAARIFA POLISI: TAN/RB/7250/2019.



## RIPOTI MAALUM

# Simu inavyoua mamilioni barabarani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KILA dakika moja inayopita, uelewe kwamba kuna kati ya watu wawili hadi watatu wanafariki dunia kutokana na ajali za barabarani. Shirika la Afya Duniani (WHO) linatanabaisha hilo kupitia ripoti yake ya usalama barabarani ya mwaka jana.

Ni namna gani watu hao wanakufa? Dereva anapoandika au kusoma ujumbe mfupi wa simu (SMS) anabweteka bila kujijua na kumfanya awe katika hatari ya ajali kwa asilimia 2,300.

Vivyo hivyo, mazoea ya kuongea na simu yanamwingiza katika hatari hiyo kwa wastani wa asilimia 400 na WHO inaenda mbali zaidi kwamba kuna vifo vya watu milioni 1.35 kila mwaka kutokana na ajali hizo.

Vilevile, ubashiri wake wa kitaalamu ni kwamba, kama hatua za udhibiti hazitachukuliwa mara moja, maana yake ni kwamba hadi mwaka 2030, ambao ni ukomo wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, vifo hivyo vitafikia milioni 1.9.

Ujumbe mkuu wa wataalamu hao kutoka Umoja wa Mataifa (UN) ni kwamba, simu ni hatari maradufu kuliko hata watu wanavyoona, kudhani au chochote kile kinachoendana na kujiamini nazo, vitendo vinavyoshuhudiwa kuwa mbwembwe za kawaida hasa kwa waendesha magari madogo na pikipiki.

WHO pia inanyooshea vidole baadhi ya viashiria vya ongezeko la ajali, huenda hata vikaoanishwa na simu kwa wakati mmoja. Hapo vinatajwa mwendo kasi, ulevi wa madereva, matumizi duni ya mikanda kwa abiria na vizuizi vya watoto, kukosekana kofia ngumu na zenye viwango kwa pikipiki.

Kuna visababisho vingine vinavyotajwa kuwa mzizi wa ajali nyingi duniani ambavyo vimekuwapo hata kabla ya zama za simu ni: Makosa ya kibinadamu; uhalisia wa mazingira; ubovu wa miundombinu; na vyombo vya moto.



Dereva akiendesha gari huku mawazo yake yakitawaliwa na simu.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

### RIPOTI TCRA

Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika ripoti yake ya mwaka jana, nayo inakiri kinachosemwa na WHO ikidai kuna ongezeko kubwa la watumiaji wa simu nchini na kuchangia ajali nyingi.

TCRA inataja moja ya viashiria ni katika matumizi ya simu yanayoteka akili za watumiaji kiasi cha kuvuka barabara huku wakitumia simu, hivyo wengi wao kupata ajali zinazotokana na magari, pikipiki au baiskeli. Ripoti inaonyesha watumiaji wa simu wameongezeka nchini kutoka milioni 27.6 mwaka 2013 hadi kufikia milioni 43.6 mwaka jana.

Takwimu za TCRA zinabainisha kasi ya ongezeko la matumizi ya simu nchini kwa mwaka na idadi yao katika mabano: 2014 (milioni 34.2); 2015 (milioni 39.8); 2016 (milioni 40.1); na mwaka 2017 (milioni 40.08). Maana yake ni kwamba ndani ya kipindi cha miaka minne, kuna ongezeko la watumiaji wa simu milioni 12.48.

Mwanasheria wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Deus Sokoni, analalamika kwamba hadi sasa nchini, hakuna sheria madhubuti kudhibiti pengo hilo la kisheria katika matumizi ya simu za mikononi kwa watumiaji wa barabara.

Analinganisha, hali ilivyo tofauti na nchi zingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), husussan Kenya na Uganda anakokutaja tayari kuna sheria hizo.

Sokoni anatetea hoja yake, kwa simulizi ya ushuhuda kwamba matumizi ya simu kwa madereva huwaondolea umakini na kuwaishia kwenye ajali.

“Hivi sasa simu ni janga sana barabarani! Mtu anaendesha huku ‘anachati’ au kuongea na simu. Matokeo yake ajali inatokea kutokana na uzembe wake,” anasimulia kinachojiri barabarani.

Mwanasheria huyo wa Polisi anaendelea: “Nimewahi kushuhudia gari likigongwa na dereva wake anakufa huku ameshikilia simu mkononi hii inaonyesha simu ndiyo chanzo cha ajali.

“Unakuta dereva wa basi anaendesha huku anaongea na simu, anashindwa kujua amebeba roho zingine za watu, kama akikutana na kitu cha kusababisha ajali, si rahisi kukwepa, kwa kuwa umakini wake utakuwa umepungua.

“Lazima tuwe na sheria kali ya kudhibiti hali hii, hasa ikizingatiwa kwa sasa watumiaji wa simu wanaongezeka siku hadi siku.

“Sheria yetu ya sasa ya usalama barabarani iliyotungwa mwaka 1973, haina kipengele cha kupiga marufuku simu, lakini sasa tunakuja na sheria mpya itakayodhibiti hali hii.”

Hata hivyo, Sokoni anarejea takwimu za ajali za miaka mitano hadi mwaka jana, kwamba kiwango cha ajali kwa ujumla kinaendelea kushuka.

Anafafanua kwamba mwaka 2013 kulikuwa na ajali 24,480 zilizosababisha vifo vya watu 4,091; mwaka 2014 zilikuwapo ajali 15,420 zilizoua watu 3,857; na mwaka 2015 zilikuwapo 8,777 na kuua watu 3,574.

Mwaka 2016 ulikuwa na ajali 10,297 zilizoendana na vifo 3,381; mwaka 2017 ajali 6,022 zenye vifo 2,705; na mwaka jana ulikuwa na ajali 3,988, vifo vyake vikiwa 1,912.

Sokoni anaeleza kinachofanyika katika nchi zingine zilizochukua hatua, ambako kuna marufuku ya matumizi ya simu dereva anapokuwa barabarani na panapokuwapo ulazima, anashauriwa kuegesha pembeni chombo cha moto ili amalizane na dharura ya simu.

### KIBANO CHAJA

Mwanasheria huyo anadokeza maudhui ya muswada ujao wa marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani, katika mambo kadhaa ikiwamo matumizi ya simu, akitamka kwamba: “Tumependekeza adhabu iwe Sh. 500,000 dereva akikutwa anaendesha huku anatumia simu.”

Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Fortunatus Muslim, anasema marekebisho ya sheria hiyo kwa sasa yako ‘jikoni’ yakishushughulikiwa kabla ya kufikishwa katika mamlaka rasmi za kutunga sheria. “Tunatarajia mwakani (2020) kabla ya Bunge la Bajeti, sheria itakuwa imepitishwa na itasaidia kusimamia yale yote ambayo tumeona yana upungufu kwenye sheria ya sasa,” anasema.

Kamanda Muslim anaoanisha vita hivyo dhidi ya ajali na ufanikishaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayonuia kupunguza ajali kwa kiwango cha asilimia 50 ifikapo mwaka ujao, ambao ndiyo unatarajiwa maboresho hayo ya kisheria yatakuwa yameanza kufanya kazi.

### WADAU, WANAHARAKATI

Mratibu Mradi wa Usalama Barabarani wa Chama cha Waandishi Wanawake (Tamwa), Gladness Munuo, anaelekeza malalamiko yake kwenye Sheria ya Usalama Barabarani nchini iko kimya dhidi ya matumizi ya simu barabarani.


“Ni vyema sheria iwe wazi ili mtu asitumie simu akiwa barabarani, ifahamike kuwa, matumizi ya simu barabarani yanatufanya tusione alama za barabarani, tusione taa nyekundu, yanaufanya ubongo ulegee,” analalamika.

Pendo William, anayejitambulisha kuwa mtumiaji wa barabara na mkazi wa Maili mbili jijini Dodoma, anakiri hatari waliyonayo watu wanapoendekeza kutumia simu barabarani.

“Unajua hizi simu sijui tunanogewa mtu hadi anajikuta anaingia barabarani ameshikilia simu, hadi anapigiwa honi,” anaeleza uzoefu wake, huku akianisha upande wa pili wa waendeshaji vyombo vya moto kwamba:

“Kuna siku nimesimama eneo la kuvuka la pundamilia, dereva hata haangalii sisi watembea kwa miguu tunahitaji kuvuka, yupo ‘bize’ na simu. Hawa ndio wanajikuta wanagonga watu barabarani, hii ni hatari inayokuja kwa kasi.”

Mkazi wa Nkuhungu, Job Mndolosi, ana simulizi inayotetea ukweli wa kutumia simu kunavyohamia kwenye ajali, akisema: “Kunawaponza wengi, mtu anavuka barabara huku ‘anachati’, anaendesha ‘anachati’. Hivi usalama wa hawa ukoje barabarani zaidi ya kujikuta wanakumbana na ajali?”



## HABARI KITAIFA



Wananchi wa Kijiji cha Munkawa, Kata ya Rungwa wilayani Manyoni, mkoani Singida wakivuka kwenye daraja la Mto Musa baada ya maji ya mvua kupungua. **PICHA: JUMBE ISMAIL**

# BoT yatoa elimu utunzaji fedha

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imewataka Watanzania kutunza vizuri fedha zao ili kuliepusha taifa kuchapisha noti mpya kila mara.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Meneja Msaidizi wa Idara ya Uhusiano wa umma kutoka BoT, Vick Msina, wakati akizungumza na madereva bodaboda na majaji mjini Babati.

Alisema mtu anapotunza vibaya fedha yake kwa kuikunja, kuiweka kwenye soksi au sehemu yoyote yenye unyevunyevu fedha hiyo inawahi kuharibika na kusababisha serikali kutumia gharama kuchapisha noti mpya.

"Iwapo watumiaji wa fedha watakuwa makini katika kuhifadhi na kuitunza, kuikunja au kuiweka sehemu yenye majimaji wataisaidia serikali kuokoa gharama za kuchapisha na fedha ambayo ingetumika itaenda kujenga shule, hospitali, barabara na kuwalipa walimu wetu," alisema Msina.

Alisema lengo la kuileta elimu hiyo imetokana na Jeshi la Polisi kuiomba BoT kutoa elimu kwa askari wake kuhusu utambuzi wa noti bandia, lakini benki hiyo waliona ni vizuri watoe elimu hiyo kwa makundi mengine kama vile bodaboda, wafanyabiashara na wajasiriamali. Alizitaja njia bora za kutunza noti kuwa ni kuhifadhi noti au sarafu katika pochi ili zisipate mikunjo au uchafu, zihifadhiwe sehemu safi isiyo na unyevunyevu, vumbi, kemikali, rangi au vyombo vya kutoa rangi.

Alizitaja njia mbaya za kutunza noti ni pamoja na kukunja au kufinyanga mkononi, kuchimbia noti au sarafu ardhini, kuweka kwenye nguo za ndani au kuzifungia kwenye kona ya kitenge au kanga.

Naye Meneja Msaidizi Idara ya Sarafu, Abdul Dolla, alisema noti ya Sh. 10,000 ambayo ni feki ikishikwa kwa pembeni inakwaruza au picha ya Nyerere kwenye mashine inakuwa kama katuni.

Ofisa mmoja wa BoT aliyefahamika kwa jina moja la Minja alisema mtu anapoitunza vibaya noti anaiingizia hasara serikali kwa kuwa fedha ikishachakaa ikirudishwa Benki Kuu huwa hairejeshwi kwenye mzunguko.

Kwa upande wake Joseph Laizer, alimwambia mtaalamu huyo wa fedha kuwa noti ya Sh. 500 haina ubora. Minja alimjibu kuwa noti hiyo ilikuwa na ubora, lakini inatumika kuliko noti zingine za Sh. 5,000, 10,000, 2,000 na 1,000 ndiyo maana inachakaa haraka.

Juma Ramadhani akizungumza na Nipashe kuhusu elimu hiyo alisema BoT imefanya vizuri kuwafuata na kuwapa elimu hiyo ambayo pia itasaidia kubaini matapeli walioku-wa wanawapatia fedha bandia.

# Zanzibar kukamilisha sheria ya Diaspora kabla ya 2020

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR



RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein (pichani), amewahakikishia wanadiaspora kuwa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) itasimamia na kuhakikisha sheria ya Diaspora inakamilika kabla ya Mei, mwakani.

Dk. Shein alitoa kauli hiyo jana mjini Zanzibar alipokuwa akifungua rasmi kongamano la sita la Diaspora ambalo limeandaliwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi-Zanzibar.

Dhamira ya kongamano hili ni kuendeleza ushirikiano uliopangwa na Diaspora na wawekezaji kama wadau wa maendeleo nchini chini ya kauli mbiu ya "mtu kwao ndio ngao".

Alisema mwaka jana alielekeza jitihada za kuanziasha ofisi za Diaspora Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wakati ule kwa kuanziasha Diaspora.

"Kutokana na kutambua umuhimu wa Watanzania waishio nje ya nchi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliunda idara maalumu ya kushughulikia masuala ya Diaspora katika Wizara ya Mambo ya Nje mwaka 2010 ili kuvitekeleza kwa vitendo azma yetu ya kuwashirikisha Wanadiaspora Tanzania katika kuendeleza nchi yetu," alisema Dk. Shein.

Aliongeza kuwa kwa umuhimu huo huo, na kwa kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 na kuyapa nguvu masuala ya Diaspora, kilianzishwa kitengo cha Diapora na baadaye Idara ya Diaspora ilianzishwa Zanzibar.

Tulitengeneza sera maalumu ya wanadiaspora, na sasa tupo mbioni kuanzisha sheria ya Diaspora, nimefurahi kuwa rasimu ya sheria hiyo imefikia katika hatua nzuri," alisema Dk. Shein.

"Kwa mantiki hiyo basi, namwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Issa Haji Ussi Gavu kuhakikisha anasimamia kwa karibu sana utayarishaji na kukamilika kwa rasimu ya sheria hiyo na iwasilishwe kwenye Baraza la Wawakilishi kabla ya Mei 2020," alisema na kuendelea:

"Atahakikisha kuwa kabla ya kumaliza muda wangu wa urais hapa Zanzibar sheria hiyo itakuwa imekaa vizuri kimkakati, kisera pamoja na kisheria kwa upande wa Zanzibar."

Aidha, Rais Shein, aliwapongeza wanadiaspora kwa michango yao ambayo wamekuwa wakiitoa kwa kusaidia serikali, pamoja na mambo mengine michango hiyo imekuwa ikisaidia kijamii na kiuchumi.

Awali akitoa salamu za wanadiaspora, Mwenyekiti wa wanadiaspora, Norman Jasson, alisema mchakato wa sera ya Diaspora umekuwa ni wa muda mrefu na kumekuwapo na ukimya takribani miaka mitatu na kumwomba Rais Shein kuwasaidia kusimamia zoezi hilo.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu zitangulize maslahi ya wachezaji dirisha dogo

**HATIMAYE** dirisha dogo la usajili kwa klabu za Tanzania Bara kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyao, limefunguliwa rasmi leo kabla ya kufungwa ifikapo Januari 15, mwakani.

Kufunguliwa kwa dirisha hilo ni nafasi pekee kwa klabu husussan za Ligi Kuu na Daraja la Kwanza kuboresha idara ambazo zilikuwa zimepwaya ama kuandamwa na majeruhi.

Tayari baadhi ya klabu tangu wiki iliyopita zilianza kutiliana saini mikataba na wachezaji wapya inaowataka kabla ya dirisha hilo kufunguliwa leo, lakini pia zikitangaza kuvunja mikataba na nyota wao wengine.

Tunatambua katika dirisha hili kama lilivyo lile kubwa, pia wapo wachezaji ambao watatemwa ili kutoa nafasi kwa nyota wapya ambao klabu husika zinaamini wanaweza kuzisaidia kutimiza malengo yao.

Hata hivyo, kutemwa huko hakuwezi kuwa safari ya mwisho kwao kisoka kwani upo msemo wa wahenga usemao "ukisema wa nini, wenzako wanajiuliza watampata lini".

Katika hilo, tunaushahidi wa kutosha kwa baadhi ya wachezaji ambao wamewahi kuonekana hawafai na kutemwa, lakini baada ya kwenda kwingineko wakang'ara na baadaye kusajiliwa tena na klabu zilizowatema awali.

Kwa mantiki hiyo, wachezaji watakaotemwa hawana budi kutambua hayo ndiyo maisha ya soka na kinachotakiwa ni kupambana zaidi kwa klabu zitakazowasajili ili kuthibitisha ubora wao.

Aidha, tunafahamu wazi zipo klabu ambazo zimetega mitego yao zikisubiri wachezaji watakaotemwa hususan kutoka kwa klabu kubwa ili ziwasajili. Katika hilo, Nipashe tungependa kuona klabu zikitangulia kwanza kutangaza wachezaji zinaowatema kabla ya kuanza kusajili wapya ili kuwapa fursa ya kujiweka sokoni mapema.

Hatutarajii kuona wachezaji wakutemwa katika dirisha hili wakiwa wa mwisho kutangazwa baada ya klabu husika kufanya usajili kwa kuwa kufanya hivyo si kuwatendea haki.

Lakini ni wakati wa wachezaji ambao walikuwa hawapati nafasi katika vikosi vya kwanza kuomba kuondolewa ili kuokoa viwango vyao na vipaji kwa ujumla.

Tunatambua wapo wachezaji ambao walishawishika kusajiliwa na baadhi ya klabu kutokana tu na fedha ama ukubwa wa klabu na baadaye kujikuta wakisugua benchi katika kila mechi ama kuishia kupata nafasi chache dimbani wakitokea benchini.


Hivyo, wachezaji kama hawa, hawana budi kuomba kuondoka ama kutolewa kwa mkopo badala ya kuendelea kusugua benchi ama kusubiri kucheza wakitokea benchini.

Kwa maana hiyo hatutarajii kuona kunakuwa na klabu zitakazowabania wachezaji ambao hawapati nafasi kuondoka ama kuwatoa kwa mkopo kama wanamalengo nao kwa baadaye.

Tunayasema hayo kutokana na kutambua kuwa soka kwa sasa ni biashara na kwa wachezaji hiyo ni sehemu ya maisha na ndiyo kila kitu kwao katika kuendesha maisha ya kila siku.

Hivyo, tunatarajia kuona usajili wa dirisha hili kanuni na sheria zikifuatwa, lakini kwa klabu zikitanguliza mbele maslahi ya wachezaji wao kwa kuwasikiliza maoni yao hususan wale wasiopata nafasi katika kikosi cha kwanza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Uwekezaji pekee ndiyo suluhisho kwa Yanga

**VIONGOZI** wa Yanga wamekiri kuwa hali ya kifedha kwenye klabu yao si nzuri. Akizungumza na waandishi wa habari hivi majuzi, Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Dk. Mshindo Msolla, alisema klabu hiyo imegubikwa na madeni lukuki, ikiwa inadaiwa na makocha kadhaa na wachezaji waliopita na waliopo.

Akaongeza hata pesa zilizopatikana kwenye hafla ya "kubwa kuliko" haikutosheleza chochote, na badala yake ilitumika tu kusajili baadhi ya wachezaji wapya ikaisha.

Dk.Msolla akabainisha kuwa hata pesa zilizotarajiwa, hazikupatikana zote kwani kuna baadhi ya wadau walioahidi hawakutimiza ahadi yao, hivyo lengo halikufikiwa.

Kwanza kabisa nipende kumpongeza Dk. Msolla kwa kuuweka ukweli wote hadharani, badala ya kufichaficha na kuonekana kuwa klabu haina matatizo, kumbe mambo hayaendi sawa.

Inawezekana kuwa aliamua kuweka mambo hadharani baada ya kuonekana kama kuna baadhi ya wanachama na mashabiki wameanza kuhoji pesa za hafla ya kubwa kuliko zilipokwenda.

Nadhani kama mwenyekiti na uongozi ungekaa kimya, ina maana dhana ya wanachama na mashabiki ingeweza kutafsiriwa kuwa ni kweli, huenda pesa nyingi zilizopatikana na hazikutumika ipasavyo.

Hata hivyo, pamoja na kuwekwa ukweli hadharani, lakini uongozi wa Yanga chini ya Dk. Msolla si kwamba umetua mzigo, bali hiyo ni hatua ya kwanza ya kuwatuliza Wanayanga na wanachopaswa kuendelea kufanya ni kuiongoza klabu hiyo na kupunguza baadhi ya madeni.

Yanga haipaswi kuendelea kuwa hivyo ilivyo, bali kama viongozi wanapaswa kutafuta njia za kuweza kuifanya iendelee kusonga mbele.

Siku hiyo hiyo, akiongea na waandishi, mwenyekiti huyo alisema kuwa klabu ya Yanga itabadili mfumo na kuelekea kwenye hatua ya uwekezaji. Hatua hiyo inatarajiwa kufanyika Mei mwakani.

Kama ni kweli Yanga imedhamiria hivi, basi huu ndiyo utakuwa mwarobaini wa matatizo yote inayopitia klabu hiyo kongwe kabisa hapa nchini.

Huu ndiyo mfumo ambao watani wao wa jadi, Simba wameshaingia licha ya matatizo lukuki waliyopita ya kujikwamisha wenyewe, kukwamishwa na kubezwa.

Ndiyo mfumo unaotumiwa na klabu nyingi za soka duniani. Mtindo au mfumo wa kuendesha klabu kisiasa au kijamaa umepitwa na wakati kwa kiasi kikubwa na Simba imeanza kuonyesha mfano kwa hapa Tanzania.

Soka ni ajira, lakini bado klabu za Tanzania zilikuwa zikiendelea kuongozwa kijamaa, wakati nchi nyingi zilishaondoka huko.

Kwa sasa wachezaji wanalipwa kwa sababu ni ajira, lakini Tanzania klabu zinaendelea kuongozwa kwa mtindo ule ule wa kijamaa, wachezaji wakipata posho tu, huku wakiwa wanafanya kazi kwenye mashirika na kampuni mbalimbali za serikali na binafsi, hivyo michezo ilikuwa ni baada ya kazi.

Wachezaji wa sasa hawafanyi kazi, kazi yao ni soka, hivyo wanapaswa kulipwa mishahara, kwa hio klabu ni lazima sasa izalishe pesa kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi wake.

Ingawa Yanga inaweza kupata tabu kidogo kuliko Simba kwa sababu wenzao walianza kupata mwekezaji kabla ya kuingia kwenye mfumo, lakini wanaweza kwanza kubadilisha katiba ambayo itaanza sasa kuruhusu mwekezaji kuwekeza.

Kama ni umaarufu, wanachama na mashabiki pia Yanga inao kama wenzao wa Simba, kwa nini hilo lishindikane?

## BARUA & MJADALA

# Machinga punguzeni kero

**Mhariri,**

*KATIKA moja ya kada ambazo ni bayana ziko katika kundi la wanufaika wa awali mara tu, Rais Dk. John Mafuguli alipoingia Ikulu ni kada ya wajasiriamali wadogo, maarufu Machinga.*

*Hawa huko nyuma walikumbana na mengi ya kuwakwaza kibiashara, wakiangukia kuendesha shughuli zao kwa ubabaishaji wakiwa na woga wa kukamatwa na mara nyingine hata kudhulumiwa vyao.*

*Sasa wamekingiwa kifua cha haki yao wasinyanyaswe na katika suala la kodi, wamewekewa utaratibu maalum wa kuwa na vitambulisho malaum vitokanavyo na malipo ya ya Sh. 20,000 kwa mwaka, inayowanyima uwezekano wa bugudha aina yoyote.*

*Lakini, wanasema binadamu anapotetewa na kusimamiwa haki zake anapaswa 'kujiongeza' ili mambo yawe sawia.*

*Nimeshuhudia baadhi ya ndugu zetu wengi Machinga, katika maeneo mbalimbali mijini nikipataja kwa upekee Dar es Salaam, ambako kuna biashara zinazotapakaa na kuharibu utaratibu uliopo.*

*Hata kama Machinga hawajakumbushwa na mamlaka zinazowahusu na jamii zinazowazunguka hapo kwenye shughuli zao, zinapaswa kujiweka sawa kimazingira wafikie hatua hawawapi kero wakazi wa mazingira yao.*


*Tujiulize jijini Dar es Salaam, maeneo kama Mtaa wa Congo, muda wote miaka nenda rudi kumetawaliwa na vurugu za kibiashara. Hao ni Machinga, vurugu zao zitaisha lini?*

***Zainabu Katembilolo,***
***Upanga Mashariki,***
***Dar es Salaam.***

# WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Mo kajenga uwanja, Simba jengeni ukuta




**Na Adam Fungamwango**

WANACHAMA na mashabiki wa Simba kutoka pande mbalimbali za Dar es Salaam na mikoa ya jirani wiki moja iliyopita walifurika kwa wingi kwenye viwanja vyao vya Bunju kushuhudia makabidhiano na ufunguzi wa Uwanja wa Simba Mo Arena.

Eneo hilo ambalo kwa kawaida huwa ni tulivu, lilibadilika na kuwa lenye pilikapilika nyingi kutokana na wingi wa umati wa watu waliofurika kushuhudia wenyewe viwanja vyao vipya.

Ilikuwa ni kama sikukuu, magari yalifurika kukiwa pia na neema kwa wafanyabiashara ambao nao walisafiri kutoka sehemu mbalimbali, wengine ni maeneo jirani kuuza vitu mbalimbali ambavyo waliona vitanunulika kwa urahisi kwenye ugeni huo, vikiwamo vyakula, matunda, maji pamoja na jezi.

Bunju ilichangamka, wanachama na mashabiki walipojionea wenyewe viwanja viwili, cha nyasi bandia na nyasi asili.

Ilikuwa ni historia. Vizazi vyao vilivyopita havikuwahi kushuhudia kitu hicho. Tangu kuanzishwa kwa Simba mwaka 1936, haikuwahi kuwa na uwanja wake wa kufanyia mazoezi. Leo kizazi hiki kimepata bahati ya kushuhudia klabu hiyo kongwe kwa mara ya kwanza ikimiliki uwanja wake, kitu ambacho watakuja kusimulia wajukuu zao kuwa walishuhudia wenyewe ufunguzi wa viwanja vyao baada ya babu zao kuhangaika miaka na miaka bila mafanikio.

Kilichofanyika Bunju ni heshima kwa klabu yote ya Simba, ikiwamo wanachama, mashabiki, viongozi na mwekezaji wao Mohamed Dewji 'Mo', pamoja na nchi ya Tanzania kwa ujumla.

Wanachama na mashabiki wa Simba hawajatoa pesa yoyote kwa ajili ya ujenzi wa uwanja huo, tofauti na klabu ya Simba ambayo ilijengwa kwa michango ya wanachama na mashabiki wake.

Kwenye Mkutano Mkuu wa klabu hiyo, Dewji alisema kuwa baada ya kukamilika awamu ya kwanza ya ujenzi, sasa klabu inakwenda kwenye uwamu ya pili ambayo itamshirikisha mwenyewe, lakini sasa wanachama na mashabiki wanatakiwa nao wafanye kitu.

Wachangie ili wawe sehemu ya mafanikio ya klabu kama vile wazee wa sasa wanavyojinadi kuwa walichangia pesa zao wenyewe kwenye ujenzi huo wa majengo ya Simba, wengine wakienda mbali kabisa na kusema walibeba hadi matofali.

Mo, anasema kuwa zinahitajika kiasi cha Sh. bilioni mbili hivi za kujenga hosteli kwa ajili ya kambi ya wachezaji pamoja na kituo cha kuzalisha wachezaji vijana.

Akasema yeye binafsi kama mwanachana wa Simba atatoa Sh. milioni 500, na kilichobaki wanachama na mashabiki wa klabu hiyo wanatakiwa wajazie ili mradi huo au awamu ya pili ya ujenzi ukamilike.

Wala haipingiki kuwa mafanikio ya awamu ya kwanza asilimia 90 na huenda zaidi, yamefanikishwa na Mo mwenyewe.

Kinachotakiwa sasa kwa wanachama na mashabiki wa Simba si kumuunga mkono Mo, bali kuchangia ili wawe sehemu ya mafanikio ya klabu na kila mmoja aje kujivunia baadaye.

Mara nyingi watu huwa wagumu kuchangia kama wanaona hakuna chochote ambacho kimeanza, lakini kwa hili ambalo limeonekana hasa viwanja, linachagiza watu kujitokea kuchangia bila ya kuwa na kinyongo wala wasiwasi.

Niliona hali ilivyokuwa Bunju, kwani umati uliokuwa pale baada ya kushuhudia wenyewe kwa macho yao, Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara alipowaambia tu kuwa sasa suala la ujenzi wa ukuta utakuwa ni juu ya wanachama na mashabiki, walitaka kuchangia hapo hapo, lakini Ofisa Mtendaji Mkuu, Senzo Mazingisa alizuia na kutaka kuwe na utaratibu maalumu na rasmi wa kuchangia na si kama vile walivyotaka kufanya hapo kwa hapo.

Hili la ukuta inaonekana linatakiwa liwe la haraka zaidi kwani Kocha Mkuu, Sven Vandenbroeck ameangalia mazingira ya uwanja na kusema kuwa hahitaji mashabiki wakati wa mazoezi, hivyo ukuta pekee unaonekana kuwa ndiyo itakuwa tiba ya jambo hili.

Wanachama na mashabiki wa Simba wakumbuke kuwa klabu yao itajengwa na wao wenyewe, kwani wanamiliki kwa asilimia 51, huku mwekezaji ambaye yeye ana asilimia 49, hivyo si kila kitu kumuachia yeye peke yake.

Uthubutu wa mwekezaji kuanza kutekeleza ahadi zake na kuonekana kwa wanachama na mashabiki, uwe chachu ya wao kuchangia bila matatizo kwa sababu tayari kwa macho yao wameshaanza kuona dalili za mafanikio.

Itakuwa si vizuri Mwanasimba kuwa na mawazo ya kumwachia kila kitu mwekezaji afanye, huku wanachama na mashabiki wakiwa hawafanyi kitu chochote kana kwamba timu ni ya Mo, wakati pande zote mbili zina ubia, hivyo kila mmoja ana wajibu wa kuijenga Simba.

Kila mmoja anatakiwa awe ni mmoja watu walioleta mafanikio kwenye klabu ya Simba, Mo kwa nafasi yake, wanachama na mashabiki nao kwa nafasi zao ili kila mmoja ajivunie kwa kuitoa ilikotoka na kuipeleka inakotakiwa.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Mkong'oto vijana wa JKT wadaiwa kuua mwanakijiji

**Na Mwandishi Wetu,**
SUMBAWANGA

BAADHI ya vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kambi ya Milundikwa wilayani Nkasi mkoani Rukwa, wanadaiwa kuvamia kijiji cha Kipande na kupiga wananchi hadi kumuua mkazi mmoja wa kijiji hicho.

Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Justine Masejo, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo lililotokea juzi jioni kijijini hapo, baada ya vijana wawili ambao ni Sabato Mbalamwezi (35) aliyeuawa na Renatus Wankamba (37) kukamatwa na kuhifadhiwa kituo cha polisi kwa tuhuma ya kuiba simu ya kiganjani yenye thamani ya Sh. 25,000.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kipande, Vitus Majaliwa, alisema watuhumiwa hao wakiwa kituo kidogo cha polisi kijijini hapo walifika vijana watano wa JKT na kuanza kuwapa adhabu wakiwatuhumu kuwa wameiba simu ya mwenzao.

Inaelezwa kuwa wakati wakiwapa adhabu za kijeshi, ndipo mmoja alizidiwa na kuzimia ambapo walimchukua na kumpeleka zahanati ya Kalangasa ambako alifariki dunia muda mfupi kabla ya kupatiwa matibabu.

Alisema kutokana na hali hiyo, baadhi ya ndugu wakiwamo wanakijiji walihamaki na kuanza kuwashambulia vijana wa JKT hali iliyosababisha mmoja wao kupigwa na kuumizwa hadi kukimbizwa katika zahanati hiyo kwa ajili ya matibabu.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, baada ya kupigwa kijana huyo wa JKT kundi la askari hao walivamia kijijini hapo na kuanza kusaka wanaume kwenye kila nyumba na kutembeza mkong'oto kwa kila waliyemkuta.

Alisema hali hiyo ilisababisha baadhi ya vijana wa kiume kijijini hapo, kuzikimbia familia zao na kuelekea kusikojulikana ambako walilazimika kulala huko kwa kuwa askari hao waliendesha msako usiku kucha katika nyumba za wakazi wa kijiji hicho.

"Hali ilikuwa mbaya sana...vijana wa JKT wamepiga sana watu jana jioni, na usiku, kuna vijana kama 20 wamelazwa katika zahanati yetu hapa kijijini wengine wamepelekwa Sumbawanga kwa matibabu zaidi," alisema.

Kamanda Masejo alisema vijana watano wa JKT waliosababisha kifo cha Mbalamwezi wanashikiliwa na Polisi kwa mahojiano zaidi kabla ya kupelekwa mahakamani. Pia wanakijiji 35 waliofanya fujo dhidi ya wanajeshi hao walihojiwa na kudhaminiwa.



Wafanyabiashara wa sekta ya usafirishaji waliohudhuria hafla ya uzinduzi wa magari ya kisasa ya mizigo aina ya Hongyan wakishuhudia moja kati ya magari hayo. Kampuni ya MFK Automobile Tanzania kwa kushirikiana na Hongyan ya China walizindua magari hayo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkemia Mkuu akusanya sampuli zaidi 5,000

**INATOKA UK. 3**

Vile vile, alisema asilimia kubwa ya sampuli hizo zilikuwa ni dawa za kulevya hususan bangi wamezipokea kwa kiasi kikubwa.

"Sampuli ambazo tunachukua ni pamoja na dawa za kulevya, mazingira kutoka kwenye viwanda kuangalia namna wanavyochakata majitaka kwenye viwanda kabla ya kutoka kwenye mazingira ya nje, zingine ni vinasaba kuangalia uhalali wa baba wa mtoto, pia kuangalia sumu," alisema. Alifafanua kuwa kanda hiyo inahudumia mikoa mitano ya Dodoma, Iringa, Morogoro, Singida na Tabora na kumekuwapo na mafanikio mengi tangu kuanzishwa kwake.

"Tunashukuru serikali ya awamu ya tano kuanzisha hii kanda kwa kuwa tumejionea mafanikio mengi ikiwa ni pamoja na kukagua maeneo 360 ambayo yanajihusisha na masuala ya kemikali," alisema.

Alisema katika ukaguzi huo wamebaini upungufu mbalimbali na kutoa elimu kwenye mambo waliyoyakuta ikiwamo utunzaji na kuweka miundombinu sahihi ya kemikali.

Kuhusu utoaji vibali vya kusafirisha kemikali, Kuzumila alisema kwa kipindi hicho wametoa vibali 139 vya kuingiza na kusafirisha kemikali kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Kadhalika, alisema ifikapo mwaka 2028 serikali itapiga marufuku matumizi ya zebaki.

"Bunge limeshapitisha mkataba ambao unazuia matumizi ya kemikali ya zebaki, ambayo inatumika sana na wachenjuaji wadogo, kuna madhara makubwa na mkakati uliopo ni kutoa elimu ili kujua madhara na namna ya kutumia kabla ya kipindi cha kupiga marufuku, na ifikapo 2028 tutapiga marufuku," alisema.

Alieleza kuwa kinachofanyika kwa sasa ni kutoa elimu ya kemikali mbadala na kuwa na miundombinu ambayo haitaruhusu kusambaa kwa kemikali kwenye mazingira.

# TPA yakamilisha ukarabati bandari

**Na Elizabeth Zaya,** BUKOBA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA), imekamilisha uboreshaji wa awamu ya kwanza ya Bandari ya Bukoba.

Meneja wa Bandari za Ziwa Victoria, Morris Mchindiuza, alisema mwishoni mwa wiki kuwa bandari hiyo ni miongoni mwa kubwa sita zilizo chini ya TPA katika eneo la Ziwa Victoria.

Alisema bandari hiyo ilijengwa wakati wa ukoloni mwaka 1945, ikiwa chini ya Shirika la Reli (TRC) pamoja na la Bandari la Afrika Mashariki hadi mwaka 1977, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ilipovunjika.

"Baada ya jumuiya kuvunjika, bandari iliwekwa chini ya TRC na ilipofika mwaka 1997, ikawa chini ya Kampuni ya Huduma za Meli Tanzania (MSCL), ambao nao waliendelea kuhudumia bandari hii mpaka mwaka 2004 baada ya kuundwa kwa Sheria ya TPA.

"Na katika maboresho haya, tumetumia gharama ya Sh. milioni 565 kwa kazi hii ya kuhuisha jengo la abiria pamoja na jengo la utawala.

"Kwa sasa, kila kitu kimekamilika na tunaendelea pia na ukarabati wa majengo ya kuhifadhia mizigo, ujenzi ambao upo katika mradi mwingine wa uboreshaji wa miundombinu ya bandari kwa eneo la Bukoba, Kemondo, Mwanza Kaskazini na Kusini," alisema.

Aliongeza kuwa bandari hiyo ni chachu ya wafanyabiashara wa Mkoa wa Kagera, hususan Bukoba Mjini, ambao wanajishughulisha na biashara ndogo na wakulima ambao wamekuwa wakisafirisha mazao yao kwenda kwenye soko la Mwanza.

"Miaka ya nyuma tulikuwa na meli kutoka MSCL ambazo zilifanya kazi ikiwamo meli ya Mv Bukoba ambayo ilianza Bukoba hadi Mwanza, lakini meli ya Mv Victoria nayo ilikuwa ikija hapa na Mv Serengeti na kuanzia Machi mwakani, safari zitaanza tena kwa kasi," alisema.

Alisema kwa sasa, Bandari ya Bukoba imekuwa ikiendelea kutoa huduma kwa wateja wakubwa wawili ambao ni Kiwanda cha Sukari Kagera kinachotumia usafiri wa meli kupeleka sukari jijini Mwanza pamoja na Kampuni ya Omukwano ya Uganda ambayo husafirisha mafuta na sabuni kuingia nchini.



Baadhi ya askari wa kikosi cha mwitikio wa haraka (RRT) waliomaliza mafunzo ya wiki mbili katika Kijiji cha Rungwa, wilayani Manyoni wakimsikiliza mgeni rasmi wakati wa kufunga mafunzo hayo. **PICHA: JUMBE ISMAIL**

# Udahili mdogo wa Watanzania elimu ya juu wamshtua Samia

**Na Joseph Mwendapole**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amesema idadi ya Watanzania wanaopata elimu ya juu ni ndogo sana kulinganisha na nchi za jirani, hivyo ameiagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuweka mikakati ya kuongeza idadi ya wanaodahiliwa.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 12 ya Chuo Kikuu cha St. Joseph katika hotuba yake iliyosomwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe.

Makamu wa Rais alisema wizara hiyo inapaswa kukaa na kuweka mikakati kwa kushirikiana na vyuo binafsi ambavyo ni mdau mkubwa wa serikali katika kuongeza udahili na kuboresha elimu ya juu.

Alisema asilimia 25 ya wahitimu wanaomaliza vyuo vikuu nchini kila mwaka wanatoka vyuo vikuu binafsi, hivyo wizara ikishirikiana na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) inapaswa kuweka mikakati ya kuviwezesha kukua na kuongeza udahili.

"Kazi kubwa ya TCU inapaswa kuwa kuvilea na kuvijengea uwezo vyuo vikuu kama St. Joseph na isionekane kwamba iko kwa ajili ya kuvifungia tu kwa sababu hivi vyuo ni mbia muhimu sana wa serikali," alisema Prof. Mdoe.

"Najua mliwahi kufungiwa na TCU kwenye baadhi ya kozi kutokana na kasoro zilizokuwapo wakati huo, lakini nafurahi sana na kufarijika kuona mlifanya marekebisho makubwa na kuendelea na ubora wenu na ujio wangu hapa ni ushahidi kwamba serikali imeridhika na maboresho ambayo mmeyafanya," alisema.

Alisema ana taarifa kuwa tangu chuo hicho kianzishwe mwaka 2004, kimefanikiwa kutoa wahitimu 7,900 wa fani za uhandisi, ualimu wa sayansi na shahada katika fani mbalimbali.

Aidha, alisifu mchango wa Kanisa Katoliki katika utoaji wa elimu ya juu nchini kwani ilikuwa ya kwanza kuitikia wito wa serikali kwa wadau binafsi miaka ya 1980 kuunga mkono juhudi za serikali katika kuanzisha vyuo vikuu hapa nchini. Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Innocent Ngalinda, aliishukuru serikali kwa namna inavyokiunga mkono chuo hicho kwa kuwapatia mikopo wanafunzi wanaojiunga nacho na kisha kuwapa ajira wahitimu wake.

Alisema chuo kimejizatiti kuhakikisha kinatoa wahitimu ambao watamudu kujiajiri na kuajiri wenzao badala ya kusubiri ajira hivyo kutoa mchango wao kuifikisha Tanzania kwenye ndoto yake ya kuwa nchi ya uchumi wa kati na wa viwanda.

"Safari ya kitaaluma siyo nyepesi sana ila nawashukuru wahadhiri wamewaandaa wahitimu na wameiva tayari kwenda kuitumikia jamii hivyo mkafanye kazi kwa ubunifu, weledi, mjitume na msijihusishe na rushwa ili watu watakapowaona wajue kwamba kweli nyinyi ni wahitimu wa Chuo Kikuu cha St. Joseph," alisema.

Alisema nchi inapoelekea kwenye uchumi wa kati inahitaji wataalamu wengi wazalendo katika fani za uhandisi na yeknolojia, hivyo aliahidi kuwa chuo hicho kitaendelea kuzalisha wahitimu wa fani hizo watakaotimiza ndoto hizo.

# Tanzania yaziangukia nchi tajiri dola bil. 100 tabianchi

**Na Mwandishi Wetu, Madrid**

TANZANIA imeziomba nchi tajiri duniani kuongeza michango ya kupambana na athari za tabianchi walau kufikia Dola za Marekani bilioni 100 kila mwaka.

Akihutubia Mkutano wa 25 wa Umoja wa Mataifa juu ya Tabianchi unaomalizika leo jinini hapa, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Musa Sima, amesema Tanzania imeathiriwa sana na matukio ya janga la tabianchi, hasa kwa matukio ya mvua nyingi na joto lililopitiliza ambavyo havikupata kushuhudiwa kwa miongo kadhaa iliyopita.

Alisema mafuriko yameua, yamevunja barabara na madaraja na kusababisha hasara kubwa.

Sima alisema Tanzania inatambua mchango wa nchi tajiri katika kupambana na janga hilo la kidunia, lakini alikumbusha kwamba nchi tajiri zimeahidi kutoa kwa hiari fedha za ziada kwenye mfuko uitwao Green Climate Fund ahadi ikiwa ni dola za Marekani bilioni 9.66.

"Bado tuko mbali na kuziba pengo la mahitaji ya fedha ya nchi zinazoendelea na lengo lililowekwa la kukusanya dola za Marekani bilioni 100 kwa mwaka. Kwa hiyo tunaziomba nchi zilizoendelea na wachangiaji wengine kuzidisha michango yao."

Alisema katika kutoa mchango wake kidunia, Tanzania inatekeleza miradi kadhaa ya kimkakati ili kupambana na athari za tabia nchi na kutaja baadhi yake kuwa ni ujenzi wa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia maji. Aidha Tanzania imeimarisha Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa kwa kununua rada mbili ili kuiongezea uwezo taasisi hiyo ya kufuatilia na kutabiri mwenendo wa hali ya hewa.

Ili kupunguza utoaji wa kaboni dioksaidi (gesimkaa), Sima alieleza kwamba Tanzania imejenga mradi wa mabasi yaendayo haraka (BRT ) katika Jiji la Dar es Salaam na inajenga reli ya kisasa na iko makini na kampeni ya kitaifa ya kupanda miti ili kupambana na upoteaji na uharibifu wa misitu na kueleza kwamba Tanzania inaendesha kampeni hii ingawa ina takribani hekta milioni 48 za misitu.

Ameeleza kuwa Tanzania inazishukuru serikali za Chile na wenyeji wa mkutano, Ufalme wa Uispaniola, kwa kuandaa mkutano huo.

Kadhalika Tanzania imemshukuru Katibu Mkuu wa Umoja wa Mtaifa, Antonio Guterres, kwa kuandaa mkutano wa wakuu wa nchi uliofanyika jijini New York Septemba 23, 2019.

Naibu Waziri huyo amesema kwa ushahidi wa ripoti ya nwaka huu ya Taasisi ya IPCC na maonyo yake na maonyo ya mwaka huu ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Hali ya Hewa (WMO), dunia ina wajibu wa kuchukua hatua za haraka kulinda sayari hii na wakati wa kufanya hivyo ni sasa.

# Wafanyakazi bora Bugando wazawadiwa

**Na Anthony Gervas,**
MWANZA

HOSPITALI ya Kanda ya Ziwa Bugando, imewapa zawadi ya Sh. 9,000,000 watumishi 18, ambao ni watendaji kazi bora.

Zawadi hizo zilitolewa juzi na Mkurugenzi Mkuu wa hospitali hiyo, Prof. Abel Makubi, kwa watumishi hao wa kada mbalimbali, wakiwamo madaktari, wauguzi na watumishi wengine katika sherehe za maadhimisho ya Bugando Day jijini Mwanza.

''Hospitali ya Kanda ya Ziwa -Bugando imeamua kutoa zawadi kwa watumishi bora, wanaofanya kazi kwa bidii, kujituma, nidhamu, kuleta wateja, wanaotoa huduma vizuri kwa wagonjwa wetu, hivyo kila mmoja katika hao 18 tumempa Sh. 500,000 kama motisha," alisema Prof. Makubi.

Prof. Makubi alisema kuwa lengo la kufanya maadhimisho hayo kwa ni kudumisha umoja kati ya watumishi na Taasisi ya Chuo Kikuu cha Tiba ya Afya (CUHAS), kujitathmini huduma zake kwa wananchi na utendaji kazi wao katika utoaji wa huuma za wagonjwa.

Alisema kwa jambo lingine la maadhimisho hayo ni watumishi wa pande zote mbili hospitali na taasisi hiyo kukutana wao na kuwapa moyo wa kufanya kazi kwa bidii, kufanya mazoezi ya miili yao ili kuimarisha afya zao kupitia michezo mbalimbali.

Alisema watumishi wa hospitali hiyo watakaoendelea kufanya kazi vizuri kwa bidii, kujituma, kutoa huduma bora kwa wagonjwa, kuleta wateja, ikiwamo idara ya fedha inayodhibiti matumizi mabaya ya fedha za hospitali wataendelea kupewa zawadi kila mwaka katika sherehe za Bugando Day.

Sherehe hizo ziliambatana na michezo ya mpira wa miguu, mikono, mbio za mita 100, mita 200, mita 400, mbio za kutumia magunia wanawake na wanaume, kukimbiza kuku na kuvuta kamba.

# Waaswa kuacha kuwanyima haki wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANANCHI kisiwani Pemba wameaswa kuacha tabia ya kuwanyima haki zao za msingi watu wenye ulemavu badala yake wawe nao karibu kwa kuwapatia haki zao wanazostahili.

Imebainika kuwa miongoni mwa haki wanazonyimwa watu wenye ulemavu ni kukoseshwa haki ya ardhi ambayo ni rasilimali muhimu na kuikosa kwao kunawasababishia umaskini wa milele.

Akitoa mada katika mafunzo ya umiliki wa ardhi na mali nyingine kwa watu wenye ulemavu Wilaya ya Mkoani yaliofadhiliwa na Foundation for Civil Society, Ofisa kutoka Ofisi ya Kamisheni ya Ardhi Pemba, Faki Ali Makame, alisema kuna baadhi ya watu hutumia hali walizonazo makusudi ili kuwanyima haki zao.

Alisema ili kuhakikisha watu wenye ulemavu hawahangaiki, serikali imeweka usawa kwa mujibu wa sheria.

Alisema hakuna tafauti yoyote katika upatikanaji wa haki za msingi kwa watu wenye ulemavu na wale wasiokuwa na ulemavu, jambo ambalo linaonekana kubezwa kwa maslahi binafsi.

Alieleza kuwa serikali inatoa hati za umiliki wa ardhi kwa watu wote bila ubaguzi.

"Mikataba mbalimbali ya kimataifa, kikanda na hata Katiba ya Zanzibar na ya Muungano zinaeleza wazi umiliki wa ardhi bila kubagua," alisema.

Alizitaja njia za kupata haki ya matumizi ya ardhi, alisema ni kupitia serikalini, kurithi, kununua, utambuzi wa ardhi pamoja na zawadi, ambapo serikali inatoa hati ya umiliki bila ya ubaguzi.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya watu Wasioona Wilaya ya Mkoani Pemba, Ali Hemed Khalifa, alisema watu wenye ulemavu wananyanyapaliwa na kuonekana kama hawana haki, jambo ambalo linawaletea unyonge na umaskini.

Alisema, baadhi ya familia hugawana mali bila ya kumshirikisha mwenye ulemavu na kusahau kama na wao ni walemavu watarajiwa.

Alieleza muda wowote mtu anaweza kupata ulemavu, hivyo ni vyema kuacha tabia ya kuwanyanyapaa na kuwanyang'anya haki zao kwa kisingizio cha ulemavu.

Mshiriki wa mafunzo hayo, Malik Muhammed Omar, kutoka Shehia ya Ng'ombeni, alisema watu wenye ulemavu hasa kinamama wamekuwa wakipata changamoto na kunyimwa ardhi hasa anapofiwa na waume, hivyo kutokana na udhaifu wao, hupewa vitu vingine na sio ardhi.

Naye Fatma Salum Abdalla kutoka Mtambile, alisema wanawake wenye ulemavu hunyimwa haki zao wakati wa kurithi na badala yake baba wadogo ndio huhodhi mali na watoto huachwa nyuma.

# Mchanga kuwanufaisha wachimbaji wadogo almasi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WACHIMBAJI wadogo wa almasi wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, wanatarajia kunufaika na madini hayo, baada ya serikali kutangaza mchanga ambao unadhaniwa kuwa na almasi.

Mchanga huo ulikuwa ukikusanywa na mgodi wa Wiliamson Diamond baada ya kumaliza kuchakata almasi, utaanza kutolewa nje ya mgodi.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Madini, Dotto Biteko, wakati akizungumza na wachimbaji wadogo wa almasi kwenye mji wa Maganzo wilayani Kishapu, kuwa serikali imeshakubaliana na mgodi wa Wiliamson Diamond kuwa mchanga huo waanze kutoa nje ili wachimbaji watafute almasi. Alisema mchanga huo ambao unadhaniwa kuwa na masalia ya madini ya almasi, hautatumia tena kufanya marudio ya kutafuta almasi, hivyo ni vyema ukatolewa nje ya mgodi ili kutoa fursa kwa wachimbaji wadogo waanze kuuchenjua na kujitafutia madini ambayo yatawainua kiuchumi.

"Kilio chenu cha miaka mingi ambacho mlikuwa mkiomba masalia ya mchanga unadhaniwao kuwa na madini ya almasi kutoka ndani ya mgodi wa Wiliamson Diamond, sasa serikali ya awamu ya tano imekisikia, na ninatangaza hapa kuwa hadi kufikia Desemba 22, mwaka huu, mchanga huo utakuwa umeshatolewa nje ya mgodi," alisema Biteko.

"Ila naagiza kwenu hakikisheni almasi ambayo mtaipata kwenye mchanga huo mnaiuza kwenye Soko la Maganzo, asije akatokea hata mchimbaji mmoja kutorosha madini hayo, tutamchukulia hatua kali za kisheria, kwa kuwa tunataka madini haya yaanze kukuza uchumi wa eneo husika na taifa kwa ujumla," aliongeza. Naye Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, alipongeza uamuzi huo ambao umetolewa na serikali kupitia Wizara ya Madini, na kutoa wito kwa wachimbaji hao waitumie fursa hiyo vizuri kutafuta madini kwenye mchanga huo, huku akitoa tahadhari ulinzi mkali utakuwapo na hakuna mchimbaji ambaye atatorosha madini hayo nje ya mkoa huo.

Kwa upande wake msemaji wa mgodi wa Wiliamson Diamond, Richard Jumanne, akizungumza na Nipashe alisema malidhiano ya kuutoa mchanga huo nje ya mgodi yalishafanyika tangu Julai mwaka huu, ambapo kwa sasa kuna taratibu zinakamilishwa ili uanze kutolewa na kupelekwa sehemu maalumu ambayo imetengwa.



Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro (wa pili kushoto), akimkabidhi viti pamoja na meza 50 Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe (wa tatu kulia). Pia benki hiyo ilikabidhi misaada ya vifaa vya afya na elimu vyenye thamani ya Sh. milioni 40 mkoani Tanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Ummy ashukuru vitanda ICU Muhimbili

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ameitaja Benki ya NMB kama mdau na mhimili mkuu wa usaidizi kwa serikali katika utatuzi wa changamoto kwenye sekta ya afya, huku akiitaka kuendeleza moyo wa kuitumikia jamii.

Hayo aliyasema Ijumaa kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), jijini Dar es Salaam, wakati akipokea msaada wa vitanda vitano vya wodi ya watoto wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU), ambayo ina uhitaji mkubwa wa vitanda hivyo kwa sasa.

Waziri Ummy alisema kuwa, vitanda hivyo vya ICU ya watoto Muhimbili, pamoja na vingine 10 na magodoro yake kwa ajili ya wagonjwa wa kawaida katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, vinadhihirisha namna NMB ilivyojikita katika kusaidia utatuzi wa changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

Alibainisha kuwa serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya afya, ambako ndani ya miaka minne sasa imejenga vituo vya afya 352, hospitali za wilaya 68, hospitali za rufani 7 na hospitali mbili za rufani za kanda, lakini bado sekta hiyo inakabiliwa na changamoto zinazohitaji usaidizi kama wa NMB. Aliishukuru benki kwa kutoa msaada wa vitanda vitano vya ICU ya watoto vyenye thamani ya Sh. milioni 37.5, ambavyo vinaifanya sasa MNH kuwa na jumla ya vitanda 93 kwa ICU zote, na kwamba kabla ya utawala wa Awamu ya Tano, kulikuwa na vitanda hivyo 21 tu hospitalini hapo.

Akikabidhi msaada huo na ule wa vitanda 10 na magodoro yake kwa ajili ya wagonjwa Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila (vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 45), Ofisa Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani wa NMB, Juma Kimori, alisema benki yake itaendelea kuisapoti serikali katika kukabiliana na changamoto za kiafya.

Aliongeza kuwa msaada huo ambao unatokana na asilimia moja ya faida yao ya mwaka, wanayoitoa kwa ajili ya kusaidia utatuzi wa changamoto za afya na elimu, unatokana na msukumo wa kuikwamia jamii, ambayo ndio mtaji mkuu katika kuifanya NMB ipate mafanikio kibiashara.

Aidha, Kimori aliishukuru MNH kwa aina ya ushirikiano wa kuvutia sio tu wa kuomba na kupewa misaada ya vifaa tiba na miundombinu, bali ushirikiano wa kibiashara baina ya pande hizo mbili, hasa ukizingatia kuwa malipo yote ya kipesa kwa wagonjwa hospitalini hapo, yanapitia NMB. Mkurugenzi wa Huduma za Ukunga na Uuguzi wa MNH, Zuhura Mawona, kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Lawrence Museru, aliipongeza NMB kwa kuguswa na changamoto za ICU ya watoto na kwamba msaada wao unaenda kupunguza uhaba wa vitanda hivyo.

"Msaada huu wa NMB unaifanya ICU ya watoto hapa Muhimbili kwa sasa, kuwa na vitanda 12, kutoka vitanda saba tulivyokuwa navyo hapo kabla. Hii ina maana tumepunguza uhaba wa vitanda, ingawa bado tunahitaji vitanda saba tu kumaliza kabisa suala la vitanda toshelevu," alisema Mawona.

# Gambo azindua vikundi soko la mifugo

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amezindua vikundi vya wafanyabiashara wa mifugo na vya ushirika soko la kimataifa la mifugo lililopo eneo la Eworendeke, wilayani Longido.

Alipongeza uongozi wa Halmashauri ya Longido kwa wanavyoshirikiana na ofisi ya mkuu wa wilaya na mkoa.

"Nawapongeza sana kwa sababu mwaka jana mwishoni wakati Rais anafanya ziara mkoani Arusha, alitoa maelekezo ya kufungua soko la kimataifa la mifugo, akifahamu kuwa tukiwa na soko tutaweka taratibu zote za mifugo kisheria na sasa tumetekeleza sababu ya ushirikiano," alisema.

Alisema moja ya faida wanayopata katika soko hilo ni kuondokana na changamoto ya kufuatilia vibali vya kusafirisha mifugo jijini Dar es Salaam au Dodoma.

"Mifugo yetu tuliyokuwa tunapeleka nje ya nchi ilitupa shida kwa sababu upatikanaji wa vibali vya kisafirisha ilikuwa shida, lakini sasa tunapata hapa hapa huduma hiyo," alisema.

Gambo alisema kufunguliwa kwa soko hilo kumeongeza kipato na kwa sasa wanakusanya zaidi ya Sh. bilioni moja.

"Kabla ya soko hili halijaanzishwa halmashauri ilikuwa ikikusanya Sh. milioni milioni kwa mwezi na tangu waanzishe soko hili hapa mpakani Namanga, wanapata zaidi ya Sh. milioni 24 kwa mwezi kiwango hiki kimeongezeka mara nane zaidi ya walivyokua wanapata na serikali kuu ilikuwa haipati chochote, lakini sasa wanapata fedha," alisema.

Akizungumzia changamoto za mnada wa soko hilo, ikiwamo wafugaji wa Tanzania kutoruhusiwa kutumia magari ya Tanzania wakati wa kusafirisha mifugo kwenda nchini Kenya, alimtaka Mkuu wa Wilaya, Frank Mwaisumbe, kufanya vikao vya ujirani mwema kati ya Longido na Kajado nchini Kenya na kulipatia ufumbuzi.

Alisema kabla ya ufunguzi wa soko hilo, mkuu wa wilaya hiyo hakufurahishwa na takwimu za upatikanaji wa fedha za ununuzi wa mifugo kutokana na malipo kufanyika baina ya mnunuzi na mnunuaji na wakilipwa walikuwa wakiingiza kwenye akaunti za nchini kwao na siyo Tanzania.

"Sasa Tanzania ilikuwa hainufaiki na rasilimali zake, lakini kila kitu kinafanyika kisheria katika soko hili na tunaona faida ya rasilimali zetu, kikubwa tuelimishe wananchi wauze mifugo yao katika minada hii na viwanda vyetu," alisema.

Aliwaomba wamiliki wa taasisi za kifedha kujenga utamaduni wa kukutana na vikundi hivyo kuwaelimisha umuhimu wa kuhifadhi fedha na kufuga kisasa ili wapate mifugo yenye tija.

"Taasisi zilizohudhuria hapa CRDB, NMB na TBA, wasaidieni hawa wafanyabiashara wa mifugo wanufaike na taasisi hizi," alisema.



Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Chiku Issa na Meneja Mikopo wa Kitengo cha Biashara, Isabela Maganga wa (CRDB), wakitoka kwenye kiwanda (ELIYA) kinachojengwa Namanga, huku wakiteta jambo wakati wafanyabiashara wa mifugo, viongozi wa serikali walipokitembelea jana. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Serikali kupitia sheria fidia ya uharibifu mazao

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI ipo katika hatua ya kupitia upya sheria ya fidia ya uharibifu wa mazao unaofanywa na wanyamapori ili kupunguza malalamiko ya wananchi ya kutokupewa fidia stahiki inayoendana na uharibifu huo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, wakati akizungumza katika mkutano wa wadau wa uhifadhi na maliasili uliondaliwa na Jumuiko la Maliasili nchini Tanzania (TRN).

Alisema, sheria hiyo ya mwaka 1974 inafanyiwa mapitio na kufanyiwa marekebisho ili wananchi wapate haki pale uharibifu unapotokea.

Prof. Mkenda alisema marekebisho yatakayofanyika yatapunguza malalamiko yanayotolewa na wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi.

"Lakini pia wizara imekuwa ikigawa mizinga ya nyuki kama njia mojawapo ya kukabiliana na uharibifu wa wanyamapori hususan tembo," alisema.

Pia alisema mbali na jitihada hizo pia wizara inakamilisha mchakato wa kuanza kuuza nyamapori kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi ili kupunguza uwindaji wa kitoweo katika maeneo hayo.

Mbunge wa Babati Vijijini, Jitu Soni, alisema kurekebishwa kwa sheria ya fidia kutawafuta wananchi machozi hasa wanaoishi mbali kidogo na hifadhi, tofauti na wale walioko karibu na pia itasaidia kuhamasisha uhifadhi endelevu miongoni mwa wananchi.

Mkurugenzi wa Jumuiko la Maliasili nchini Tanzania, Zacharia Faustine, alisema mchakato wa kulipa fidia unachukua muda mrefu na kiasi wanacholipwa hakiendani na hasara wanayopata jambo linaloshusha hamasa kwa wananchi kushiriki uhifadhi.

"Naipongeza serikali imefanya vyema kupitia sheria hii ili wananchi wanaokumbwa na changamoto za wanyama hao wapate stahiki zinazolingana na gharama halisi," alisema.

Mmoja wa wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi ya Taifa ya Arusha, Asha Salim alisema marekebisho ya sheria ya fidia sio rafiki kwa wananchi hivyo inapaswa kuangaliwa upya kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla.

# Takukuru yaagizwa kuchunguza ubadhirifu zahanati

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Zephania Chaula, amemwagiza Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) wilayani humo, Adam Kilongozi, kuchunguza ubadhirifu wa Sh. milioni mbili unaodaiwa kufanyika kwenye zahanati ya kijiji cha Lengast.

Chaula alitoa agizo hilo juzi wakati alipofanya ziara ya siku moja ya kutembelea Kijiji cha Lengast na kuambiwa kero hiyo na wananchi.

Alisema suala la ubadhirifu wa fedha hizo amelisikia na anamwagiza Mkuu wa Takukuru wa wilaya hiyo alifuatilie kisha atoe majibu kwa wananchi hao na hatua nyingine za kisheria.

"Ufujaji wa fedha za wananchi siyo mzuri hivyo Takukuru chunguzeni hilo na endapo mtaona kuna ushahidi wa hilo, mhusika mfungulieni kesi mahakamani ili akajibu shtaka hilo," alisema Chaula.

Mkuu wa Takukuru wa Wilaya ya Simanjiro, Adam Kilongozi, alisema suala hilo analichukua na atalifanyia kazi ili kuchunguza madai hayo.

Kilongozi alisema wananchi wa eneo hilo ambao wanafahamu suala hilo wanapaswa kutoa ushirikiano ili uchunguzi ufanyike na hatua kuchukuliwa.


Awali, Mwenyekiti wa Kijiji cha Lengast, Tulipo Paul, alilalamika kwa mkuu huyo wa wilaya kuhusu, ubadhirifu wa Sh. milioni mbili unaofanyika kwenye zahanati hiyo.

Paulo alisema wananchi walichanga fedha hizo kwa ajili ya kununua samani za zahanati hiyo, lakini mmoja kati ya madaktari wa zahanati hiyo alifuja fedha hizo na hakuna hatua iliyochukuliwa.

"Huyo daktari pia ni mtoro kazini kwa kuwa anafika kwenye zahanati muda anaotaka na kuna mkunga ambaye anatoa lugha mbaya kwa wagonjwa ila tunashukuru amehamishwa," alisema.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Gabriel Quleka, alisema wanafuatilia suala hilo ili kuhakikisha huduma ya afya inaboreshwa kwenye zahanati hiyo ya Lengast.

"Huyo nesi alilalamikiwa ikiwamo kutoa lugha chafu na hata kondo la nyuma hakuwa anawaelekeza ipasavyo wanawake wanaozalishwa kwenye zahanati hiyo namna ya kuchoma hivyo wakawa wanatupa ovyo," alisema Quleka.





# Miundombinu yakwamisha huduma afya

**Na Mary Mosha,** MOSHI

UBOVU wa miundombinu ya barabara katika vijiji vinne vya Kata ya Kirua Vunjo Magharibi, Wilaya ya Moshi umesababisha wajawazito na watoto kushindwa kwenda hospitalini kupata huduma za afya.

Kutokana na hali hiyo, wananchi wa vijiji hivyo wameiomba serikali wilayani humo kutatua tatizo hilo, kwa kuwa wanalazimika kutumia gharama kubwa kukodi usafiri wa pikipiki baada ya mabasi madogo ya daladala kupandishwa nauli.

Kwa nyakati tofauti juzi, wakazi wa Kijiji cha Manu, Jenipher Nyambo na Clementina Dominiki, walieleza adha wanayoipata kutokana na ubovu wa barabara hiyo na kusababisha mabasi kususia kufanya shughuli za usafirishaji katika vijiji vya Manu hadi Kongo.

"Hali ni mbaya kwa wananchi wanaotumia barabara hii, wajawazito na watoto ndio waathirika wakuu wa tatizo hilo kwa sababu wanalazimika kutembea zaidi ya kilomita 20 kufuata huduma kata ya jirani. Tunamwomba Mkuu wa Wilaya awasukume Tarura (Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini watusaidie kumaliza tatizo," alisema Clementina.

Naye Adam Lyimo, mkazi wa Marangu, alisema katika kipindi hiki cha mvua wamekuwa wakipata adha kubwa, huku baadhi ya wajawazito wakishindwa kwenda hospitali kutokana na ubovu wa barabara hiyo.

Barabara hiyo ya Kongo hadi Manu ina urefu wa takribani kilomita sita, inaunganisha vijiji vya Mare, Kanango, Manu na Yamu.

"Ipo haja ya serikali kuwatengenezea barabara wakazi wa vijiji hivi ili kuondokana na adha wanayoipata. Unakuta kwa siku mtu anatumia hadi shilingi 15,000 kwa ajili ya kikodi usafiri wa bodaboda," alisema Lyimo.

Mwenyekiti wa serikali ya Kijiji cha Many, Joseph Chaki, akizungumzia malalamiko hayo, alisema wapo baadhi ya wananchi wanaoishi nje ya mkoa wa Kilimanjaro wamechangishana fedha kidogo kwa ajili ya kusaidia ukarabati wa barabara hiyo.

Alipotafutwa Meneja wa Tarura katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Roy Johansen, alisema wanapokea malalamiko ya wananchi kuhusu tatizo hilo na sasa wanajipanga kwenda kufanya matengenezo ya dharura.

Meneja huyo alisema ubovu wa barabara hiyo wameuingiza kwenye bajeti ya mwaka 2019/2020 ambapo itatengenezwa kilomita nne kwa kiwango cha changarawe.

# Mradi wa samaki kunufaisha 3,000 Same

**Na Godfrey Mushi,** SAME

UJENZI wa mradi wa mabwawa makubwa ya kufuga samaki katika Kijiji cha Kalimawe, Wilaya ya Same, unatarajia kunufaisha zaidi ya wananchi 3,000 wa vijiji sita vya ukanda wa milimani. Wanufaika wa mradi huo ni vijiji vyote vinavyolizunguka Bwawa la Kalimawe.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alithibitisha kuanza kwa awamu ya kwanza ya ujenzi huo chini ya kampuni ya kigeni kutoka nchini Norway.

"Tayari tumepokea wageni hao kutoka nchini Norway ambao ndio watakaojenga mabwawa hayo, kampuni hii itakuwa ni ya mfano kwa kufanya vijiji vifaidike moja kwa moja kwa kushirikiana kama mmiliki wa kampuni," alisema.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Norway na Kampuni ya Kalemawe Dam Investment Ltd inayomilikiwa na wazawa kwa ushirikiano kati yake na Halmashauri ya Wilaya ya Same, zimeingia mkataba wa makubaliano ya kuendesha miradi hiyo kwa ubia.

Alisema Bonde la Mto Pangani (PBWO) limetoa kibali cha matumizi ya maji kwa ajili ya mradi huo utakaovinufaisha vijiji vya Makokane, Mgandu, Msufini na Karamba, Kalimawe na Ndungu.

Aidha, Senyamule aliongeza kuwa vijiji hivyo vimeridhia kutoa nguvu kazi ya kuchangia maendeleo ya ujenzi huo.

Zaidi Senyamule alisisitiza: "UNCDF wamefadhili awamu hii ya kwanza ya ujenzi, ambapo utaalamu toka nchi ya Norway utatumika kwa kuwa ni nchi inayotegemea uchumi wa samaki kwa kiasi kikubwa."



Paulo Martin na Issa Shaban wakilinganisha vyuma ili kuvisuka kwa ajili ya kumimina zege kwenye moja ya jengo la uzalishaji la kiwanda cha kusindika nyama cha (ELIYA), kinachoendelea kujengwa wilayani Longido eneo la mpaka wa Namanga chenye uwezo wa kusindika mbuzi na kondoo 3,000 hadi 4,000 kwa siku na ng'ombe 500 kwa ajili ya soko la nje hasa Kenya. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Bakwata yatakiwa kubuni vyanzo vipya mapato

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata), limetaka viongozi wa baraza hilo kuanzia ngazi ya misikiti, kata, wilaya na mkoa kubuni vyanzo vya vipya vya mapato, badala ya kuendelea kutegemea sadaka peke yake kuendesha shughuli za maendeleo.

Ushauri huo ulitolewa jana na Kaimu Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Shaban Mlewa, wakati akizungumza na waumini wa dhehebu hilo katika msikiti wa Riadha mjini Moshi.

"Tuna kila sababu ya kubadilika ndugu zangu, wenzetu wote waliofanikiwa wamewekeza katika miradi ya elimu, afya, biashara na mambo mengine mengi. Ukiangalia misikiti mingi haina vitega uchumi kwa asilimia kubwa na inategemea sadaka pekee za waumini kuendesha misikiti na miradi," alisema na kuongeza:

"Tumesema sasa hapana, tunataka kila msikiti ubuni vyanzo vyake vipya vya mapato vitakavyowezesha kujiendesha. Uchumi ni jambo muhimu kwa Waislamu hivi sasa, ndio maana mara nyingi tunashindwa kufikia malengo."

Aliwataka viongozi wa misikiti kuangalia uwezekano wa kuanzisha miradi ya kiuchumi kama ufugaji wa kuku kisasa, kilimo cha umwagiliaji na maduka makubwa ya bidhaa.

Mlewa alisema mbali na msikiti kupata faida kutokana na vyanzo hivyo, pia itaongeza ajira kwa watu wa maeneo hayo hivyo kukuza uchumi wa taifa.

Wakati akisisitiza kuhusu maelekezo hayo Shekhe Mlewa alisema: "Nawaomba viongozi wa mkoa huu kuanzia wilaya zote kata zote msikiti yote kuanzisha miradi hiyo na kama kuna ya zamani muiboreshe nipo tayari kuwatafutia masoko ya uhakika ya bidhaa zenu."

Alieleza kufurahishwa kwake na baadhi ya viongozi wa Kiislamu kuona mbali na kuanza kubuni vyanzo vipya vya mapato.

Alisema kilichomfurahisha zaidi ni kuona msikiti mmoja wameanza kilimo cha umwagiliaji cha kutumia teknolojia ya mapone, huku akiahidi kuwaunga mkono kwa kuwatafutia soko la kuuza mazao yao watakapoyavuna.

Kwa upande wake, Katibu wa Bakwata wa wilayani Siha, Ramadhan Mollel na Katibu wa baraza hilo Wilaya ya Hai, Omari Mahamoud, walimpongeza Kaimu Shekhe huyo kwa ushauri alioutoa kwamba utaamsha kasi ya uwekezaji wa miradi ya kiuchumi itakayowaongezea kipato.

NIPASHE JUMATATU DESEMBA 16, 2019

Nipashe

# Spotika



MATATIZO MA5 YANAYOMTESA GUARDIOLA MANCHESTER CITY UK. 16&17




## ISIKUPITE

Mshambuliaji wa Manchester City, Sergio Aguero ni mmoja kati ya wachezaji wawili wenye hat-trick nyingi (11) zaidi Ligi Kuu England, akiungana na Alan Shearer (Blackburn Rovers / Newcastle United), tofauti ikiwa ni Muargentina huyo yeye amefunga akiwa na klabu moja wakati Shearer yeye alifikisha idadi hiyo akichezea klabu mbili tofauti.

# CHANA NYAVU...

Mohamed Salah akishangilia bao lake la kwanza kati ya mawili aliyoifungia Liverpool wakati ikishinda 2-0 dhidi ya Watford kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi. **PICHA: MTANDAO**

SOKA

# WATANO WAKUTINGISHA USAJILI JANUARI

**LONDON,** England

TUNAKARIBIA katikati ya msimu na kwenye dirisha dogo la usajili la Januari. Bila shaka kutakuwa na matukio mengi katika klabu kwenye soko la usajili kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyao kwa kujiandaa na nusu ya msimu uliobaki.

**Ingawa usajili wa kipindi hicho cha majira la baridi huwa hakina nguvu sana kama lile la majira ya joto, lakini timu zinakuwa na nafasi ya kurekebisha vikosi vyao.**

Usajili mkubwa umewahi kufanyika kwenye kipindi hicho kwa siku za hivi karibuni kama vile kusajiliwa kwa Virgil van Dijk aliyetua Liverpool na Philippe Coutinho kwenda Barcelona.

Hapa, makala haya inakuchambulia majina ya wachezaji watano ambayo yatabamba zaidi kwenye usajili kipindi cha Januari 2020...

### 5. DEJAN KULUSEVSKI

Dejan Kulusevski ni kinda mwenye umri wa miaka 19 raia wa Sweden na kwa sasa akicheza pale Parma kwa mkopo akitoka Atalanta. Kiwango chake msimu huu kimekuwa cha kuvutia mno na klabu nyingi barani Ulaya zimekuwa zikimtolea macho. Amefunga mabao matatu na pasi za mwisho tano kwenye mechi 15 za Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu huu.

Kocha wa Parma, Roberto D'Aversa akimzungumzia kinda huyo amesema, "Ni mchezaji mwenye akili na uvumi mwingi umemzunguka kuhusu wapi atakwenda. Tunatakiwa kuwa vizuri na kutompa majukumu mengi zaidi."

Kiwango chake kimezivutia klabu za Inter Milan, Manchester United, Juventus na Arsenal. Parma wanaweza kutaka kumbakisha mchezaji huyo kwa msimu wote, huku Atalanta wakitaka kuendelea kumuacha pale Parma ili ajiimarishe zaidi na beki yake ipande. Inter Milan na Man United wanaonekana kuanza kuonyesha ishara ya kutaka kumshawishi katika wiki za hivi karibuni.



SANCHO

### 4. ERLING BRAUT HAALAND

Erling Braut Haaland pengine ndiye mshambuliaji wa kati yupo 'hoti' sana sokoni kwa sasa. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, alitoka klabu ya Molde FK na kutua pale RB Salzburg Januari mwaka 2019 na tangu hapo hajaangalia nyuma. Hadi sasa amefunga jumla ya mabao 28 na pasi za mwisho saba katika mechi 22 alizocheza msimu huu ukiacha mabao nane na pasi ya mwisho moja kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kiwango chake kimezivutia klabu nyingi Ulaya zikiwamo, Manchester United, Borussia Dortmund, Real Madrid na RB Leipzig wenyewe wameonyesha nia ya kutaka kumbakisha.

### 3. JADON SANCHO

Jadon Sancho ametengeneza jina lake kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, msimu uliopita akicheza pale Dortmund. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, amefunga mabao 13 na pasi za mwisho 19 kwenye mechi 43. Ingawa Dortmund mara kadhaa wameweka wazi hawataki kumuachia, lakini klabu kadhaa zimekuwa zikimuwania.

Liverpool, Manchester United na Chelsea zinatajwa zipo kwenye mbio moja za kuwania saini yake.

### 2. CHRISTIAN ERIKSEN

Christian Eriksen ni mchezaji wa Tottenham Hotspur kwa sasa na msimu ujao atakuwa huru na imeripotiwa kwamba yeye mwenyewe anataka kuondoka hapo kwa miamba hao wa Kaskazini mwa London. Anakaribia kubakiza miezi sita kwenye mkataba wake na bado hajawa tayari kusaini mkataba mpya na klabu hiyo. Tottenham pengine italazimika kumuweka sokoni ili kuepuka kumuachia aondoke bure.

Klabu za Man United na Real Madrid zinatajwa kuwania saini yake. Eriksen alijiunga na Spurs kutoka Ajax mwaka 2013 na amekuwa kiungo muhimu kwa kikosi hicho cha Tottenham katika miaka ya hivi karibuni.

### 1. ZLATAN IBRAHIMOVIC

Kwa sasa anacheza kwenye Ligi Kuu ya Marekani (MLS) na Zlatan Ibrahimovic mkataba wake unamalizika Januari na klabu kadhaa za Ulaya zimekuwa zikihusishwa kuwania saini yake.

Alijiunga na LA Galaxy akitokea Manchester United Machi 2018 na anaonekana kurudi tena Ulaya.

Nyota huyo wa kimataifa wa Sweden bado anaonekana kuwa imara ingawa umri wake unakwenda na atakuwa tayari kucheza msimu wake wa 11 katika maisha yake ya soka. Amekuwa akihusishwa na Napoli na AC Milan huku pia ripoti nyingine zikimtaja kuwa anakwenda Hispania. Hivi karibuni aliposti video kwenye mtandao wake wa Instagram akisema, "Hola Espana, unajua nini? Nakuja tena."

Hivi karibuni amekuwa pia akihusishwa na Everton huku 'Toffees' hao wakiwa tayari kumfanya mchezaji atakayelipwa fedha nyingi zaidi klabuni hapo. Ukizingatia kwamba wakala wake ni Mino Raiola, uvumi zaidi unaweza kusambaa kwa siku zijazo.

**JE, WAJUA?**



TANGU ilipopanda Ligi Kuu England mwaka 2015, hakuna timu iliyoshinda mechi nyingi za ugenini dhidi ya Chelsea kama Bournemouth (tatu, sawa na Liverpool).

## MICHEZO



Wachezaji wa Simba kutoka kushoto, Mzamiru Yassin, Francis Kahata na Meddie Kagere.

# SIMBA KUFUTA GUNDU LA DESEMBA, KRISMASI?

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Simba inaweza kupitia tena kwenye kipindi kigumu kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA kipindi hiki cha Desemba kuelekea Sikukuu ya Krismasi, kutokana na rekodi yao mbovu inapofika kipindi hiki.

**Sikukuu ya Krismasi Desemba 25, Simba itacheza mechi dhidi ya Lipuli kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Bodi ya Ligi na siku tatu baadaye Desemba 28 itashuka tena kwenye uwanja huo huo kupambana na KMC ya Kinondoni.**

Kabla ya mechi hizo za ligi, kati ya Desemba 20, 21 au 22, Simba itatakiwa kucheza Kombe la FA dhidi ya Arusha FC.

Hiki kitakuwa kipindi kigumu kwa Simba kwani rekodi na takwimu zinaonyesha kushindwa kufanya vizuri kwenye kipindi hicho.

Kwa bahati mbaya sana msimu huu Simba inakutana na mechi tatu za Ligi Kuu na moja ya Kombe la FA kipindi hiki, tofauti na misimu miwili nyuma ilipokuwa ikikutana na mechi za FA tu, huku mechi za ligi zikiwa zimesimama kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kupisha mechi za kimataifa.

Ni kipindi ambacho Simba inapaswa kuwa makini kutokana na rekodi mbaya ambayo sababu yake haijajulikana.

Huenda kipindi hiki, Simba huwaachia wachezaji wao kwenda majumbani kula sikukuu badala ya kukaa kambini, na kwenda kucheza mechi wakiwa wanatokea nyumbani, hali hiyo, inayosababisha kupata matokeo mabovu, hivyo kama ikiendelea tena hivyo, basi mechi hizi zinaweza tena ngumu kwao kama ilivyokuwa zilizopita.

**SIMBA 3-4 GREEN WARRIOS (2017)**

Siku tatu kabla ya Sikukuu ya Krismasi ya mwaka 2017, Simba ilitolewa mapema kwenye michuano ya Kombe la FA na timu ya Daraja la Pili, Green Warrios kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Ilikuwa ni Desemba 22 wakati ilipolazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya timu hiyo yenye maskani yake Mwenge jijini Dar es Salaam na kuondolewa kwa mikwaju ya penalti 4-3.

Straika Hussein Bunu alianza kuiandikia Green Warrios bao la kwanza dakika ya 43, kabla ya John Bocco hajasawazisha dakika ya 53 kwa mkwaju wa penalti, baada ya mlinzi mmoja kuunawa ndani ya eneo hatari na mechi ikamalizika dakika 90 kwa bao 1-1, hivyo kulazimika kupigiana mikwaju ya penalti.

Penalti za washindi zilifungwa na Amir Haji, Juma Mdindi, Zuwaku Mugala na Bunu, huku za Simba zikiwekwa nyavuni na Erasto Nyoni, Shiza Kichuya na John Bocco, Mohamed Hussein 'Tshabalala', Mzamiru Yassin na Jonas Mkude wakikosa na kuwafanya wanachama na mashabiki wa Simba Krismasi yao kuwa chungu.

Ikumbukwe kuwa ni mechi ambayo iliondoka na 'kichwa' cha aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Joseph Omog ambaye siku moja baadaye alitimuliwa.

**SIMBA 2-3 MASHUJAA FC (2018)**

Siku moja tu baada ya Sikukuu ya Krismasi, Desemba 26, mwaka 2018 kwenye Uwanja wa Taifa, Simba ilikutana tena na kipigo cha mabao 3-2 kutoka kwa Mashujaa FC kutoka mkoani Kigoma.

Kwa mara nyingine tena ilikuwa ni Kombe la FA, kutafuta timu itakayoshiriki michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Haikuwa sikukuu nzuri kwa wanachama na mashabiki wa Simba, kwani siku moja tu baada ya kusherehekea, kesho yake walitarajia kuendelea kujirusha na 'boxing day', wakitegemea ushindi rahisi kutoka kwa wageni hao, lakini hali ikawa tofauti.

Alikuwa ni Paul Bukaba aliyeitanguliza Simba dakika ya 18 na bao hilo lilidumu hadi mapumziko.

Dakika ya 47 tu kipindi cha pili, Shaaban Hamisi aliisawazishia Mashujaa, kabla ya Jeremiaha Josephat kupachika bao la pili dakika ya 56.

Bukaba tena, aliisawazishia Simba dakika ya 78 na wakati kila mmoja akidhani kuwa mechi hiyo ingekwenda kwenye mikwaju ya penalti, Rajab Athumani aliwaliza mashabiki wa 'Wekundu wa Msimbazi' uwanjani alipofunga bao la tatu kwa shuti la mbali, kwenye dakika za nyongeza, sekunde chache tu kabla ya mechi hiyo kumalizika. Na Simba ikatolewa tena kwa mara ya pili mfululizo kwenye michuano ya FA, lakini ikiendeleza rekodi yake mbaya mwezi wa Desemba na Sikukuu ya Krismasi.

**NJE YA UWANJA**

Liverpool haijapoteza mechi katika michezo 34 ya Ligi Kuu iliyocheza (kushinda 29, sare tano), hivyo kuwa timu ya tatu kwa kucheza kipindi kirefu zaidi bila kupoteza kwenye historia ya ligi hiyo baada ya Arsenal (mechi 49) kati ya Mei 2003- Oktoba 2004 na Chelsea (mechi 40) kati ya Oktoba 2004- Oktoba 2005.



## Extra Time

# MATATIZO MA5 YANAYOMTESA GUARDIOLA MAN CITY



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United iliushtua ulimwengu wa soka wakati walipowafumua wapinzani wao wa jiji moja, Manchester City katika Uwanja wa Etihad Jumamosi ya Desemba 7, mwaka huu kwenye mchezo wa Ligi Kuu.

**Mabao kutoka kwa Marcus Rashford na Anthony Martial katika kipindi cha kwanza yalionyesha kiwango kizuri cha kocha wa kikosi hicho cha United, Ole Gunnar Solskajer ambacho sasa kimezifunga timu ya Jose Mourinho, Tottenham Hotspur na City ya Pep Guardiola ndani ya siku tatu.**

'Mashetani Wekundu' hao sasa wamejinyanyua wenyewe hadi nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu kabla ya mechi za mwishoni mwa wiki hii na kama kiwango chao sasa kitaendelea, bado wanaweza kutoa changamoto kubwa zaidi ndani ya nne bora msimu huu.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu tayari wamepoteza mechi nne msimu huu, zikiwa nyingi zaidi kuliko msimu uliopita.

Man City mechi zao nne zijazo kabla ya mwishoni mwa mwaka huu ni dhidi ya Arsenal (uliyopigwa Emirates jana Jumapili), nyumbani dhidi ya Leicester na ugenini dhidi ya Wolves na dhidi ya Sheffield nyumbani.

Mabingwa hao sasa wanaanza kusahau kuhusu kushinda taji la Ligi Kuu na wanajaribu kufanya mipango namna ya kurudi tena kwenye reli msimu huu.

Makala haya yanakuchambulia matatizo matano ambayo yanamsumbua Guardiola pale Man City kwa sasa...

### 5. KUKOSA HAMASA

Manchester City imevunja rekodi zote kwenye Ligi Kuu ya England katika misimu yake miwili iliyopita, ikishinda mataji hayo mara mbili kwa jumla ya pointi 198.

Pia wameshinda taji la Carabao mara mbili pamoja na lile la FA na kuifanya kuwa moja ya klabu iliyoweka historia ya aina yake kwenye soka la Uingereza.

Msimu huu ulitakiwa kuwa sawa na uliopita, lakini kipigo cha Jumamosi Desemba 7 kutoka kwa Man United kwa kiasi fulani kinakiweka kikosi cha Guardiola kwenye matatizo wakiwa katikati ya msimu.

Mabingwa hao tayari wamepoteza pointi 20 msimu huu, nyingi zaidi kuliko walizopoteza msimu wote uliopita. Kufungwa pale kwenye dimba la Anfield halikuwa jambo la kushangaza, kupoteza dhidi ya Norwich na Wolves na sare ya hivi karibuni dhidi ya Newcastle imefanya watu macho yaanze kuwatoka.

City wanaonyesha kukosa nguvu yake kama ilivyokuwa msimu uliopita. Ndio waliwafumua Watford 8-0 na pia wakatoka nyuma na kushinda 2-1 dhidi ya Southampton.

Hata hivyo, ni wazi kabisa kunakukosekana kwa hamasa kati ya wachezaji, kitu ambacho kilionekana hata kwenye mchezo dhidi ya United.

### 4. PEA YA KINA SILVA

Nahodha wa Manchester City, David Silva pengine ndiye mchezaji bora katika historia ya klabu hiyo. Wengi wanaweza kuwatazama Sergio Aguero na Vincent Kompany, lakini raia huyo wa Hispania amekuwa na kiwango cha aina yake tangu alipotua hapo City mwaka 2010.

Kwa sasa yupo kwenye msimu wake wa kumi na wa mwisho klabuni hapo, na Silva mwenye umri wa miaka 33, amekuwa nahodha wa City wakati ambao klabu hiyo ikivunja rekodi zote msimu uliopita. Kwa sasa amekuwa akifanya maamuzi kwa kasi ndogo akiwa dimbani.

Takwimu zinazungumza, Silva amepoteza mipira mingi zaidi mwenyewe ikilinganishwa na msimu uliopita. Uhakika wa pasi zake pia umekuwa wa kiwango cha chini ikilinganishwa na misimu iliyopita.

Bila shaka Silva bado ni kiungo bora kwenye Ligi Kuu ya England, Guardiola anahitaji kutomwanzisha katika kila mchezo. Silva alicheza kwa dakika zote 90 kwenye mechi dhidi ya Newcastle, Burnley na United. Kama ilitakiwa kupumzishwa, kwa Silva ilitakiwa kufanywa hivyo msimu huu.

Anayeonekana kuwa mrithi wa Silva ni Mreno Bernardo Silva. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alisajiliwa hapo City kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 43 mwaka 2017.

Hata hivyo, msimu uliopita ulikuwa ni kama ndio alijijengea heshima yake. Bernardo si tu kwamba alicheza mechi zote muhimu za City msimu uliopita, lakini pia alishinda taji la Ligi ya Mataifa ya UEFA akiwa na Ureno na kuwa mchezaji bora wa mashindano hayo.

Hata hivyo, amekuwa akichezeshwa kama winga wa kulia msimu huu. Kama ilivyo kwa Silva, naye kiwango chake msimu huu kinaonekana kutokuwa cha kuvutia. Uamuzi wa Guardiola kumchezesha Bernardo winga ya kulia ndio pia unachangia Riyad Mahrez kushindwa kupata nafasi nyingi za kucheza. Guardiola anahitajika kumchezesha Bernardo kiungo cha kati nafasi ambayo ndio inayomfaa kucheza na kuacha kumuanzisha Silva.

### 3. BEKI WA KUSHOTO

Nafasi ya beki ya kushoto kwa Manchester City imeendelea kuibua mjadala usioisha tangu Pep Guardiola alipotua hapo mwaka 2016. Wakati akitoka kule Bayern Munich, kocha huyo aliwakuta Gael Clichy na Aleksander Kolarov, na wote walikuwa watumishi wazuri kwa klabu hiyo wakati wakiwa kwenye umri wao miaka ya 30.

Hawakuweza kuendana na falsafa za kocha huyo ambaye alipendelea kumchezesha Fernandinho kama beki wa kushoto. Mwishoni mwa msimu City wakagundua kwamba walikuwa wanahitaji damu changa.

Benjamin Mendy alitua Etihad akitokea Monaco, lakini sasa ni majeruhi wa muda mrefu na kiungo wa kati, Fabian Delph alipelekwa kucheza huko msimu wa 2017/18. Na baada ya makosa akamhamisha Oleksandr Zinchenko ambaye kiasili ni kiungo mshambuliaji.

### 2. KUTOMCHEZESHA PHIL FODEN

Miezi michache iliyopita, Pep Guardiola alisema kwamba, Phil Foden kwenye umri wa miaka 18 "ni mchezaji mwenye kipaji bora" kuwahia kumuona na akaenda mbali hadi kumfananisha na Lionel Messi. Lakini Foden amecheza dakika 83 tu katika mechi saba alizochezeshwa hadi sasa.

Ingawa kinda huyo ameanza kwenye mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Carabao.

Katika umri wa miaka 18, Foden tayari ameshinda Kombe la Dunia la Fifa chini ya umri wa miaka 17, mataji mawili ya Ligi Kuu, mawili ya Carabao, Ngao ya Jamii mara mbili na FA, lakini Guardiola hana muda naye.

### 1. BEKI YA KATI

Manchester City imefunga mabao 44 katika mechi 16 msimu huu, moja pungufu ya msimu uliopita, huku wakiruhusu mabao 10 kwenye lango lao na hivyo inaonyesha wana tatizo kubwa kwenye safu ya beki wa kati.

Pengine kuumia kwa Aymeric Laporte kumesababisha matatizo makubwa kwa City, ingawa wana John Stones na Nicolas Otamendi, ambao walikuwa nguzo kuu kwa City msimu wa City wa 2017/2018.

Fernandinho sasa ndiye anayecheza nafasi ya beki wa kati kutoka kwenye nafasi yake ya kiungo ili kuziba pengo la Laporte.

Ni wazi kwamba, Man City wanahitaji beki wa kati haraka iwezekanavyo ili kutatua matatizo yao.

## Nukuu

"Kama Freddie [Ljungberg] atashindwa kuweka mambo sawa ndani ya mechi tano au sita zijazo, unahitaji kupata kocha mwenye uzoefu kunusuru mambo, lakini naamini watakuwa vizuri tu chini ya Freddie," **Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger**



"Nina heshima ya kumjua Mourinho, yeye ni mtu asiyetabirika kwamba yupo tofauti kabisa na mtazamo wa dunia ulivyo. Ilikuwa ni kitu cha kufurahisha kumjua yeye. Kucheza dhidi yake si kazi rahisi, lakini kumuona nikicheza naye ni jambo kubwa," **Kocha wa zamani wa Chelsea anayeinoa Juventus kwa sasa, Maurizio Sarri, akielezea kiu yake ya kutaka kukutana na Tottenham ya Mourinho kwenye hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.**



"Hakuna harakati zinazotarajiwa Januari, tuna kikosi chenye uwiano, hatuna upungufu wowote, lakini pia hatuwezi kumudu kumpoteza yeyote. Mara kadhaa kabla ya mchezaji kuonyesha utashi wa kuondoka, lakini kamwe si Januari. Katika hali nyingine tumekuwa tukiwaacha waondoke, katika mazingira mengine tumekuwa tukiwashawishi kubaki," **Rais wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, akizungumzia dhamira ya klabu hiyo ya kutomruhusu Arturo Vidal kuondoka katika dirisha la Januari.**





# KILI STARS INAVYOTESEKA NA MZIMU NUSU FAINALI

Beki wa kushoto wa Kili Stars, Mohamed Hussein 'Tshabalala' na kiungo Jonas Mkude (kulia) wakiwadhibiti washambuliaji wa Kenya kwenye michuano ya Chalenji inayoendelea nchini Uganda, ambapo Wakenya hao walishinda 1-0. **NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

KESHO, Jumanne timu ya soka ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Stars inatarajiwa kucheza mechi ya nusu fainali nchini Uganda kwenye michuano ya Kombe la Chalenji ikiwa ni baada ya miaka sita.

**Mara ya mwisho Kili Stars kucheza nusu fainali ilikuwa Desemba 10, 2013, michuano hiyo inayoandaliwa na Baraza la Vyama vya Soka Af rika Mashariki na Kati (Cecafa) ikichezwa nchini Kenya na kuchapwa bao 1-0 dhidi ya wenyeji hao ambao ndiyo waliokuwa mabingwa mwaka huo kwa kuichapa Sudan ma bao 2-0 kwenye mechi ya fainali.**

Kili Stars inataka kufuta rekodi mbaya ya kushindwa kutinga fainali kwa miaka tisa sasa.

Mara ya mwisho kufanya hivyo ilikuwa 2010, michuano hiyo ya Chellenge ikichezwa nchini na ilifanikiwa kulitwaa kombe hilo kwa kukichapa kikosi cha pili cha timu ya Taifa ya Ivory Coast bao 1-0 lililofungwa na Shadrack Nsajigwa.

Kikosi hicho cha Ivory Coast kilikuja nchini kama wageni waalikwa na kikaleta changamoto kubwa, kikiwa na wachezaji kama Kipre Tchetche na Paschal Wawa ambaye baadaye walisajiliwa na Azam FC, huku Wawa kwa sasa akiichezea Simba.

Kili Stars imekamata nafasi ya pili kwenye Kundi B, nyuma ya Kenya yenye pointi tisa, yenyewe ikiwa na pointi nne, ikicheza mechi tatu; kushinda moja, sare moja na kufungwa pia mechi moja.

Ilianza kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Kenya, ikalipiza kisasi kwa zanzibar kwa kuifunga bao 1-0, kabla ya kutoka suluhu ya bila kufungana dhidi ya Sudan.

Bado mashabiki wa soka nchini wana wasiwasi na kikosi hicho kuelekea mechi hiyo kwani kinaonekana kuwa na uwezo mdogo wa kufunga mabao, kwani kimepachika bao moja tu kwenye mechi tatu kilizocheza.

**REKODI MBAYA NUSU FAINALI**

Wakati wa kuelekea mechi ya kesho, rekodi zinaonyesha kuwa Kili Stars imekuwa na rekodi mbaya kwenye hatua za nusu fainali tangu mwaka 2011.

Miaka ambayo kimekuwa kikifanikiwa kupenya hatua za awali na hata robo fainali, kimekuwa kikikwama kwenye hatua ya nusu fainali, hivyo mechi ya kesho ni muhimu kwa kikosi hicho kuzima mzimu unaoitafuna na kukwamia hapo.

Zifuatazo ni mechi ambazo Kili ilikwamia hatua ya nusu fainali, na hii ni baada ya kutwaa kombe hilo mwaka 2010.

**KILI STARS 0-1 KENYA (2011)**

Ni michuano iliyofanyika nchini Tanzania, jijini Dar es Salaam na wenyeji Kilimanjaro Stars wakatolewa hatua ya nusu fainali kwa kuchapwa mabao 3-1 dhidi ya Uganda, ambao ndiyo waliokwenda kuchukua kombe hilo kwa kuichapa Rwanda kwa mikwaju ya penalti 3-2 baada ya kutoka sare ya mabao 2-2 ndani ya dakika 120.

**KILI STARS 0-3 UGANDA CRANES (2012)**

Kwenye michuano ya 2012 iliyochezwa nchini Uganda, Kilimanjaro Stars kwa mara nyingine ilikomea hatua ya nusu fainali kwa kuchapwa mabao 3-0 dhidi ya mwenyeji Uganda (Cranes) kwa mabao ya Emmanuel Okwi na Robert Ssentongo aliyefunga mawili.

Wenyeji Uganda alifanikiwa kulibakisha kombe hilo kwa kushinda mabao 2-1 dhidi ya Kenya kwenye mechi ya fainali.

**KILI STARS 0-1 KENYA (2013)**


Ikichezwa nchini Kenya mwaka 2013, Kilimanjaro Stars ilifanikiwa kuvuka vizingiti, lakini kama kawaida, ilipofika hatua ya nusu fainali, ilikumbana na Kenya, Harambee Stars na kuchapwa bao 1-0, ikawa ndiyo mwisho wake na kama ilivyo kawaida, rekodi zinaonyesha pia timu zinazoifunga Tanzania Bara kwenye hatua ya nusu fainali ndizo zinazokwenda kuchukua ubingwa.

Kenya iliichapa Sudan mabao 2-0 na kuchukua 'ndoo'. Mwaka 2014 michuano hiyo haikuchezwa, huku mwaka 2015, Kili Stars iliishia hatua ya robo fainali, michuano ikichezwa nchini Ethiopia, ikatolewa na wenyeji kwa penalti 4-3, michuano ambayo Uganda ilitwaa kombe kwa kuichapa Rwanda bao 1-0.

Mwaka 2016, michuano hiyo haikufanyika, huku 2017 ikichezwa nchini Kenya, lakini Kilimanjaro Stars ikakamata nafasi ya mwisho kwenye Kundi lake la A, hivyo kushindwa kwenda hata robo fainali.

Mwaka jana michuano hiyo haikufanyika, na mwaka huu Kili Stars imefanikiwa kutinga nusu fainali, hivyo mashabiki wanataka kuona kama mwiko wa kukomea hatua ya nusu fainali utavunjwa.

**NAJUA WAJUA**




TANGU kuanza kwa msimu uliopita, mshambuliaji wa Norwich, Teemu Pukki amefunga mabao mengi zaidi kwenye ligi (ikiwa ni pamoja na mechi za mchujo) kuliko mchezaji yeyote kwenye timu za nne bora Ligi Kuu England (mabao 38).

## SOKA



# SABABU 3 KWA NINI UNITED ITAMALIZA 4-BORA

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United ilionyesha kubadilika na kucheza kwa kiwango cha kuvutia zaidi wakati ilipowafunga wapinzani wao wa jiji moja, Manchester City kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England mabao 2-1.

**Ushindi huo ukawafanya wajivute hadi nafasi ya tano kwenye msimamo kwa mabao ya Marcus Rashford kwa penalti na lile la Anthony Martial.**

Ushindi huo wa vijana hao wa kocha, Ole Gunnar Solskjaer unaonekana kuwaweka kwenye wakati mzuri Man United.

Na pia matarajio ya wengi kwamba, Solskjaer anaweza kutimuliwa klabuni hapo sasa yanaonekana kuwa kama yamefifia, kwani sasa Man United inaonekana kurudi kwenye kiwango chake.

Hapa tunazichambua sababu tatu kwa nini United wanaweza kumaliza kwenye nne bora katika Ligi Kuu England msimu huu na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

**1. KIWANGO CHA MARCUS RASHFORD**

Ni miaka mitatu na nusu tangu Marcus Rashford mwenyewe alipoitangazia dunia kwa kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye mchezo wa ushindi dhidi ya Arsenal wakati akiwa bado kinda mdogo. Muingereza huyo alichezeshwa kwenye mchezo huo na kocha, Louis Van Gaal na aliiburuza safu ya ulinzi ya Arsenal kwa mabao mawili na kusaidia kutengeneza moja kwenye ushindi wa 3-2 Februari mwaka 2016.

Rashford, ambaye alichipukia kwenye akademi ya United, alikwenda kujiimarisha yeye mwenyewe kikosi cha kwanza kwa klabu yake hiyo ya utotoni. Msimu huu mambo mengi yamebadilika kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ambaye amefikia rekodi yake ya kufunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu na hii ndio kwanza Desemba.

Alifunga penlati vizuri katika kipindi cha kwanza na ndiyo iliyotoa taswira ya ushindi kwa United pale Etihad na kumfanya afikishe mabao 10, lakini ulikuwa uwezo na akili yake kuweza kupelekesha safu ya ulinzi ya Manchester City.

Hakuna shaka kwamba, ubora wa Rashford umeimarika zaidi kwa kile alichokifanya kwenye mchezo huo. Amefunga jumla ya mabao 13 katika mechi 14 zilizopita kwa klabu na nchini yake hadi sasa.

'Mashetani Wekundu' hao kwa sasa wapo nafasi ya tano kwa kiwango bora cha Rashford, na kama ataendelea hivyo wana nafasi kubwa ya kumaliza kwenye nne bora ya msimamo wa Ligi Kuu.

**2. SULUHISHO KWENYE KIUNGO**

Inaweza kuwa imechukua muda fulani, pengine ni muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa, lakini Ole Gunnar Solskjaer amepata nafasi ya kuifanyia kazi safu ya kiungo ya United bila ya kumtegemea anayetaka kuondoka, Paul Pogba.

Fred na Scott McTominay wametengeneza upatina mzuri zaidi sehemu ya kiungo ya United na hilo limefanya wachezaji kama Nemanja Matic na Andreas Perreira kukosa nafasi kwenye kikosi cha kwanza. Safu ya kiungo wa kati kwa raia huyo wa Brazil na mchezaji wa Scotland kumeondoa woga wa mashabiki wa United ambao walikuwa wanahofia kuondoka kwa Pogba.

Fred, alicheza kwa mara ya kwanza kwenye 'dabi' ya Manchester, na alionyesha kiwango cha kuridhisha zaidi na kuwazidi wale wa City. Hiyo ilikuwa ni mechi ya tisa mfululizo kwa raia huyo wa Brazil kwenye Ligi na imemfanya aonyeshe maajabu.

Kama United wanaweza kuendelea kumchezesha McTominay na Fred kunaweza kumfanya Pogba aondoke.

**3. 11-BORA YA SOLSKJAER**

Kocha wa Manchester United amekua akibadilisha timu yake mara kwa mara msimu huu na halikuwa jambo la kushangaza kujikuta wakiwa kwenye wakati mgumu wa kupata ushindi. Uwezo wao dimbani ulitegemea na kiwango binafsi cha mchezaji mwenyewe wakati wa kuanza kwa msimu huu.

Lakini kwenye mchezo ule wa Jumamosi pale kwenye dimba la Etihad, Solskjaer alionekana kukijua vizuri kikosi chake cha kwanza. Kuwapo kwa Jesse Lingard na kurudi kwa Martial kuliimarisha zaidi Man United.

Kwa uhakika kama wataendelea na kiwango hicho, kuna uwezekano mkubwa, Man United wakamaliza kwenye nne bora msimu huu.

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa England, Jadon Sancho ni miongoni mwa wafungaji wakati Borussia Dortmund ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Mainz juzi, hivyo kumfanya kucheka na nyavu kwenye mechi sita mfululizo, lakini amekuwa mchezaji wa kwanza katika ligi tano bora Ulaya kufunga na kutoa pasi za mwisho 'assists' 10 kwenye mashindano yote msimu huu.



NDANI YA 18



MANCHESTER United iliushtua ulimwengu wa soka wakati walipowafumua wapinzani wao wa jiji moja, Manchester City katika Uwanja wa Etihad Jumamosi ya Desemba 7, mwaka huu kwenye mchezo wa Ligi Kuu.

Uk. 16&17

# WATATU WAKUSEPA CHELSEA JANUARI



OLIVIER GIROUD

**LONDON,** England

SASA inaonyesha wazi jinamizi la usajili kwa klabu ya Chelsea limemalizika rasmi. Wakati wa kipindi cha majira ya joto kilichopita alipochukua nafasi ya ukocha kutoka kwa Maurizio Sarri, Frank Lampard alikuwa anatakiwa kuipa mafanikio Chelsea huku hakiwa hana 'vifaa'.

Chelsea ilimpoteza mchezaji wake bora, Eden Hazard na walikuwa hawawezi kufanya usajili. Hata hivyo, wachezaji vijana wamemsaidia kujiweka kwenye mbio za ubingwa na timu kama Liverpool na Manchester City.

Timu hiyo pia imekua na matokeo ya kuvutia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na sasa Lampard ana uhakika wa kuimarisha kikosi chake baada ya adhabu ya kufungiwa kutosajili kusitishwa rasmi.

Pamoja na kwamba, Chelsea sasa wanaweza kufanya usajili kwenye dirisha dogo la Januari, lakini kuna wachezaji ambao wanaweza kuondoka klabuni hapo kutokana na kutokuwa na namba kwenye kikosi cha kwanza. Hapa tunawaangalia wachezaji watatu ambao wanaweza kuondoka Chelsea wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari...

**3. PEDRO RODRIGUEZ**

Raia huyu wa Hispania amekuwa na muda mgumu uwanjani kwa sasa. Ameshindwa kupenya kwenye kikosi cha Lampard. Inaonyesha wazi kwamba siku zake katika jiji hilo la London zinaelekea mwisho na anaweza kuondoka.

Mchezaji huyo aliyelelewa na kituo cha kulea vipaji cha Barcelona pale La Masia, Pedro ameshinda mataji kadhaa katika kipindi chake cha uchezaji likiwamo Kombe la Dunia na mara tatu taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ingawa bado anaonekana ana nafasi ya kucheza kwa miaka kadhaa ijayo, lakini kwa sasa hana nafasi pale Chelsea.

Pedro awali aliwahi kuonyesha nia yake ya kutaka kurudi Hispania, lakini kwa sasa klabu ya Fenerbahce ndiyo inapewa nafasi kubwa zaidi ya kumchukua na pia kuna uwezekano wa kwenda China kwa mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona.

**2. OLIVIER GIROUD**

Mshindi wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa, amecheza mechi tano tu za Chelsea msimu huu, nne kati yake akitokea benchi. Na bado hajafunga bao msimu huu na anaweza kuondoka wakati wa dirisha dogo la Januari.

Kijana Tammy Abraham amekuwa mfungaji mzuri zaidi wa mabao ya Chelsea. Licha ya kucheza mara kwa mara kwenye kikosi cha timu ya taifa ya Ufaransa, lakini pale Chelsea nafasi imekuwa ngumu kwake.

Kuna uvumi kwamba anataka kwenda kuungana na kocha wake wa zamani, Antonio Conte kule Inter Milan, huku pia Crystal Palace ikitajwa kuwania saini yake pamoja na timu za Marseille na Lyon.

**3. MARCOS ALONSO**


Kitu pekee kinachomfanya Marcos Alonso kuwa kwenye kikosi cha kwanza cha Chelsea msimu huu ni kuumia kwa Emerson. Kwa kumtoa na nafasi yake kuchukuliwa na Reece James dhidi ya Ajax kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Lampard alisema kwamba, hamhesabii raia huyo wa Hispania. Hivyo kuna uwezekano mkubwa asiendelee kubakia hapo baada ya Januari.

Akiwa amesajiliwa kutoka Fiorentina kipindi cha majira ya joto mwaka 2016, Antonio Conte alimchezesha kwa mafanikio kama winga.

Chelsea inaonekana ipo tayari kuendelea na maisha bila ya Alonso wakiwa wanamfuatilia kwa karibu nyota wa Leicester City, Ben Chilwell. Uwezo wa Azpilicueta beki ya kushoto kunaaminisha kwamba Lampard haihitaji msaidizi mwingine.

Atletico Madrid imeonyesha nia ya kutaka kumsajili Alonso na kuna uwezekano mkubwa asiendelea kucheza hapo baada ya Januari.

**USILOLIJUA**



Mohamed Salah hadi sasa amefunga mabao 84 katika mechi 126 alizoichezea Liverpool kwenye mashindano yote - ikiwa ni mabao mawili zaidi ya Luis Suarez (82) aliyofunga kwenye mechi 133 wakati akiwachezea Wekundu hao kabla ya kutua Barcelona.



# Watoto 120 mazingira magumu wasaidiwa kwenda sekondari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATOTO 120 wanaoishi katika mazingira magumu, lakini wamefaulu mitihani ya darasa la saba na kutakiwa kujiunga kidato cha kwanza mwakani katika Jiji la Mbeya, wamepatiwa msaada wa daftari 10 kila mmoja kwa ajili ya kuwasaidia kuanza masomo mapema. Msaada huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na mdau wa maendeleo wa Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, ambaye aliahidi kuwapeleka shule za bweni kwa gharama zake wanafunzi hao endapo watafanya vizuri kwenye masomo yao.

Alisema aliamua kutoa msaada huo kwa ajili ya kuwapongeza watoto hao ambao pamoja na kutoka katika mazingira magumu, lakini walifanya vizuri kwenye mitihani yao ya kumaliza darasa la saba iliyofanyika Septemba mwaka huu.

Mwaselela ambaye ni mmiliki wa Shule za St. Patrick Mission za Dar es Salaam, alisema yuko tayari kuwasomesha watoto hao kidato cha tano na sita endapo watafanya vizuri kwenye mitihani ya kidato cha nne.

Pia aliahidi kutoa msaada wa mifuko 50 ya saruji katika shule mbili za kata za Mwasanga na Itigi ambazo baadhi ya watoto hao wanatokea kwa ajili ya kukamilisha vyumba vya madarasa kwa ajili ya watoto hao.

"Najitolea hivi sio kwa sababu mimi ni tajiri hapana, mimi pia ni mtoto wa maskini (mama ntilie), sasa nawasaidia ili nanyi mkifanikiwa mje muwe na moyo wa kuwasaidia wenye uhitaji," alisema Mwaselela.

Kadhalika, aliahidi kuendelea na utaratibu wake wa kusaidia kuboresha miundombinu ya elimu ikiwemo ujenzi wa vyumba vya madarasa, vyoo pamoja na miundombinu mingine.

Aliwapongeza viongozi wa serikali kwa kusimamia vema sekta ya elimu na kuufanya mkoa huo kuwa miongoni mwa mikoa inayofanya vizuri, huku pia akiwashauri wazazi kushiriki kwenye shughuli za maendeleo. Baadhi ya walezi wa watoto hao ambao waliongozana na watoto kupokea misaada hiyo walimshukuru Mwaselela kwa msaada huo kwa madai kuwa utawasaidia kupunguza gharama wakati shule zitakapokuwa zimefunguliwa. Mmoja wa wazazi hao, Furaha Lyenje, alisema asilimia kubwa ya watoto wanaotoka katika mazingira magumu huwa hawaendi shule kutokana na kukosa mahitaji muhimu. Alisema moja ya vitu ambavyo huwa vinawakwamisha watoto hao ni pamoja na sare za shule, daftari pamoja na chakula hivyo akawaomba wadau wengine kuiga anachokifanya Mwaselela ili kuwasaidia watoto hao.



Mdau wa maendeleo Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela (kulia), akimkabidhi msaada wa daftari 10 kwa mmoja ya watoto 120 wa kata saba za Jiji la Mbeya wanaoishi katika mazingira magumu ambao wamefaulu mitihani ya darasa la saba na wanatakiwa kujiunga kidato cha kwanza Januari mwakani. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Kyela yaipa tano serikali mradi wa maji

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WANANCHI wa vijiji nane vya Kata ya Masoko wilayani Kyela, wameishukuru serikali kwa kukamilisha mradi wa maji ya bomba wa Kapapa Group kwa maelezo kuwa utawasaidia kusogeza huduma hiyo karibu na makazi yao.

Walitoa shukurani hizo wakati wa ziara ya Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, ambaye aliuzindua mradi huo ambao umegharimu Sh. bilioni 3.55 na wananchi wakaanza kunufaika.

Diwani wa Kata hiyo, Mpokigwa Mwankuga, alisema kabla ya mradi huo wananchi walikuwa wanahangaika kwa kutembea umbali mrefu kwenda kuchota maji mtoni ambako pia ilikuwa ni hatari kwa maisha yao.

Alisema tatizo hilo lilikuwa linahatarisha afya za wananchi kutokana na kutokuwa na uhakika wa usalama na kwamba mradi huo umekuwa suluhisho la tatizo hilo.

Alisema kutokana na mradi huo kudumu muda mrefu bila kukamilika, wananchi hao walikata tamaa na walikuwa hawana matumaini ya kupata maji ya bomba kwenye maeneo yao.

"Huu ndio mradi pekee ambao tulikuwa tunaamini kuwa utatukomboa lakini baada ya makandarasi kuutelekeza tulikata tamaa kabisa, tunaishukuru serikali kwa kutuona na sasa tunafurahia," alisema Mwankunga. Naye Maines Mwasomola, alisema wanawake na watoto ndio waliokuwa wanapata shida zaidi ya kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta huduma hiyo usiku na mchana.

Alisema maji waliyokuwa wanatumia yalikuwa sio salama kwao na kwamba walikuwa katika hatari kubwa ya kukabiliwa na ugonjwa wa kipindupindu pamoja na magonjwa mengine.

Vile vile, alisema walikuwa wanatumia muda mwingi kutafuta huduma hiyo badala ya kufanya shughuli za maendeleo hasa kilimo ambacho ndicho chanzo kikuu cha mapato yao.

Prof. Mbarawa alisema mradi huo ulikuwa unasuasua kwa muda mrefu kutokana na matatizo ya makandarasi, lakini baada ya serikali kuingilia kati mradi huo umekamilika ndani ya muda mfupi.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wa maeneo ya miji na wilaya wanapata maji kwa asilimia 90 na wa maeneo ya vijijini wawe wanapata maji ya bomba kwa asilimia 85 mwaka 2020.

Alisema mradi huo unatakiwa kuhudumia wananchi 13,000 wa vijiji hivyo, hivyo aliahidi kuwa serikali iko tayari kutoa fedha zingine kwa ajili ya kuongeza vituo vya wananchi kuchota maji.

Prof. Mbarawa aliwataka wananchi hao kuunda jumuia za watumia maji kwa ajili ya kusimamia mradi huo na kukusanya mapato ili iwe rahisi kuutunza mradi huo kwa kufanya matengenezo ya miundombinu inapoharibika. "Mbunge wa Jimbo hili, Dk. Harrison Mwakyembe alikuwa ananisumbua sana kutokana na mradi huu ambao ni wa muda mrefu, sasa Rais aliniagiza nifanye kila linalowezekana ili mradi huu ukamilike na kweli tumeweza," alisema Prof. Mbarawa.

# Latra yaonya wasafirishaji

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imetoa onyo kwa wamiliki na wasafirishaji wa abiria kuzingatia bei elekezi za vyombo vya usafiri katika kipindi cha kuelekea katika msimu wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Ofisa Mfawidhi wa Latra ya Nyanda za Juu Kusini, Denis Daudi, alitoa onyo hilo hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili kuhusiana na changamoto ambayo huwakabili abiria katika kipindi hiki cha kuelekea katika sikukuu hizo.

Alisema ofisi ya Latra imejipanga kukabiliana na wamiliki ambao wamekuwa wakikiuka taratibu na sheria kwa makusudi, zikiwamo kupandisha bei na kujaza abiria kwa lengo la kutaka kujipatia kipato zaidi, na kuwa hali hiyo haiwezi kukubalika na hatua kali zitachukuliwa dhidi yao. Aidha, ofisa huyo alisema kwa sasa wametoa fursa kwa wamiliki na wasafirishaji wa abiria kuongeza magari yenye ubora na yanayokidhi vigezo kwa lengo la kukabiliana na uhaba wa mabasi ya masafa marefu kwenda katika mikoa ya Arusha, Mwanza na Tanga yakitokea Mbeya.

"Mabasi yatakayo kuwa tayari kusafirisha abiria katika mikoa ya Mwanza, Arusha na Tanga yatapewa vibali maalum vya muda mfupi kutokana na kuwapo kwa ongezeko la abiria katika kipindi hiki cha sikukuu za mwaka," alisema. Daudi aliwaonya abiria kuhakikisha wanaenda kukata tiketi za kusafiria katika ofisi za mabasi, badala ya kukata tiketi kwa wapigadebe ambao huishia kuwalaghai abiria na kuleta usumbufu usio wa lazima kwa vyombo vya dola.

"Napenda kuwaasa abiria kwenda katika ofisi za mabasi wanayotakiwa kusafiri nayo kwa lengo la kukata tiketi kwa uhakika zaidi, badala ya kukata tiketi kwa wapiga debe ambao wengi wao huishia kukimbia na fedha za abiria na kuleta usumbufu usio wa lazima," alisema.

Aliongeza kuwa wamiliki na watoaji huduma za usafiri ni lazima wazingatie sheria zikiwamo za kuhakikisha magari yanafungwa mfumo wa udhibiti mwendo, madereva ni lazima wawe mawili kwa mabasi ya masafa marefu na madereva ni lazima wajiepushe na vitendo vya ulevi wakati wa kuendesha vyombo vya moto.

Alisema miongoni mwa majukumu ambayo Latra inasimamia katika usafiri wa ardhini ni kutoa kuhuisha au kufuta leseni, kuratibu usalama wa shughuli za usafiri ardhini, kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva pamoja na kuthibitisha ubora wa vyombo vya usafiri wa abiria na mizigo. Kwa mujibu wa ofisa huyo, Latra ina wajibu wa kuimalisha ustawi wa jamii ya kitanzania ikiwamo kulinda maslahi ya watumia huduma, kuboresha upatikanaji wa huduma kwa watumiaji wote na kukuza elimu, ufahamu na uelewa wa sekta zinazodhibitiwa kwa umma pamoja kulinda na kutunza mazingira.



# Makinda ataka vigezo vya ajira kuzingatiwa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MWENYEKITI wa Mfuko wa Bima ya Taifa (NHIF), Anna Makinda, ametoa rai kwa serikali na mamlaka nyingine za kuajiri katika sekta ya afya nchini, pamoja na vigezo vingine kuzingatia cha upendo kwa watumishi wa afya kwa kuwa ni sehemu ya tiba kwa wagonjwa wanapofika hospitali.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa vifurushi vipya vya bima ya afya vya Timiza, Wekeza na Najali, Makinda alisema kukosekana kwa hali ya upendo kwa wauguzi na madaktari hasa kwa wagonjwa wanaotumia kadi za bima ya afya kumekuwa kukikatisha tamaa na kuondoa hamasa kwa watu wengine wanaotarajia kujiunga na mfuko huo wa bima ya afya.

"Wagonjwa wanaoenda kutibiwa hasa wale wenye bima ya afya wanapokutana na lugha mbaya wanashindwa kuwa mabalozi wazuri wa mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) kwa wananchi wengine ambao hawajajiunga na mfuko," alisema Makinda.

Alisema wauguzi wote waliopo katika vituo vya afya na hospitali waongeze upendo kwa wagonjwa wanaojitokeza kupata huduma za matibabu katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Akizungumzia watu wanaodai vifurushi vya NHIF vilivyoboreshwa ni biashara, alisema sio kweli bali vimeboreshwa kwa staili hiyo ili kila mmoja aweze kumudu kujiunga na mfuko huo.

Alisema vifurushi ni muhimu hivyo ni vema watu wajiunge kabla ya kuugua ili iwe rahisi kupata matibabu.

"Usisite kifurushi ambacho una uwezo nacho hivyo hata usipoumwa hadi mwaka unaisha fedha itatumika kwa mtu mwingine," alisema Makinda.

Naye Mkurugenzi wa NHIF, Bernard Konga, alisema mpaka sasa ni Watanzania milioni nne kati ya milioni milioni 55 wamejiunga na mfuko wa taifa wa bima ya afya.

Alisema tayari wametembelea mikoa 15, ambako wameona kuna upungufu wa madaktari bingwa na wanaendelea na utaratibu wa kuwatafutia madaktari bingwa katika mikoa hiyo.

Alisema kutokana na uboreshwaji huo kuna ongezeko la mapato hadi kufikia Sh. trilioni moja.

Alisema NHIF itaendelea kufuata maagizo ya Wizara ya Afya kuhakikisha mfumo huo unatoa fursa kwa wote kujiunga na bima ya afya.

Naye Naibu Katibu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Edward Mbaga, alisema katika kuhakikisha wagonjwa wanaojiunga na bima ya afya wanahakikisha kuwa hawapati vikwazo vya matibabu.

Mwenyekiti wa bodaboda nchini, Micheal Haule, alisema wanampongeza na kumshukuru Rais Magufuli kutokana na kuwajali Watanzania wote katika suala la afya.

Alisema hivi sasa kila mmoja ana kadi yake ya bima ya afya ya NHIF kutokana na vifurushi vilivyoainishwa vya kujipimia mwenyewe.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, akizungumza na Maofisa Michezo wa Mikoa na Halmashauri za Tanzania Bara waliohudhuria kikao kazi cha siku mbili kilichoongozwa na kauli mbiu "Michezo kwa Afya, Ajira na Maendeleo ya Viwanda" wakati akifunga kikao hicho mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. **PICHA: PETER MWAVILA**

# Wafanyabiashara walia bidhaa kuharibika

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

ZAIDI ya wafanyabiashara 100 wa soko kuu la Majengo jijini Dodoma, wanaofanya biashara katika eneo la Stock yard ya kuuza nyanya na vitunguu, wamedai kuwa bidhaa zao zinaharibika na kusababisha hasara kubwa ya mamilioni ya fedha kwa kuwa eneo hilo lipo wazi.

Madai hayo yalitolewa kutokana na kile walichodai wafanyabiashara hao kusubiri ahadi ya kuezekwa katika eneo hilo iliyoahidiwa na Mbunge wao wa Dodoma, Athony Mavunde, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji. Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara wa soko hilo, Mwenyekiti Hamisi Bomu, alisema kuwa eneo hilo linatumiwa kwa kuuza nyanya na vitunguu vya jumla ambalo lipo wazi na kusababisha hasara hiyo ya mamilioni ya fedha.

Alisema kwa kipindi chote tangu soko hilo lijengwe, wafanyabiashara hao wanapata adha hiyo kwa kufanya biashara kwenye eneo ambalo halina baa hali ambayo imekuwa si rafiki kwao.

Alisema kwa muda mrefu wanafanya biashara katika mazingira magumu hasa kwenye msimu wa mvua na huhifadhi bidhaa zao kwa maturubahi hali inayosababisha mvua zinaponyesha kuharibiwa na maji.

"Ila wao kama wafanyabiashara wana imani kubwa kwa ahadi tuliyoahidiwa na mbunge wetu kwa kushirikiana na halmashauri kuwa eneo hilo adha hiyo inaenda kuondolewa baada ya kutuahidi kuwa hivi sasa pataezekwa ili wafanyabiashara hao waweze kuwa huru kibiashara," alisema Bomu.

Alisema hivi sasa wamepewa ahadi kuwa upauaji wa eneo hilo utaanza hivi karibuni kazi ambayo itafanywa kwa kushirikiana kati ya Halmashauri ya Jiji na Mbunge wa Dodoma.

Alisema kuezekwa kwa eneo hilo kutafanya wafanyabiashara zaidi ya 100 wanaofanya biashara zao eneo hilo kuwa katika mazingira salama ya kufanyia biashara.

"Eneo hili ni la kuuza nyanya za jumla na vitunguu pia pembeni yake kuna wafanyabiashara mbalimbali na kuna mama lishe wanaoleta chakula hapa," alisema.

Alisema kinachowaumiza wafanyabiashara wa soko hilo ni biashara holela inayofanyika nje ya soko na kufanya wateja wengi kuishia nje na kushindwa kuingia ndani na hivyo kusababisha wafanyabiashara wengi wa ndani ya soko kushindwa kufanya biashara kikamilifu licha ya kulipia pango na michango mbalimbali ya soko.

# Waomba kusitishwa mnada wa punda

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WADAU wa sekta ndogo ya wanyama punda wameiomba serikali kusitisha mnada na machinjio ya punda hadi ufanyike utafiti ambao utasaidia kutambua idadi ya wanyama hao ili kukabiliana na changamoto ya uchinjwaji, utoroshaji pamoja na usafirishaji kwenda nchi jirani ya Kenya.

Pia wameomba ijaribu kuishawishi nchi jirani ya Kenya kusitisha shughuli hizo ili kudhibiti utoroshwaji wa punda kutoka nchini Tanzania.

Hayo yalielezwa na wadau hao jijini Dodoma katika kikao chao chenye lengo la kujadili changamoto ya upungufu wa wanyama kazi ambao wengine wanakutwa wamechunwa ngozi na kutupwa katika maeneo mbalimbali.

Mkurugenzi Mtendaji ya Shirika lisilo la kiserikali la The Arusha Society Protection of Animals (ASPA), Livingstone Masija, alisema Tanzania pamoja na kuwapo takwimu sahihi kuhusu wanyama hao, watu wengi wanalalamika kuibiwa wanyama hao hivyo ni wakati muafaka wa serikali kusitisha minada ili kufanya utafiti kwanza.

Masija alisema kupungua kwa wanyama hao kunaathiri shughuli za kibinadamu hususani wanawake pamoja na watoto ambao ndio wanawatumia wanyama hao kuchota maji, kwenda sokoni pamoja na kulima.

"Kuna maeneo mfano kwenye jamii ya wafugaji wanakwambia hawa watoto hawaendi shule, lakini wanawake wamepunguza ufanyaji wa shughuli nyingine za kuwaingizia kipato maana punda wao waliokuwa wanawatumia kuchota maji wameibiwa," alisema.

Alisema wakati anatumia punda alikuwa anaenda mara moja katika shughuli hizo za utekaji maji na nyingine, lakini baada ya kupoteza wanyama hao inamlazimu kubeba ndoo moja kila safari ili idadi ya maji itimie.

"Katika maeneo mengine tunakuta punda wamechunwa ngozi na kutupwa, wengine wanasafirishwa kwenda nchini Kenya, ili kukabiliana na changamoto hiyo tulifanya mkutano maalumu na wadau wa nchi za Afrika Mashariki wa kupitia na kujadili hali ya sasa, ya kijamii na kiuchumi, biashara na madhara ya punda katika hizo," alisema Masija.

Alisema Tanzania na Kenya wanashauriwa kufikiria kutunga sheria kupiga marufuku biashara zote za punda, nyama na bidhaa za kuhusishwa wanyama hao badala yake waweke mikakati ya kuongeza idadi ya punda.

Mkurugenzi mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali linalotekeleza mradi wa kuimarisha maisha (Inades), Herman Hishamu, alisema kupungua kwa idadi ya punda kunaathiri shughuli za binadamu hivyo badala ya kuwaza kuuza punda wananchi wafikirie kuongeza idadi yao ili kukuza uchumi.

"Serikali za kikanda zinapaswa kushirikiana ili kupata ufumbuzi endelevu ikiwa ni pamoja na kuongeza uwekezaji wa punda kupitia mpango wa muda mrefu ambayo utasaidia kukabiliana na changamoto ya kupungua kwa idadi ya punda ili kuisaidia jamii," alisema Hishamu.

Kwa upande wake mkuu wa mnada wa Kizota jijini Dodoma, Januari Kilunga, alisema ni wakati muafaka wa kuishauri Serikali ya Tanzania na Kenya kuzuia biashara ya punda ili kuokoa uhai wa wanyama hao.



# ZEC kuandikisha wapigakura zaidi ya 200,000

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imesema inatarajia kuandikisha wapigakura wapya 204,752 katika kazi ya uandikishaji itakayoanza Desemba 18, mwaka huu.

Hayo yameelezwa na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Jaji Mkuu mstaafu Hamid Mahomoud Hamid, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, mjini hapa.

Alisema kazi hiyo itaanza katika kisiwa cha Pemba, Wilaya ya Micheweni na baadaye Wilaya ya Mkoani Februari 3, mwakani. Kazi hiyo pia itahusisha uhakiki wa taarifa za wapigakura waliomo kwenye daftari la kudumu la wapigakura na wanatarajia kuhakiki taarifa zao wapatao 503,580.

Kadhalika, baada ya kumaliza katika kisiwa cha Pemba watahamia Unguja kuanzia Februari 9, mwakani katika Wilaya ya Kaskazini A na Wilaya ya Mjini Machi 4, mwakani.

Jaji Hamid alisema uandikishaji huo utawahusisha watu wote wenye sifa za kuandikishwa, lakini hawajawahi kuandikishwa katika daftari la kudumu la wapigakura.

Hata hivyo, alisema wapigakura ambao watakwenda vituoni kujiandikisha watatakiwa kwenda na vitambulisho vyao vya Mzanzibari mkaazi vilivyohakikiwa taarifa zao.

Aliwataka Wazanzibari wenye sifa kujitokeza kujiandikisha ili waweze kupata fursa ya kuandikishwa katika daftari la kudumu la wapigakura na ambao waliandikishwa katika chaguzi zilizopita waende kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki taarifa zao.



Kaimu Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Jorg Herrera, akizungumza na Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid, wakati alipomkabidhi vitabu vya kibunge kwa ajili ya maktaba ya Baraza la Wawakilishi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Siku ya Maadili na Haki za Binadamu kuadhimishwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusudia kuadhimisha Siku ya Maadili na Haki za Binadamu kwa lengo la kuondoa ubaguzi na kupambana na uvunjifu wa haki hizo.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa, alisema maadhimisho hayo yanatarajiwa kufanyika kesho katika ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdul Wakil, Kikwajuni mjini Uguja.

Alisema katika kuadhimisha siku hiyo, taasisi zinazosimamia maadili ya haki za binadamu zimefanya shughuli mbalimbali ikiwamo utoaji wa elimu kwa kuandaa na kurusha vipindi, kufanya makongamano na mikutano Unguja na Pemba.

Aliwataka wananchi kushiriki katika maadhimisho hayo kwa kuwa mapambano dhidi ya rushwa, maadili ya uongozi, haki za binadamu ndio chachu ya maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

Kaulimbiu katika maadhimisho hayo ni 'Maadili katika Utumishi wa Umma ni Msingi wa Utawala Bora, Haki za Binadamu na Mapambano ya Rushwa'.

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo anatarajiwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein.

# Wasaidizi wa sheria wasifiwa kutumikia wananchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Katiba na Sheria Zanzibar, Khamis Juma Mwalimu, amesema wasaidizi wa sheria wanafanya kazi kubwa ya kuwatumikia wananchi hasa wa vijijini.

Alisema hayo wakati akifungua kongamano la kitaifa la wasaidizi wa sheria huko lililofanyika mjini Zanzibar.

Alisema kilio cha wasaidizi wa sheria kilikuwa kikubwa kutaka kutambuliwa na kupitia jitihada zilizochukuliwa na Serikali ya Zanzibar katika kuthamini kazi zao, mwaka 2017 ilipitisha sera ya msaada wa kisheria na mwaka 2018 ilipitisha sheria ya msaada wa kisheria namba 13 ya 2018.

Alisema pamoja na mambo mengine pia sheria imeanzisha idara ya msaada wa kisheria ambayo ina jukumu la kuratibu, kuendesha na kusimamia utoaji wa msaada wa kisheria.

Pia alisema wasaidizi wa sheria wamekuwa mstari wa mbele kuwasaidia wana jamii kutatua migogoro mbalimbali katika jamii hasa kwa kutumia njia mbadala za usuluhisho bila ya kuihusisha mahakama.

Alieleza wakati umefika kwa wasaidizi wa sheria kufanya kazi zao kwa weledi na kufuata madili ya kazi yao.

Wizara ya Katiba na Sheria kupitia idara ya msaada wa kisheria ipo katika hatua za mwisho ya kukamilisha kanuni za utendaji za watoa huduma za msaada wa kisheria, zitakapo kamilika itakuwa hatua nyingine muhimu kwa Zanzibar. Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Msaada wa Kisheria Zanzibar, Hanifa Ramadhan Said, alisema kila jamii ina fahamu umuhimu wa msaidizi wa sheria hivyo wasaidizi kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria.

Alisema wasaidizi wa sheria wakiwa wazuri kutoa elimu ndani ya jamii, wananchi watajengwa kujiamini katika mambo ya kisheria. Alieleza kuwa hivi sasa Serikali ya Zanzibar wasaidizi wa sheria wanawatambua hivyo ni wajibu wa wasaidizi hao kushirikiana na masheha ili kutatua migogoro ambayo mwananchi anakutana nayo ya kisheria.

Alisema, katika kufikia malengo ya wasaidizi wa sheria ni lazima kujituma na kufanya kazi bila ya kumwonea mtu.

Kwa upande wake Ali Haji Hassan, kutoka Wizara ya Katiba na Sheria wakati akiwasilisha mada alisema hivi sasa kumekuwa na uhuru mkubwa kwa wasaidizi wa sheria wa kufanya mambo yao kwa kushirikiana na masheha.

Vile vile, katika kutambua umuhimu wa wasaidizi wa sheria serikali imeamua kupitisha sheria ya kuwatambua hiyo ni moja ya mafanikio kwa wataalamu hao.

Alisema hivi sasa kesi nyingi zimekuwa zikitatuliwa na wasaidizi wa sheria kupitia majadiliano na masheha ili kuhakikisha kesi mahakamani zinapungua kwa sasa.

# Wafanyabiashara watakiwa kutumia ubunifu

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

WAFANYABIASHARA wametakiwa kutumia maarifa, ubunifu na weledi katika uzalishaji wa bidhaa sambamba na kulipa kodi, kutunza kumbukumbu kwa mashine za EFD ili kukuza uchumi wa taifa na kujenga misingi mizuri ya biashara. Hayo yalisemwa na Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Msafiri Mbibo, wakati akizungumza na wafanyabiashara wa Mkoa wa Mwanza wakati wa kikao kazi cha kupokea maoni, ushauri na kero ili kufanya maboresho katika miundombinu ya kodi, ambapo alisema ushirikiano kwenye jamii ya wafanyabiashara na walipa kodi ndio itaifanya TRA kufanya vizuri.

Alisema wanashirikiana na wadau kujenga misingi mizuri ya biashara ili kukuza shughuli zote za kiuchumi ili nao waweze kukusanya mapato, hivyo ili kufikia hayo wafanyabiashara wanapaswa kutunza kumbukumbu na kutumia mashine za EFD ambazo zinasaidia utunzaji kumbukumbu pia ya manunuzi na uuzaji wa bidhaa.

"Mnatakiwa kutumia weledi na maarifa ili kuhakikisha biashara zenu zinakuwa endelevu njia pekee ni ya utunzaji kumbukumbu katika kufanya biashara na kuwa na taarifa sahihi, kuwa na weledi kwa kuangalia fursa zilizowazunguka, kutafuta masoko, kuzalisha bidhaa bora pamoja na kufuata taratibu na sheria zilizowekwa," alisema. Na kuongeza kuwa TRA imeleta mfumo wa matumizi ya EFD ambayo inasaidia katika utunzaji wa kumbukumbu hivyo wafanyabiashara wanapaswa kutumia mashine hizo.

Aidha, alisema TRA inajitahidi kutengeneza mazingira bora ya biashara kwa kumfanya mlipa kodi haweze kulipa kodi kwa urahisi kwani ndio hazina ya nchi.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mwanza, Joseph Mtandika, alisema wameanza kutoa elimu ili kuwafikia walengwa pia ni vyema wafanyabiashara wakaitumia Chemba ya Wafanyabiashara na wenye Viwanda na Kilimo Tanzania,(TCCIA) ili kupatiwa elimu inayohusiana na biashara na kuweza kufanya biashara yenye tija kwa maendeleo ya taifa.

Mwenyekiti wa TCCIA, Elibariki Mmari, alisema wafanyabiashara wa Mkoa wa Mwanza ni wengi na walikuwa wanakabiliwa na kero nyingi ambazo zilikuwa zinawakatisha tamaa ya kufanya biashara ipasavyo hivyo imani yao changamoto zao zilizochukuliwa na Naibu Kamishna na zitafanyiwa kazi.



Mafundi wakiendelea na kazi ya kuweka viraka kwenye barabara inayoelekea kwenye Hospitali ya Kairuki Mikocheni jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# MUHAS kushirikiana na chuo kikuu Ufaransa

**Na Faustine Feliciane**

CHUO Kikuu cha Afya na Tiba Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS), kimesaini makubaliano ya ushirikiano na Chuo Kikuu cha Bordeaux cha Ufaransa.

Makubaliano hayo yalisainiwa jijini Dar es Salaam na Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier na Makamu Mkuu wa MUHAS, Prof. Andrew Barnabas, wakati wa hafla ya mdahalo na maonyesho ya vyuo vikuu vinavyoshirikiana na Ubalozi wa Ufaransa.

Akizungumza baada ya kutiliana saini, Pro. Barnabas alisema ushirikiano huo utahusu afya ya mazingira na afya sehemu ya kazi.

"Ushirikiano wetu utahusu zaidi afya ya mazingira kwa binadamu kwenye mwingiliano wa watu na mimea...tutaangalia hasa katika mimea na matumizi ya dawa za viwandani zinavyoathiri afya za binadamu.

Alisema: "Hawa wenzetu wa Bordeuaux wana uzoefu wa muda mrefu na pia ni chuo kikubwa, sisi tuna wanafunzi 4,400 kwa mwaka, wao wana wanafunzi 66,000 wa fani tofauti kwa wakati mmoja.

"Makubaliano haya yatasaidia sana kwenye utafiti wetu na kukuza kazi za kitafiti, lakini pia kusaidia kwenye kutunga sera katika kusaidia taifa kukinga afya za binadamu na maradhi tunayoweza kudhibiti."

Kuhusu ushirikiano huo, Balozi Clavier alisema ni furaha kwa taifa lake kushirikiana na Tanzania, huku akisisitiza kwamba ufadhili wa masomo watakaopata Watanzania utaletea manufaa taifa hili chimbuko la lugha ya Kiswahili.

# Tanga yasaidiwa mil. 40/- elimu, afya

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kusaidia utatuzi wa changamoto zinazoikabili sekta ya afya na elimu, ilitenga kiasi cha Sh. bilioni 1 kwa mwaka kurejesha kwa jamii, Benki ya NMB imetumia Sh. milioni 40 kutoa misaada ya vifaa vya ujenzi na elimu katika shule mbalimbali kwenye wilaya za mkoa wa Tanga.

Desemba 10 mwaka huu, NMB ilikabidhi madawati na vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa shule mbili katika wilaya za Korogwe na Mombo, huku Desemba 11 ikitoa misaada kama hiyo kwa wilaya za Handeni na Kilindi Sh. milioni 5 kila wilaya).

Wilaya zingine za Mkoa wa Tanga zilizonufaika na misaada hiyo ni Pangani (vifaa vya afya vyenye thamani ya Sh. milioni 5) na Wilaya ya Mkinga (madawati, vifaa tiba na vifaa vya ujenzi – vyenye thamani ya Sh. milioni 15), wilaya zilizosaidiwa Desemba 12.

Kiasi hicho kinaifanya NMB kufikisha zaidi ya Sh. milioni 900 sasa inapokaribia kuumaliza mwaka 2019, ambao waliutengea kiasi cha Sh. bilioni 1, ambayo ni sawa na asilimia moja ya faida yao kwa ajili ya kusaidia utatuzi wa changamoto za kijamii kwenye Sekta za Elimu na Afya.

Wilayani Handeni, NMB kupitia Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro, ilikabidhi viti pamoja na meza 50 kwa Shule ya Sekondari Kisaza iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, ambavyo vilipokelewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Godwin Gondwe.

Gondwe alitoa shukrani kwa NMB kwa msaada mkubwa walioutoa kwa shule zote wilayani mwake, na kwamba madawati hayo yametatua kero ya wanafunzi wa kidato cha tano katika Shule ya Kisaza, jambo ambalo litaongeza hamasa ya kusoma na kukuza kiwango cha ufaulu wilayani Handeni.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, William Makufwe, alisema kiwango cha ufaulu kwenye halmashauri kimeongezeka kutoka asilimia 62.2 mwaka 2016 hadi asilimia 87.7 kwa mwaka 2019, jambo ambalo ni mikakati ya serikali wilayani humo kuongeza kiwango cha ufaulu.

Awali Mkuu wa Shule ya Sekondari Kisaza, Leonard Mshana, alisema changamoto ya madawati imetokana na shule hiyo kupangiwa wanafunzi wapya kwa kidato cha tano Septemba mwaka huu, ambapo kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pamoja na Mkurugenzi wa Handeni, wakapeleka maombi NMB.

Wilayani Korogwe, Muro pia ndiye aliyekabidhi msaada wa mabati 150 ya kuezekea pamoja na meza 52 na viti 52, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 10 kwa Shule ya Sekondari Patema na Shule ya Msingi Mkumbara, zilizopo wilayani humo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, Mandia Kihiyo, alisema wamepokea msaada mkubwa kutoka kwa NMB, kwani wanaunga mkono kwa dhati juhudi za Rais John Magufuli za kutoa elimu bure katika nchi yetu.

Naye Ofisa Elimu Sekondari Korogwe, Mwalimu Sophia Msofe, alisema wamekuwa wakihangaika kuomba misaada katika taasisi mbalimbali, lakini hakuna hata moja iliyoguswa na kupeleka mrejesho, isipokuwa NMB baada ya kusikia changamoto yao, hawakuchukua muda wamewasaidia haraka sana.

## HABARI KIMATAIFA

### Mkutano wa tabianchi waibua maswali kibao

**MADRID,** Hispania

MKUTANO wa hali ya hewa wa COP 25 wa Umoja wa Mataifa unaofanyika mjini Madrid, Uhispania bado haujafikia suluhisho. Mkutano huo wa wiki mbili ulipangiwa kumalizika Jumamosi.

Wajumbe kwenye mkutano huo wanajadili jinsi ya kukabiliana na matatizo yanayosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na pia kuhusu nani anayepaswa kugharamia. Kuna wasiwasi kwamba wajumbe kwenye mkutano huo hawatofaulu kufikia suluhisho.

Mataifa tajiri, yale yanayoendelea pamoja na nchi maskini yalikataa rasimu iliyowasilishwa na mwenyeji wa mkutano huo Chile katika jaribio la kupata makubaliano ya msingi. **DW**

### Rais mpya Algeria akingiwa kifua jeshini

**ALGIERS,** Algeria

JESHI la Algeria lenye ushawishi, jana liliahidi kumuunga mkono Waziri Mkuu wa zamani wa nchi hiyo, Abdelmadjid Tebboune, aliyechaguliwa kuwa Rais wa nchi hiyo katika uchaguzi uliofanyika Alhamisi.

Uchaguzi huo umefanyika baada ya miezi kadhaa ya maandamano. Mkuu wa majeshi nchini humo, Gaid Salah, alimpongeza Tebboune na kusema kuwa ni mtu sahihi mwenye uzoefu na mwenye uwezo wa kuiongoza Algeria kuelekea hatma bora ya baadaye.

Hata hivyo, pamoja na kuchaguliwa kwake, raia wa Algeria waliandamana Ijumaa katika mji mkuu Algiers na miji mingine kupinga ushindi wake. Tebboune anachukua nafasi ya mtawala wa muda mrefu, Abdel Aziz Bouteflika, aliyelazimika kujiuzulu Aprili baada ya maandamano na shinikizo la jeshi. **DW**

### Polisi wakabiliana na waandamanaji

**BEIRUT,** Lebanon

POLISI wa kupambana na ghasia walikabiliana na waandamanaji mjini Beirut baada ya waandamanaji hao walipojaribu kuingia katika eneo lilipo Bunge la Lebanon.

Waandamanaji walijaribu kuingia kwenye eneo la Najmeh lenye ulinzi mkali juzi usiku kwa kuvisukuma vizuizi vya chuma, hatua ambayo ilisababisha polisi wa kupambana na ghasia na walinda usalama kufyatua gesi ya kutoa machozi ili kuwatawanya waandamanaji hao.

Maandamano yamekuwa yanafanyika nchini Lebanon tangu katikati ya mwezi Oktoba huku mtikisiko wa kiuchumi na kisiasa ukiwa umeitumbukiza nchi hiyo kwenye hali mbaya zaidi. **DW**

# Mtoto asoma shule ya siri Cameroon

**DOUALA,** Cameroon

MVULANA mwenye umri wa miaka 11, Mackjourney, huenda kusoma katika shule ya siri nchini Cameroon.

Wakati hivi karibuni familia yake ilivyotoroka uasi wa wanaotaka kujitenga katika majimbo yanayozungumza Kiingereza, walifikiri kuwa wamepata mahali ambapo anaweza kuwa anasoma kwa usalama.

Lakini hilo limegeuka kuwa ni kinyume kwani shule anayosoma mjini Douala, iko katika hatari ya kufungwa kwa sababu inaonekana na maofisa wa serikali kuwa ni shule haramu. Shule kama hizo zisizokubalika kisheria zimeanzishwa kwa haraka mjini Douala, ambako wengi wa wakazi ni wazungumzaji wa lugha ya Kifaransa.

Nyingi kati ya shule katika majimbo yanayozungumza lugha ya Kiingereza kaskazini- Magharibi ikiwamo mjini Bamenda, na Kusini-Magharibi zimefungwa kwa miaka mitatu iliyopita, na kuwafanya watoto zaidi ya 600,000 kukosa shule.

**Niliondoka Bamenda kwa sababu kulikuwa na vita walikuwa wanawaua watu na kuwapiga risasi.**

"Niliondoka Bamenda kwa sababu kulikuwa na vita walikuwa wanawaua watu na kuwapiga risasi," Mackjourney aliiambia BBC.

Shule ambazo bado zimefungwa ziko katika hatari ya kushambuliwa na wapiganaji wanaotaka kujitenga.

"Tulikua tunakaa darasani na kusikia risasi zinaanguka kwenye paa la darasa kama mvua. Ilikua inatisha," alisema.

Mackjourney hutembea mwendo wa kilomita 2 (zaidi ya maili moja) kila asubuhi akipitia njia nyembamba katika eneo la vichaka kwenda katika shule yake, iliyotengenezwa kwa mbao bila madirisha.

Kutoka ndani ya darasa wanaweza kuona majani marefu pande zote. Eneo hilo limechaguliwa ili iwe vigumu kugundulika na mamlaka. Kuna shule ya pili ya kibinafsi ambayo alisomea mjini Douala - ya kwanza ilifungwa na serikali kwa kuwa haikuidhinishwa.

Maofisa wa serikali nchini humo wanasema kuwa shule ni lazima iwe na uwanja wa kuchezea, maktaba na madarasa ili isajiliwe rasmi.

Lakini wamiliki wa shule hizi, wako tayari kuvunja sheria kwani kuna pesa ambazo wanapata kutoka kwa wazazi wanaohangaika kuwapatia watoto wao elimu.

Mzozo ulianza mwaka 2016 kufuatia uamuzi wa serikali wa kuongeza matumizi ya Kifaransa katika shule na mahakama hususan ni katika majimbo yanayozungumza Kiingereza. **BBC**



Mtoto Mackjourney akienda katika shule ya mafichoni nchini Cameroon kutokana na mzozo uliopo nchini humo, kati ya wazungumzaji wa lugha ya Kiingereza na wazungumzaji wa Kifaransa. **PICHA: BBC**

## Chama kinachopinga wahamiaji chakosolewa

**ROMA,** Italia

CHAMA kinachotumia nembo ya samaki "Sardines," kinachoendeleza harakati za kupinga sera za mrengo wa kulia za chama cha League cha Italia na kiongozi wake, Matteo Salvini, kilifanya mkutano wake mkubwa kabisa mjini Rome Jumamosi.

Mkutano huo ulifanyika katika eneo la Piazza San Giovanni, ambapo maelfu ya watu walikusanyika huku vyombo vya habari vya ndani vikikadiria kuwa watu wapatao 100,000 walihudhuria.

Wanaharakati wa chama hicho cha Sardines wanapinga kauli za chuki na ubaguzi za chama cha League cha Matteo Salvini kinachopinga wahamiaji.

Mwakilishi wa chama cha Sardine mjini Rome Stephen Ogongo, mwandishi wa habari mwenye umri wa miaka 45 kutokea nchini Kenya, amesema kwamba kiongozi wa chama cha mrengo wa kulia, Matteo Salvini, amechochea kustawi ubaguzi nchini Italia.

Wanaharakati hao pia wanapinga makundi ya mafia, mabadiliko ya hali ya hewa, na umaskini nchini Italia.

Bwana Salvini ameeleza kuwa anataka kuongeza umaarufu wa chama chake katika kila mkoa nchini Italia ili kuiondoa madarakani serikali ya mseto ya vyama vya Nyota Tano na Chama cha Kidemokrasia cha kushoto na kwa kulazimisha ufanyike uchaguzi mpya. **DW**

# Kortini tuhuma kulisha abiria biskuti, kuwaibia

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU watatu waishio maeneo tofauti nchini, wamefikishwa Mahakama ya Wilaya ya Lindi, wakikabiliwa na mashtaka mawili, likiwamo la kuwapa biskuti zenye dawa za usingizi baadhi ya abiria kisha kuwaibia fedha na vitu mbalimbali.

Walifikishwa mbele ya Hakimu Elimo Massawe na kusomewa mashtaka na Mwanasheria wa Serikali, Abdurahamani Mohamed.

Watuhumiwa hao ni dereva Saadati Issa Kibainzi (40), mkazi wa Ubungo jijini Dar es Salaam; Kamugisha Phillemon Mtafungwa (43), mkazi wa Sinza, jijini Dar es Salaam na Godfrey Sebastian Laurent (40), mkazi wa Kijiji cha Kashenye, Wilaya ya Bukoba, mkoani Kaera.

Mohamed alidai kuwa Novemba 26, mwaka huu majira ya usiku kati ya vijiji vya Nangurukuru na Mavuji wilayani Kilwa, mkoani Lindi, washtakiwa waliwalisha biskuti abiria Dadi Mohamedi Issa na Omari Issa Buriani kisha kuwaibia.

Alidai washtakiwa na abiria hao na wengine, walikuwa wakisafiri kwa basi la Kampuni ya Buti la Zungu namba T 237 DRM kutoka Dar es Salaam kuelekea mikoa ya Lindi na Mtwara kisha kuwaibia vitu mbalimbali, yakiwamo mabegi ya nguo, kompyuta mpakato moja, kadi nne zikiwamo mbili za Benki ya NMB, bima ya afya, kupigia kura, vitambulisho vya uraia na fedha taslimu Sh. 107,000.

Mwanasheria huyo aliendelea kudai kuwa washtakiwa hao walipata mwanya wa kuwaibia, baada ya kupoteza fahamu kutokana na biskuti walizokula kuchanganywa na dawa zinazosadikiwa kuwa ni sumu.

Aidha, alidai kuwa kufuatia kitendo hicho, washtakiwa wamefanya makosa kwa mujibu wa vifungu 265 na 277 Kanuni ya Adhabu sura ya 16 rejeo la 2002.

Hata hivyo, washtakiwa hao walikana mashtaka na kupelekwa mahabusu, baada ya kukosa wadhamini, huku kesi yao namba 24/2019 ikipangwa kutajwa tena wiki mbili zijazo.



Mkurugenzi Mtendaji wa UBA Bank, Usman Isiaka (kulia), akifanyiwa mahojiano na mtangazaji Deogratius Kithama wa East Africa Television katika mwendelezo wa kampeni ya Kibiashara Zaidi, ambapo alielezea juu ya uwekezaji mkubwa ambao benki hiyo imefanya. **PICHA: EATV**

# Ubia kilimo wainua wakulima Mbarali

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wa mpunga wilayani Mbarali mkoani Mbeya, wameeleza kuridhishwa kwao na mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi wa ubia wa kilimo Tanzania unaotekelezwa wilayani humo kupitia Baraza la Kilimo Tanzania.

Wamesema tangu kuanza kutekelezwa kwa programu hiyo, wameanza kufanya kilimo kibiashara baada ya kufundishwa kutumia njia bora za kilimo.

"Nilikuwa nimezoea kulima kienyeji bila hata kuweka mbolea na mbegu nilikuwa naweka zozote tu ilimradi nipande na kimsingi nilikuwa namwaga, jambo ambalo lilikuwa linafanya nipate mazao kidogo tu ya kujikimu, lakini tangu hawa jamaa waje nimeanza kuona umuhimu wa kilimo, lakini kama utafuata mbinu za kitaalamu," alisema Shabani Ismail.

"Kwa heka zangu tatu tangu nianze kutumia mfumo huu wa kilimo cha kisasa ninapata gunia hadi 90 za mpunga, na ninapata hadi ziada ya kuuza, kitu ambacho zamani hakikuwapo nilikuwa nikivuna naweka kwa ajili ya chakula basi," alisema Husna Abdulmariki, mkulima wa mpunga Chimala.

Kwa mujibu wa mratibu wa programu hiyo mkoani Mbeya, Rojaz Masha, wilaya hiyo ni miongoni mwa halmashauri zilizonufaika na programu ya ubia wa kilimo tanzania awamu ya pili, lengo ni kuhakikisha inatoa fursa kwa wakulima kunufaika na sekta ya kilimo.

"Programu ya TAP II imesaidia kwa kiasi kikubwa kuwa na ongezeko la uzalishaji hasa katika zao la mpunga baada uhamasishaji, ambapo kwa sasa wakulima wengi wanatumia teknolojia ya kilimo shadidi katika zao hilo," alisema Masha.

"Programu ya TAP II imesaidia pia shughuli za kilimo ambapo sasa kuna ongezeko la uwekezaji kwenye miundombinu ya umwagiliaji, maghala na mitambo ya kusindika mpunga.

"Miongoni mwa mafanikio makubwa tuliyoyapa hapa Mbarali kwa kushirikiana na Shirikisho la Wakulima Mbarali (AMBERICO) tumewawezesha wakulima ndani ya shirikisho kuifikia mikopo ya pembejeo (toka YARA) na fedha (toka NMB) pamoja na kufikia soko na kuuza kwa pamoja mazao yao," alisema Masha.

Alisema kuwa programu ya TAP II imeshiriki kikamilifu katika ujenzi wa maghala na uwekezaji wa mitambo ya kusindika mazao jambo linalothibitisha mwitikio mkubwa kwenye kujibu mpango wa uwekezaji kwenye zao.

"Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na Maghala unaofanywa na serikali kupitia Halmashauri za Wilaya ni kudhihirisha utekelezwaji wa CIP na yote hayo yanaonyesha kuimarika kwa ushirikiano," alisema.

"TAP II pia imetoa msaada wa ujenzi wa ghala la kuhifadhi mpunga kwa kushirikiana na Shirikisho la Wakulima Mbarali ili kuwaondolea wakulima adha ya kukodisha maghala ya kuhifadhia mpunga kabla ya kuuza kwa pamoja."

Akizungumzia mafanikio ya programu hiyo Meneja wa AMBERICO, Steven Mwapwani, alisema kupitia programu hiyo wamefanikiwa kuwa na uhakika wa soko la mazao yao baada ya kuyavuna, huku pia wakulima wakiwa na uhakika wa kupata pembejeo na mbegu bora kwa wakati.

"Wakulima wote walioko kwenye shirikisho letu wana uhakika wa kupata mbegu bora na pembejeo zote pamoja na mikopo ya fedha kutoka Benki ya NMB, na hii inatokana na uhakika wa soko tulilonalo," alisema Mwapani.

# Maisha ya abiria bodaboda rehani

**Na Beatrice Moses**

MFUMO wa ukataji wa bima za pikipiki unatajwa kuweka rehani maisha ya abiria wa vyombo hivyo, kwa kuwa umetenganishwa na wamiliki wengi hufanya kuwa wa hiari.

Hayo yamebainishwa mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa chama cha mawakala wa bima nchini.

Akizungumza katika mahojiano ya gazeti hili Mwenyekiti wa chama hicho, Sayi Daudi, alisema kiwango cha bima ya pikipiki inaanzia Sh. 50,000 ambayo haimhusu abiria.

"Utaratibu ulivyowekwa ni kwamba abiria anapaswa kukatiwa yake, lakini wengine hawaoni umuhimu kuikata, hatua ambayo imekuwa ikiwasababishia usumbufu abiria wengi inapotokea ajali kwa vyombo hivyo," alisema.

Daudi alisema wao kama mawakala wanapenda kuona bima zote zinapewa uzito ili huduma hiyo iwanufaishe wote wanaostahili.

Alisema wana furaha kufanikiwa kuanzisha chama hicho ambacho kitawasaidia kufanya kazi yao kwa ushirikiano wenye manufaa ya jumla kwenye sekta hiyo.

Daudi alisema mawakala wamekuwa na jukumu la kuunganisha wateja na kampuni hadi kufikia hatua ya kuandikiana mikataba.

Awali Kamishna wa Mamlaka ya Bima Tanzania (Tira), Dk. Mussa Juma, akizungumza katika hafla hiyo alisema juhudi za kuboresha na kuinua vipato vya wananchi zinazofanywa na serikali zikifanikiwa zitasaidia kuhamasisha wananchi wengi kukata bima ya maisha.

Dk. Juma alisema wenye kipato kidogo hufikiri kukata bima ya maisha ambayo ni sawa na uwekezaji, wakati hawana uhakika wa kupata chakula na kulala.

Dk. Juma aliwataka mawakala hao kuhakikisha wanakitumia vyema chama hicho ikiwamo kushiriki kikamilifu katika kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kukata bima," alisema.

Meneja Masoko wa Kampuni ya Bima ya Icea Lion, Davis Mwijage, alisema miongoni mwa mambo yatakayosaidia mafanikio ya utekelezaji wa sera ya uchumi wa viwanda ni pale mwekezaji atapokata bima ya ulinzi wa mali zake hivyo kuwa na amani.

Mwijage alizungumzia kuhusu uzinduzi huo kwamba zaidi ya asilimia 60 ya soko la bima linaendeshwa na mawakala na madalali wa bima ya afya, hivyo wanaunga mkono juhudi zao za kuanzisha chama hicho.

# Benki Kilimo yataja mafanikio miaka 4

**Na Juster Prudence**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imeeleza juu ya mchango wa serikali ya awamu ya tano katika ukuaji wake na mafanikio yaliyopatikana.

Akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Japhet Justine, alisema mafanikio waliyonayo sasa kama benki pamoja na faida imetokana na mchango mkubwa wa Rais Magufuli na serikali kwa ujumla.

Alisema wakati benki inaanza mwaka 2015 serikali ilitoa zaidi ya Sh. bilioni 300 ambapo Sh. bilioni.60 zilikuwa ni kwa ajili ya mtaji wa benki, Sh. bilioni 208 kama fedha ambayo benki itatumia kwa ajili ya kujiendeshea na kutoa mikopo pamoja na Sh. bilioni 44 kwa ajili ya kilimo zaidi.

Kwa mujibu wa Japhet, benki imefanikiwa kutoa mikopo ya zaidi Sh. bilioni 148 mpaka sasa kwa zaidi ya viwanda 13 na miradi 40 ikiwa ni pamoja na Sh. bilioni 1 kwa ajili ya sekta ya uvuvi, Sh. bilioni 2.9 kwa ajili ya mpango wa maendeleo ya kilimo na kuongeza uzalishaji kwa kununua trekta, Sh. bilioni 17 katika miradi ya umwagiliaji Bagamoyo, Pwani, Rufiji na Tanga pamoja na Sh. milioni 60 katika uvunaji wa asali.

"Tumetoa mikopo kwa vyama vya ushirika 99 ambavyo ni vyama vya msingi pamoja na vyama vikuu viwili," alisema Japhet.

Pia wamefanikiwa kujenga mahusiano mazuri na benki nyingine zikiwamo CRDB, NMB na FINCA ambapo wametoa Sh. bilioni 18.2 kati ya Sh. bilioni 36.2 kwa ajili ya ushirikiano na benki hizo.

Aliongeza kuwa kwa mwaka mmoja walioshirikiana na benki hizo, wamefikia miradi zaidi ya 5,000 kuwezesha viwanda vingine 19 kwa kuongeza Sh. bilioni 8 kutoka katika benki hiyo na Sh. bilioni 11 kwa ajili ya kununua pembejeo msimu huu.

Japhet alisema malengo yao mwaka 2020 ni kupata maeneo ya kuwekeza zaidi hususani katika zao la pamba ambapo wana mpango wa kutoa elimu kwa wakulima wadogo juu ya uongezaji wa thamani katika pamba jambo litakalowezesha kuongeza mapato yao.

Alisema zao la katani kwa sasa wanazalisha zaidi ya tani 40,000 kwa mwaka na kwamba kwa zao la korosho wana mpango wa kuwezesha wadau wanaotaka kuanzisha viwanda vya kuibangua nchini.

Kwa zao la kahawa hususani mkoani Kagera, mpaka sasa wamewekeza Sh. bilioni 50 kwa ajili ya mitaji pamoja na sekta ya umwagiliaji ambayo kwa miaka minne iliyopita waliwekeza Sh. bilioni 17.

Japhet alieleza baadhi ya changamoto wanazokabiliana nazo ni kutorudisha mikopo kwa wakati.

# Wito ujenzi viwanda saruji Kanda ya Ziwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAFANYABIASHARA mkoani Shinyanga, wametakiwa kujenga viwanda vya saruji katika mikoa ya kanda ya ziwa ili kuwawezesha wananchi wenye vipato vya chini kumudu gharama za ununuzi wa bidhaa hiyo na kujenga nyumba za kisasa.

Wito huo ulitolewa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, katika kongamano la wafanyabiashara, makandarasi na wazabuni wa mikoa ya Kanda ya Magharibi kwa lengo la kujadili shughuli za maendeleo katika mikoa hiyo.

Alisema wananchi wa Kanda ya Ziwa wanashindwa kujenga nyumba za kisasa kutokana na bei ya saruji kuwa kubwa, na kutolea mfano kwa mkoa wa kagera ambako mfuko mmoja wa saruji unauzwa kuanzia Sh. 29,000, kiasi ambacho ni mara mbili ya mikoa ya Kanda ya Pwani.

"Hatutaweza kukuza uchumi wa mikoa ya kanda hii kama bei ya saruji itaendelea kuwa juu kiasi hiki, sisi kama serikali tupo tayari kuwasaidia wawekezaji wa ndani ili kujenge viwanda vya saruji katika mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Geita na Tabora," alisema Bashungwa.

Aliongeza: "Kahama tuna mwekezaji mkubwa anayemiliki kiwanda cha Kahama Oil Mill na amekuwa akijenga viwanda mbalimbali katika mikoa ya Mwanza na Pwani...nimwombe achangamkie fursa hii na kujenga kiwanda cha saruji ukanda huu wa ziwa ili gharama ya saruji zisiendelee kuwa kubwa."

Aidha, Bashungwa alisema katika mikoa yote ya Kanda ya Ziwa malighafi yote inayotumika kutengenezea saruji ipo, hivyo wawekezaji wasiwe na hofu ya kupata hasara kwani uhakika wa soko ni mkubwa na itasaidia wananchi kumudu gharama hizo.

Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa mikoa ya kanda hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, alisema serikali imeandaa sera nzuri za kuwawezesha wawekezaji wa ndani kwa kuwapa maeneo ya uwekezaji na kujenga viwanda.

Hata hivyo, alisema katika kuelekea uchumi wa kati, ni lazima wawekezaji wa ndani wapewe kipaumbele katika shughuli mbalimbali wanazozifanya hasa katika kujenga viwanda na hii imekuwa ikisaidia kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana.



Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Marco Saguti (wa tatu kushoto), akishikana mikono na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, wakati mkurugenzi huyo pamoja na ujumbe wake walipomtembelea ofisini kwake katika ziara yao mkoani Kagera hivi karibuni. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wasanii maarufu nchini kutangaza vivutio vya utalii

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (Tanapa), limezindua kampeni maalumu ijulikanyo 'Talii na Tanapa Msimu huu wa Sikukuu ya X-mass na Mwaka mpya' kwa kushirikisha wasanii maarufu, warembo, watangazaji maarufu na watu maarufu lengo ni kutaka kuhamashisha Watanzania kutembelea hifadhi za taifa badala ya kwenda kutalii nje ya nchi katika kipindi hicho.

Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa Tanapa, Witness Shoo, alisema hayo mbele ya waandishi wa habari kwa kushirikisha viongozi wa uhifadhi, wasanii na watangazaji, jijini Arusha.

Shoo alisema kuwa lengo la Tanapa ni kutaka kila Mtanzania kuwa mzalendo na nchini yake kwa kutembelea vivutio vilivyokuwa katika hifadhi 22 nchini kwa kuvitembelea na kuwa balozi wakubwa wa kuvitangaza.

Alisema kundi la kwanza la wasanii, watangazaji na watu maarufu litaanza kufanya kampeni hiyo Desemba 20 mwaka huu katika hifadhi sita ikiwamo Ruaha, Katavi, Mkomazi, Rubondo, Mikumi na Hifadhi ya Gombe, mkoani Kigoma.

Alisema katika Hifadhi ya Ruaha, msanii Idris Sultan atakwenda kutalii katika mbuga hiyo na kuitangaza ndani na nje ya nchi katika mitandao ya kijamii kwa kuwa ana wafuasi wengi katika mitandao ya kijamii hivyo anawajibu wa kutoa ujumbe kwa Watanzania kuacha kukimbilia nje ya nchi kutalii badala yake watembelee hifadhi taifa.

Alisema msanii Mrisho Mpoto atakuwa katika Hifadhi ya Katavi, mrembo Nancy Sumary atakuwa katika hifadhi ya Mkomazi, mtangazaji kijana aliyejipatia umaarufu nchini, Milard Ayo na Miss wa mwaka 2018 Elizaberth Makune, watakuwa na jukumu la kuwakumbusha Watanzania kutembelea hifadhi ya Robondo.

Wengine ni pamoja na wasanii wa muziki wa Bongo Fleva Lulu Abas, maarufu kwa jina la Lulu Diva, atakuwa katika Hifadhi ya Mikumi na msanii aliyetambulika kwa jina moja la Rubby atakuwa katika hifadhi ya Gombe.

Naye Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Tanapa, Pascal Shelutete alisema kuwa lengo la kampeni hiyo ni kuwataka Watanzania kuwa na tabia ya kutembelea mbuga za wanyama katika vipindi vyote vya Sikukuu ya Krismasi na Mwaka mpya na sikukuu nyingine kwa kutumia kiasi kidogo cha fedha na pia kuvitangaza vivutio hivyo kwa faida ya nchi.

Shelutete alisema kuwa wasanii wa fani mbalimbali, watu maarufu na watangazaji watashirikishwa katika kampeni hiyo iliyolenga kumtaka Mtanzania kupenda cha nchi yake na kuacha kujali vya nje.

Naye msanii Idris alisema katika maisha yake hajawahi kufika katika Hifadhi ya Ruaha hivyo kwa fursa aliyopewa atahakikisha anaitangaza hifadhi hiyo kwa kadri awezavyo lengo ni kutaka Watanzania kuwa wazalendo na kupenda cha kwao na kuacha ulimbukeni wa kikumbilia nje ya nchi kama Dubai na kwingine kwa kutumia mamilioni ya pesa bila ya sababu za msingi.

# KLOPP ASHTUSHWA MPANGO LIGI YA MABINGWA ULAYA



**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amebainisha upinzani wake juu ya madai kwamba Ligi ya Mabingwa Ulaya inatakiwa kupanuliwa na kufanya iwe na michezo mingi zaidi.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, klabu kubwa za Ligi Kuu England ikiwamo Liverpool zinaunga mkono mpango wa kuona mfumo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya unaundwa upya.

Hatua ya makundi ambayo kwa sasa inacheza mechi sita, sasa inatakiwa ipanuliwe hadi mechi 10 kwa timu, gazeti hilo la Uingereza limeripoti.

Hatua hiyo itaongeza mapato kwa timu, lakini pia itakuwa na athari kwa ratiba za Ligi Kuu. Timu ya Klopp inaongoza kwenye Ligi Kuu na wiki hii inakwenda nchini Qatar kwenye michuano ya Klabu Bingwa ya Dunia baada ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa msimu uliopita.

Majeruhi yanaanza kuwaandama vijana hao wa dimba la Anfield, huku Georginio Wijnaldum akiwa ameuumia juzi Jumamosi wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Watford.

Timu moja ya Liverpool itacheza na Aston Villa kwenye Kombe la EFL Jumanne, kabla ya nyingine kucheza kwenye Klabu Bingwa Dunia pale Monterrey.

"Ratiba kama zilivyo. Wanapenda kuona sisi tunapata tabu na hivyo ndivyo ilivyo," alisema Klopp.

"Unaweza kuangalia jinsi ilivyo, lakini mwisho wa siku hakuna anayejali."

Aliongeza: "Leo nimesoma habari ikisema kwamba klabu kubwa zinataka mechi zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Mimi sijahusishwa kwenye mipango hiyo. Huo ni upuuzi kwa kweli.

# Rodgers: Leicester haitauza nyota wake

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers amesisitiza nyota wake James Maddison hatauzwa kwa Manchester United wakati wa dirisha dogo la usajili.

Nyota wa Leicester wamekuwa wakiwaniwa na klabu kadhaa baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye Ligi Kuu ya England, huku Ben Chilwell naye akiwa anawindwa na Chelsea.

Lakini, Rodgers, ambaye aliwahi kuwa kocha wa Liverpool alisema makocha wenzake, akiwamo Ole Gunnar Solskjaer wasisumbuke kwa sababu hakuna mchezaji atakayeruhusiwa kuondoka kwenye dirisha la Januari.

Kocha huyo alidai mpango wake ni kuhakikisha hauzwi mchezaji yeyote kwenye kikosi chake huku kauli hiyo ikiwa na ujumbe mzito kwa Ole, ambaye mipango yake ni kwenye kuisuka upya Man United kuwa timu ya kibabe huko Ulaya.

"Hatuna mpango wowote wa kuuza nyota wetu Januari, hivyo klabu zinazowafikiria wachezaji wetu zinatakiwa kutofikiria mpango huo," alisema Rodgers.



# Ribery afanyiwa upasuaji kukaa nje wiki 10



**FLORENCE,** Italia

NYOTA wa Fiorentina, Franck Ribery anatarajiwa kukaa nje ya dimba kwa wiki 10 baada ya kufanyiwa upasuaji wa kifundo cha mguu juzi, Jumamosi.

Ribery mwenye umri wa miaka 36, aliumia wakati Fiorentina ikifungwa 1-0 na Lecce kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Novemba 30.

Fiorentina ilitangaza Jumamosi kwamba, mshambuliaji huyo wa Ufaransa amefanyiwa upasuaji na wanamtarajia kurudi uwanjani na kuanza mazoezi baada ya wiki 10.

"Franck Ribery leo (juzi) amefanyiwa upasuaji," taarifa ya klabu hiyo ilisema.

"Operesheni hiyo ilifanywa na profesa, na ilikuwa na mafanikio makubwa.

"Mchezaji huyo alitarajiwa kurudi mjini Florence jana Jumapili kwa ajili ya kujiuguza. Ataanza mazoezi ndani ya wiki mbili zijazo.

"Atakuwa amepona na kuanza mazoezi kamili wiki 10 zijazo."

Ribery amefunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho mbili katika mechi 11 za Ligi Kuu msimu huu.

HABARI MICHEZO



# GUARDIOLA ALIA CITY KUATHIRIWA NA MAFANIKIO

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anaamini Manchester City wamekuwa waathirika wa mafanikio yao kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu.

City wameshinda taji la Ligi Kuu mara mbili mfululizo kwa miaka miwili iliyopita, wakipata jumla ya pointi 198, na kutengeneza rekodi kwenye soka la Uingereza.

Lakini baada ya kuwashinda Liverpool kwa pointi moja msimu uliopita, vijana hao wa Guardiola sasa wamepitwa pointi 17 na timu hiyo ya Jurgen Klopp ambao ndio vinara wa Ligi, kabla ya mchezo wa jana Jumapili dhidi ya Arsenal.

"Wakati tulipowasili hapa (mwaka 2016) kawaida ilikuwa pointi 85 kushinda taji la Ligi Kuu," alisema Guardiola.

"Sasa unatakiwa kufikisha angalau pointi 100 kushinda taji la Ligi kuu.

"Ndio maana tuliwasaidia Liverpool kufikia hatua hii, kununua wachezaji wa kiwango cha juu na sasa ndio hatua unayoweza kuifikia.

"Timu zote zilizopo nyuma ya Liverpool zinatakiwa kufikisha pointi 100.

"Ndani ya miaka 11 hakuna atakayeweza kushinda taji la Ligi Kuu mara mbili mfululizo na sisi tulifanya hivyo kwa kushinda mechi 14 mfululizo.

"Na ndio maana watu sasa wanasema hatuko vizuri, siwezi kusahau timu yake ilichokifanya.

# Moura: Naona mataji Spurs chini ya Mourinho

**LONDON,** England

LUCAS Moura anaamini Jose Mourinho anaweza kumaliza muda mrefu wa kusubiri taji kwa klabu ya Tottenham.

Mourinho ameiongoza Spurs kwenye ushindi mara nne katika mechi sita tangu alipoteuliwa kuwa kocha wa timu hiyo, akichukua nafasi ya Mauricio Pochettino.

Lucas amesema Tottenham imejiandaa vizuri kutwaa taji lao la kwanza tangu mwaka 2008 chini ya Mourinho, ambaye ameshawahi kutwaa mataji akiwa na timu kama Real Madrid, Manchester United, Chelsea, Inter na Porto.

"Kila mmoja anavutiwa kufanya naye kazi. Bila shaka yeye ni jina kubwa, na ana mchango kwa kila mmoja. Kila mmoja anajua kipaji chake, namna gani alivyo bora, kwa sababu ameshinda mataji katika kila klabu aliyofanya nayo kazi," alisema Lucas akiwaambia waandishi wa habari.

"Sasa ni nafasi kwetu sisi kujifunza kutoka kwake na tuna kila kitu tunachokitaka – kocha mzuri ambaye ana uzoefu wa kutosha. Kwa uhakika naamini anaweza kushinda taji hapa.

"Kila kocha ana mtazamo tofauti. Mara zote anazungumza na sisi, anajaribu kutuelezea mtazamo wake na kutueleza kwamba tupo kwenye klabu kubwa na sisi ni mabingwa.

"Anajaribu kutujaza hisia zake na kile tunachotakiwa kufanya katika kila hatua. Lakini hasa anataka tuwe mabingwa na tuna uwezo wa kufanya hivyo."

Wakiwa nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu, Spurs jana walikuwa wakisafiri kwenda kucheza na Wolves.






# Morata amerudi kwenye kiwango

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone anaamini kuna washambuliaji wachache kwenye soka wenye uwezo kama wa mshambuliaji wa Atletico Madrid, Alvaro Morata.

Raia huyo wa Hispania, Morata alikuwa katikati ya ushindi wa 2-0 dhidi ya Osasuna - ukiwa ni ushindi wa kwanza wa Atleti katika mechi nne za Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, na kuwarudisha kwenye nafasi ya nne katika msimamo.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea, Real Madrid na Juventus alifunga katika mechi saba mfululizo kwa klabu hiyo na nchi yake.

Simeone amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kuimarisha safu yake ya ushambuliaji kwa kudaiwa kwamba anataka kuwasajili Timo Werner, Edinson Cavani na Olivier Giroud.

"Nina matumaini sasa amerudi kwenye nafasi yake ya kufunga na kama alivyokuwa kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Alikuwa anafunga karibia katika kila mechi. Kuna watu wachache kama yeye kwenye soka ambao wanaweza kufanya kama kile alichokifanya."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# COUTINHO AISAHAULISHA BAYERN LEWANDOWSKI

●●● Kile alichokifanya kilinivutia. Tunahitaji mchezaji kama yeye. Nimefurahishwa naye...

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa muda wa Bayern Munich, Hansi Flick amesifia "kiwango cha kuvutia" kilichoonyeshwa na Philippe Coutinho wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 6-1 dhidi ya Werder Bremen, juzi Jumamosi.

**Milot Rashica aliwapa wageni uongozi ndani ya dakika 24, lakini Bayern walirudi mchezoni na kutawala baada ya Coutinho kusawazisha dakika ya 45.**

Akiwa anacheza kwa mkopo kutoka Barcelona, nyota huyo alitengeneza bao la Robert Lewandowski lililowapa vijana wa Flick uongozi katika kipindi cha pili, kabla ya yeye kufunga la tatu.

Lewandowski akafunga la nne na Coutinho akamtengeneza Thomas Muller aliyetokea benchi na kufunga la tano.

Na Coutinho akafunga bao lake la tatu na la sita kwa Bayern kwenye mchezo huo na kukamilisha ushindi huo mnono

Mfungaji anayeongoza kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Lewandowski yeye akiwa amefunga mawili, lakini kiwango cha Coutinho kilizungumzwa zaidi baada ya mchezo huo.

"Nafikiri kila mmoja uwanjani alifurahia kiwango chake," alisema Flick akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo ambao timu yake iliendelea kupata ushindi mfululizo.

"Nilijisikia furaha kwamba, timu nzima ilisherehekea pamoja naye na walionyesha kumuunga mkono kwa furaha kutoka moyoni.

"Alifunga mabao matatu na kutoa pasi ya mwisho mara mbili. Hakika alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia. Tunafuraha kubwa na kiwango chake."

Lewandowski naye alionyesha kufurahia upatina na Coutinho wakati wakiiadhibu Bremen kwenye mchezo huo.

"Ule ulikuwa ni mchezo wake leo, kwa kiwango chake alicheza soka la kuvutia kabisa," alisema mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Poland akinukuliwa na tovuti ya Bayern.

"Kile alichokifanya kilinivutia. Tunahitaji mchezaji kama yeye. Nimefurahishwa naye kwamba alionyesha namna gani alivyo mchezaji mzuri na mwenye kiwango cha juu."

Bayern watarudi tena kwenye mchezo wa Ligi Kuu Jumatano dhidi ya Freiburg.

## ZISIKUPITE

### KUMFUATA SOLSKJAER

MSHAMBULIAJI wa Red Bull Salzburg, Mnorway Erling Haaland, 19, ameweka wazi kuwa raia mwenza Ole Gunnar Solskjaer alipo Manchester United ndilo chaguo lake la kwanza kujiunga nayo Januari. ***(Star on Sunday)***

### BERGE APOTEZEA TETESI LIVER

KIUNGO wa Genk, Mnorway Sander Berge, 21, amesisitiza kuwa kichwa chake kimetulia, licha ya tetesi zinazomhusisha na kujiunga na Liverpool. ***(Sport Witness)***

### ERIKSEN AMTESA MOURINHO

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho amesema hatafunga suala la majadiliano na kiungo Mdenmark Christian Eriksen, 27, kuhusu mustakabali wake wa baadaye. ***(Sunday Mirror)***

### ZINEDINE AMFUNGUKIA MBAPPE

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amepaza sauti kuheshimiwa kwa uhusiano wake na mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, 20, huku kukiwa na tetesi kuwa straika huyo wa Ufaransa hana furaha klabuni hapo. ***(Goal.com)***

### BARCA YAMSIKILIZIA GUARDIOLA

BARCELONA inasubiri kama Pep Guardiola ataamua kuondoka Ligi Kuu England kwa mabingwa Manchester City mwishoni mwa msimu. ***(Sunday Express)***

### SANCHO AVUTA VIGOGO EPL

MANCHESTER City inajiandaa kutoa upinzani kwa mahasimu zao, Manchester United, Liverpool na Chelsea kwa kumsajili kwa mara nyingine winga Muingereza Jadon Sancho, 19. ***(Sun on Sunday)***

### ATAJWA KUMRITHI PELLEGRINI

KOCHA wa West Ham, Manuel Pellegrini bado anajiandaa kutimuliwa licha ya kupata ushindi Jumamosi dhidi ya Southampton, na kocha wa zamani, David Moyes ndiye anayepewa nafasi ya kurithi mikoba yake. ***(Star on Sunday)***

### YATAJA DAU LA ALONSO

CHELSEA imeweka dau la pauni milioni 25 kwa beki wake wa pembeni Mhispania Marcos Alonso, 28. ***(Calciomercato)***

### RODGERS ATAJWA MAN CITY

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers ni miongoni mwa wanaopewa nafasi ya kurithi mikoba ya Pep Guardiola kama Mhispania huyo ataondoka dimba la Etihad. ***(Sun on Sunday)***

### KANTE AZIITA JUVE, MADRID

KIUNGO wa Chelsea, N'Golo Kante, 28, anataka kuondoka Magharibi mwa London, lakini atapuuzia matakwa ya mchezaji mwenzake wa Ufaransa, Ousmane Dembele, 22, na kutafuta nafasi ya kujiunga na Juventus ama Real Madrid kuliko kutua Barcelona. ***(Eldesmarque)***

### HAZARD KURUDI DARAJANI

KIUNGO wa zamani wa Chelsea, Eden Hazard, 28, ameahidi kurudi Stamford Bridge pindi mkataba wake utakapomalizika Real Madrid. ***(Sun on Sunday)***

HABARI MICHEZO

## Mundu yapania kupanda Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mundu inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, imesema malengo yake makubwa msimu huu ni kuhakikisha inapanda daraja na kucheza Ligi Kuu ya Zanzibar kwa msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki, Katibu wa timu hiyo, Malik Diku alisema wamecheza Ligi Daraja la Kwanza kwa kipindi kirefu, hivyo kwa mwaka huu watahakikisha jitihada zao wanazielekeza kwa timu hiyo ili iweze kupanda daraja.

Alisema timu yake ipo vizuri licha ya kuwa na tatizo la washambuliaji hali inayosababisha kushindwa kumalizia vizuri nafasi za ufungaji wanazozipata huku akiahidi kulifanyia kazi tatizo hilo wakati huu wa dirisha dogo la usajili.

Alisema licha ya ugumu uliopo katika daraja hilo, lakini tayari wachezaji wana uzoefu wa kutosha wa daraja hilo nakusema kuwa atautumia uzoefu huo ili timu iweze kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Aidha, aliwataka mashabiki wa timu hiyo kuendelea kuipa sapoti timu yao itanaposhuka dimbani kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ambapo mashabiki walikuwa wakiujaza uwanja wakati ikicheza.

Mundu ipo nafasi ya nane kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 16 baada ya kushuka dimbani mara 11 na imebakiza mechi moja tu kukamilisha mzunguko wa kwanza.

## ZFF sasa kugeukia soka la Wanawake

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu, amesema jitihada zaidi zinahitajika katika kuhakikisha soka la wanawake linapewa kipaumbele visiwani hapa ikilinganishwa na hivi sasa.

Akizungumza na gazeti hili wiki iliyopita, alisema soka la wanawake visiwani Zanzibar kwa sasa lipo nyuma ikilinganishwa na miaka iliyopita, hivyo ni vyema wakashirikishwa wadau wa soka kuanzisha timu za wanawake ili kuweza kulinyanyua na kufikia mafanikio.

Alisema wadau wa soka visiwani Zanzibar wamehamasika zaidi katika timu za wanaume, hivyo ZFF itaandaa mkakati shirikishi ili waweze kuwa na timu za wanawake zitakazosaidia kupatikana timu za taifa ambazo zitawakilisha nchi katika mashindano mbalimbali ambayo Zanzibar wanashiriki.

Aidha, alisema ZFF katika mkakati wake wa kulinyanyua soka la wanawake visiwani Zanzibar tayari limeandaa mpango mkakati utakaoweza kupata timu kuanzia ngazi za chini ili kupata vipaji ambavyo vitaendelezwa na kufikia malengo husika.

"Tuna timu chache za wanawake, ambapo kwa sasa zipo nne tu, inabidi tufanye jitihada za kuhamasisha wadau kuanzisha timu za wanawake ili tuweze kucheza Ligi ya Wanawake msimu unaofuata na matumaini yangu tutafanikiwa," alisema.

# CECAFA YAMZUIA STRAIKA MGANDA

**Na Mwandishi Wetu,** JINJA

BARAZA la Soka Afrika Mashariki na Kati ( Cecafa), limemsimamisha mchezaji wa Uganda, Nacakwa Simalei, kuendelea kucheza katika mashindano ya Kombe la Chalenji kwa wasichana wa umri chini ya miaka 17, kutokana na afya yake kutokuwa imara.

**Simalei alidondoka na kupoteza nguvu katika mechi dhidi ya Burundi na hali hiyo ilijitokea tena walipoivaa Djibouti.**

Taarifa za awali zinaonyesha kuwa mshambuliaji huyo anasumbuliwa na maradhi ya moyo, na hivyo Cecafa inataka kuona anafanyiwa vipimo zaidi ili kutambua tatizo halisi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya Cecafa (U-17), Doris Petra, alisema uamuzi huo wa kumsimamisha mchezaji huyo umefanywa na kamati yake kwa faida ya kuokoa maisha ya nyota huyo.

Petra alisema wanaamini vipimo atakavyofanya na matibabu atakayopewa, yataimarisha na kuokoa afya yake na atarejea kuisaida Uganda.

"Hatutaki kuona hali inakuwa mbaya zaidi, imetokea mara mbili kwa mchezaji mmoja, hatujui nini kitatokea siku nyingine, kama ni mchezaji muhimu, anatakiwa kutibiwa kwanza na baadaye ushauri ya kitaalamu kutoka kwa madaktari," alisema Petra.

Mechi atakazokosa mchezaji huyo ni dhidi ya Tanzania Bara ambayo ilichezwa jana jioni na mchezo wa mwisho wa mashindano haya utakaochezwa kesho dhidi ya Kenya.




Waombolezaji wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Katibu wa Baraza la Wazee wa Yanga, Ibrahim Akilimali, kuelekea Msikiti wa Barakati Tandale kwa ajili ya kumsalia na baadaye kuzikwa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNEJUMA**

## *Tanzania Bara, Uganda hakuna mbabe*

**Na Somoe Ng'itu,** JINJA

TIMU ya soka ya wasichana ya umri chini ya miaka 17 ya Tanzania Bara, imelazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya wenyeji Uganda katika mechi ya mashindano ya Kombe la Chalenji iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Njeru mjini hapa.

Kwa matokeo hayo, Uganda, ambayo nayo haijapoteza mchezo hata mmoja imefikisha pointi 10 wakati Tanzania Bara inayofundishwa na Bakari Shime imefikisha pointi nane.

Uganda itamaliza mashindano hayo kesho Jumanne kwa kucheza dhidi ya Kenya wakati Tanzania Bara wao watamaliza na Djibouti ambayo imepoteza mechi zake nne zilizotangulia.

Tanzania Bara ndio ilikuwa ya kwanza kufunga bao kupitia kwa Aisha Masaka dakika ya 20 na wenyeji walisawazisha kwa penalti iliyopigwa na Najemba Fauzia dakika 34.

Katika mechi ya mapema asubuhi jana, Eritrea ilipata ushindi wa kwanza kwa kuwafunga Djibouti mabao 4-0 wakati Kenya ilipata ushindi wa 3-2 dhidi ya Burundi, mchezo ambao ulikuwa na ushindani kwa pande zote mbili.

Mechi nyingine ya mashindano hayo yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa) na kudhaminiwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), itakuwa ni kati ya Eritrea dhidi ya Burundi.

# Michezo



Jumatatu Desemba 16, 2019
Nipashe

**Coutinho aisahaulisha Bayern Lewandowski** HABARI UK.30

**JARIBIO...**



Mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi, akijaribu kufunga kwa kichwa katika mechi ya LaLiga iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Anoeta na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2. Mabao ya Barca yalifungwa na Antoine Griezmann na Luis Suarez huku Mikel Oyarzabal na Alexander Isak wakitupia kwa upande wa wenyeji. **PICHA: MTANDAO**

# SVEN AIBUA VITA KALI HUKO SIMBA

●●● Ashikilia namba kikosi cha kwanza, wachezaji mazoezini ni vita ya kutupia kukaba huku usajili...

**NA Mwandishi Wetu**

LICHA ya takriban siku tatu kuwa mshuhudiaji tu wa mazoezi ya timu yake kutokana na kutokuwa na kibali cha kufanya kazi nchini, huko mazoezini unaambiwa Kocha Mkuu mpya, Mbelgiji Sven Ludwig Vandenbroeck aimeibua vita kali ya kila mchezaji kutaka kujimwambafai uwezo wake.

**Katika soka mara nyingi huwa ni kawaida anapotua kocha mpya, namba zote zinakuwa hazina mwenyewe na kila mchezaji hutakiwa kupambania nafasi ya kuanza kwa kuonyesha uwezo wake mazoezini.**

Hilo ndilo linalotokea kwa sasa katika mazoezi ya Simba, ambayo kwa sasa ipo chini ya benchi jipya la ufundi kutokana na aliyekuwa Kocha Mkuu, Patrick Aussems kutimuliwa na nafasi yake kurithishwa na Mbelgiji mwenzake, Sven huku nafasi ya Kocha Msaidizi kwa sasa akiwa ni Selemani Matola baada ya klabu hiyo kufikia makubaliano ya pamoja ya kuvunja mkataba na Denis Kitambi aliyekuwa akimsaidia Aussems.

Katika mazoezi ya Ijumaa, baada ya yale ya viungo, timu hiyo ilicheza mechi kwa kuwagawa wachezaji katika timu mbili, ambapo walionyesha soka la nguvu kama vile mechi ya mashindano, hata hivyo kilichovutia zaidi mashabiki si hat-trick iliyopigwa na mshambuliaji Meddie Kagere, bali ni uwezo wa Francis Kahata wakati akitupia mawili kwa kumtungua Benno Kakolanya. Lakini beki Mbrazil Tairone Santos aliyekuwa akicheza timu moja na Kahata, alikuwa na shughuli pevu dhidi ya Kagere ambaye alikuwa akilishwa mipira na Ibrahimu Ajibu.

"Unajua hapa Matola kafanya la maana sana kwani kocha mkuu anaweza kuwaona na kuelewa uwezo wa kila mchezaji pindi atakapoanza kuinoa rasmi na angalia kila mchezaji anavyoonyesha kupambana," alisema shabiki wa Simba, aliyejitambulisha kwa jina la Miraji Shahibu.

Aidha, chanzo chetu ndani ya Simba kililiambia Nipashe kuwa, Sven ameitaka klabu hiyo kumwandalia mechi moja ya kirafiki kabla ya kuivaa Lipuli Desemba 24, mwaka huu ili aweze kuwasoma wachezaji wake vizuri.

"Kocha anataka atakapoanza baadaye apate mechi moja ya kirafiki ili kuweza kuwasoma wachezaji wake na kuwaelewa vizuri kabla ya kucheza na Lipuli baadaye mwezi huu, tunaamini hilo litafanikiwa pindi tu atakapokuwa tayari," kilieleza.

Kuhusu usajili wa dirisha dogo ambalo limefunguliwa rasmi leo, chanzo chetu kililiambia gazeti hili kuwa kwanza kocha amehitaji ripoti ya kila mchezaji kwanza na muda wa kuwaelewa wachezaji wote hasa ukizingatia wengine wapo na kikosi cha Tanzania Bara kwenye michuano ya Chalenji nchini Uganda.

"Hilo kwa kocha mpya ni mapema kwa sababu hawaelewi wachezaji wake wote ila kwa sababu yupo na Matola ambaye anaijua vema Simba pamoja na kocha wa viungo [Mtunisia Adel Zrane], wanaweza kumshauri nini cha kufanya," kilisema chanzo chetu huku kikiomba hifadhi ya jina lake.

Hata hivyo, licha ya mashabiki wengi kuendelea kujitokeza kushuhudia mazoezi ya timu hiyo, tayari imeelezwa changamoto kubwa katika Uwanja wa Simba Mo Arena ni kutokuwa na ukuta jambo ambalo Kocha Sven anataka kuwapo na utulivu wakati wa mazoezi.

## Kilimanjaro Stars kuivaa Uganda kivingine

**Na Somoe Ng'itu,** UGANDA

BAADA ya timu yake kuingia hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la Chalenji yanayoendelea nchini hapa, Kocha Mkuu wa Kilimanjaro Stars ya Tanzania Bara, Juma Mgunda, amesema wataingia na mbinu tofauti kuwakabili wenyeji Uganda katika mchezo huo utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa KCCA jijini Kampala.

Kilimanjaro Stars ilimaliza katika nafasi ya pili ikiwa na pointi nne nyuma ya vinara wa Kundi B, Kenya ambao wamemaliza hatua ya makundi kwa kushinda mechi zote tatu, Zanzibar (Zanzibar Heroes) na Sudan, ndio zimeyaaga mashindano hayo kutoka kwenye kundi hilo.

Katika Kundi A, tayari wenyeji wenye pointi tisa, wameshaongoza kundi hilo hata kabla ya kumaliza mechi za mwisho jana jioni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda, alisema anatarajia mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani kwa sababu timu zote zinaundwa na wachezaji wenye uzoefu na mashindano haya.

Mgunda alisema atawaandaa wachezaji wake kuingia uwanjani kwa tahadhari kwa sababu wanahitaji kupata matokeo mazuri na hatimaye kutinga fainali.

"Tunajua mechi ijayo itakuwa ngumu, yenye ushindani, lakini tutacheza kwa mipango na mikakati tofauti, tunahitaji kupata ushindi na si matokeo mengine, tutajipanga kupambana hadi mwisho," alisema Mgunda.

Aliongeza kuwa wachezaji wake wanaendelea kuimarika na kucheza katika kiwango cha juu ili kuhakikisha wanatimiza malengo yao waliyojiwekea wakati wanakuja kwenye michuano hii.

"Tunamshukuru Mungu tumepata nafasi hii, katika kundi letu timu zote zilikuwa na nafasi ya kusonga mbele, sasa tunakwenda kucheza na wenyeji (Uganda), itakuwa mechi ngumu, yenye ushindani, lakini yote kwa yote tutaingia kupambana mpaka dakika ya mwisho," alisema Mgunda.

Aliongeza kuwa wanahitaji kuongeza umakini kwa kutumia vizuri nafasi zote watakazozitengeneza katika mechi hiyo ya hatua ya nusu fainali, tofauti na ilivyojitokeza kwenye mhezo wao dhidi ya Sudan ambao ulimalizika kwa sare ya bila kufungana.

Mara ya mwisho kwa Kilimanjaro Stars kutwaa ubingwa wa mashindano hayo ya Chalenji ilikuwa mwaka 2010, wakiwa nyumbani jijini Dar es Salaam baada ya kuwafunga Rwanda (Amabuvi), mabao 2-1.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002